# TUKUTANE MJINI

**“ Katika mwaliko wa kuurithi uzuri wa Mji ule *si salama kukawia* maana unaweza usiusikie tena”**

**UFUNUO 14:6-12**

**Lugha za kibinadamu hazitoshi hata kujaribu kusimulia jinsi Mbingu ilivyo. Uzuri wa Nchi ile utaeleweka tu kwa wale watakaoiona,**

JEREMIA M.K MEI 2015

SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa karama zake alizowatunuku wanadamu ili wazitumie kwa utukufu wake. Nawashukuru wote wanaothamini kazi ya Roho mtakatifu inayoendelea Duniani. Nawashukuru wote waliokuwa wanaomba usiku na mchana ili kitabu hiki kikamilike. Namshukuru Mke wangu Bachita Msilu kwa Mchango mkubwa alioutoa ili kukamilisha kazi hii. Namshukuru Mhariri kwa kazi yake nzuri ingawa hakutaka jina lake liandikwe katika kitabu hiki.

Ninawaombea maelfu watakaosoma kitabu hiki kwamba kama tusipoonana katika dunia hii ya shida, tukutane mjini pale ng'ambo kwenye bahari ya kioo ambapo shida, vifo na magonjwa vitakoma milele. Kwa hakika tutasimulia ajabu za pendo la yule ambaye tangu kale aliapa kutukomboa na kuhakikisha kwamba hatatulia mpaka mimi na wewe tumeirithi nchi mpya. Hakuna lugha ya mwanadamu yeyote mwenye roho ya kufa anayeweza kusimulia utukufu wa Mji ule. Kitabu hiki ni barabara ya kukufikisha katika makao ya nuru.

Wale watakaofanikiwa kukisoma kitabu hiki na kuthibitisha kila fungu wakilinganisha andiko kwa andiko watakuwa wamejipatia kidonge cha uhai. Hatimaye nuru ing'aayo itawazukia. Watakapoitii nuru hiyo takatifu watajikuta wanapita njia nyembamba na kuwaongoza wengine kuifikia mede ya thawabu ambayo wengi wataikosa kwa sababu ya upofu wa kiroho, kutotubu, kutoamini na kiburi cha uzima.

..............................................................................................................................................

***HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA***

***Ruhusa imetolewa kukichapisha,kudurufu na kukisambaza bure kitabu hiki ikiwa tu kitatolewa kama kilivyo bila mabadiliko wala kuongeza maoni yeyote.***

***Mawasiliano +255715 64 77 65 +255756 64 77 65 mkiselema@ymail.com***

..............................................................................................................................................

YALIYOMO

SURA UKURASA

Utangulizi…………………………………………………………………....4

1. Waliopotea watapotea…………………………………………….........5

2. Kuchagua ni kujitenga…………………………………………….........12

3. Mimi niko ambaye niko………………………………………………....20

4. Njia kuu……………………………………………………………………..29

5. Hila za shetani…………………………………………………………….55

6. Lugha ya shetani…………………………………………………………60

7. Urembo wa kweli…………………………………………………………64

8. Madhara ya nyama………………………………………………………75

9. Kanisa la Dictionary……………………………………………………….81

10. Picha ya shetani…………………………………………………………...91

11. Chombo cha shetani……………………………………………………..97

12. Shetani na Maiti…………………………………………………………...103

13. Uchawi kanisani…………………………………………………………..110

14. Madaraja ya Imani………………………………………………………114

15. Mwisho wa Dunia………………………………………………………...117

16. Tukutane mjini……………………………………………………………...122

Vitabu vya rejea…………………………………………………………131

# UTANGULIZI

Kuna watu wanaowazuia watu wasiifikie nchi ya ahadi na wao wenyewe hawaiingii. Hivi karibuni kitatokea kitu cha kusisimua sana. Malumbano yale ya zamani yataanza tena. Karani wa shetani sasa yupo ofisini akiratibu hatima ya mwisho kwa wale watakaoikataa bendera yake. Karani ametengeneza kadi ambayo nakala zake zitasambazwa dunia nzima. Wakati hayo yanaendelea Malaika wa rehema nao wanakunja mabawa kuondoka zao. Picha halisi itakapoanza itafanya watu wajute kwa nini hawakufa mapema. Mkono unaosukuma hayo ni wa shetani kupitia Ukristo bandia. Injili inayopelekwa ulimwenguni sasa si ile ambayo Yesu aliiagiza tuipeleke. Kuna Injili ya shetani inahubiriwa duniani.

Mungu halazimishi mtu yeyote amuabudu, amekusudia kuwa kila mwanadamu aamue kwa hiari yake kumtumikia au kumkataa kabisa. Mungu hatabadili sheria yake ili kumuokoa mwanadamu aliyeshindwa kuitii. Mungu ana watu duniani ambao ni watii na waaminifu kwake wanaomheshimu na kumthamini kuliko kitu chote duniani.

Mungu hana haja ya watu wenye Roho ya kusitasita wanaotangatanga katika njia mbili. Mungu hana haja na mtu ambaye anaujua ukweli lakini haupeleki kwa wengine. Mungu hana haja na mtu ambaye anahubiri mambo yaliyomshinda kuyatenda. Mungu hana haja ya uzuri wa mavazi kama ambavyo ana haja ya moyo safi uliotakaswa. Mungu hana haja ya dini yoyote kama ambavyo ana haja na mtu yeyote mwaminifu.

Mungu hana haja ya umoja wa aina yeyote unaodharau mahusia yake kuliko ambavyo ana haja na utengano ambao unamtukuza. Mungu hafurahishwi na yeyote anayeishi huku anamkataa kuliko ambavyo ana haja na yeyote atakayekufa kwa ajili ya kutetea neno la Kristo. Mungu hana haja na Mapadre maaskofu mashehe na wachungaji wanaosaliti kazi yake kuliko ambavyo ana haja na watu binafsi waaminifu ambao sasa wamejitoa kuutangaza ukweli wa Mungu kwa uaminifu.

Hitaji kuu la ulimwengu, ni hitaji la watu. Watu ambao hawatanunuliwa wala kuuzwa, watu ambao ndani ya nafsi zao hasa ni waaminifu na wa kweli. Watu ambao hawaogopi kuitaja dhambi kwa jina lake. Watu ambao dhamiri zao zina uaminifu kwa wajibu kama dira ionyeshavyo ncha ya kaskazini. Watu watakaosimamia ukweli hata kama Mbingu zinaanguka. *Ellen G. White – Education p 57.*

## SURA YA KWANZA

## WALIOPOTEA WATAPOTEA

Yaliyokuwako ndiyo yatakayokuwako na yaliyotendeka ndiyo yatakayotendeka wala jambo jipya hakuna chini ya jua. Je! Kuna jambo lolote ambalo watu husema juu yake tazama ni jambo jipya? Limekwishakuwako tangu zamani za kale zilizokuwa kabla yetu sisi. (*Muhubiri 1:9-10, 3:15)*

Tunakwenda kuchunguza historia ya wokovu na makundi mbalimbali ya watu waliodai wanautafuta wokovu lakini mwisho wakajikuta wamepotea ama kwa kujua au kwa kutokujua. Ipo njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu lakini mwisho wake ni njia za mauti. *(Mithali 16:25)* katika siku hizi za mwisho watu wa Mungu watakabiliwa na hatari zilezile zilizowapata Israeli wa zamani.Wale ambao hawatapokea maonyo atoayo Mungu wataanguka katika hatari zilezile kama ilivyowapata Israeli wa zamani hata wakakosa kuingia katika raha kwa kutokuamini. Israeli wa zamani walipatwa na misiba kwa sababu ya mioyo yao isiyotakaswa na nia zao za kutojiweka chini ya Mungu, kukataliwa kwao kama Taifa,kutotubu, upofu wa akili, na ugumu wa mioyo viliwafanya waikose nchi ile njema. Katika historia yao tunayo ishara ya hatari ikituonya mbele yetu.

Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo, bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani nao waionao ni wachache *(Mathayo7:13-14)* Huu ni ujumbe kutoka kwa Yesu mwenyewe tunaopaswa kuutii na kuihubiri maana yake kwa ulimwengu. Hii ni kazi ya kwanza kwa kila Muhubiri wa neno la Mungu Ulimwenguni. Injili ya shetani inayowaelekeza watu wamuamini Yesu kwa sababu kwa Yesu ni tambarale bila Milima ni kinyume na maneno ya Yesu mwenyewe. Ingekuwa vizuri kama nini ikiwa yule Muhubiri wa kwanza angewafundisha kwa uaminifu hawa waongofu mambo ya muhimu hata kama ni wachache tu wanaoingia kanisani. Mungu angependa kuwa na watu *sita* walioongoka kuliko watu *sitini* ambao hawajaongoka kabisa *(Ellen G. White- Gospel Workers p. 370)*

## MUNGU HUTUMIA WATU WALIO NJE YA MFUMO

Sauti ya taharuki ya matukio makubwa ya wokovu kwa kila kizazi kilichopita haijatokea ndani ya mfumo wa madhehebu ambako kuna mfumo wa madaraka, watu wa kawaida tu ndiyo waliotoa ujumbe wa taharuki ili kuwaamsha waliolala kiroho.

1. *Swali:* Wakati Yesu anazaliwa kulikuwepo na Madhehebu yaliyokuwa na mfumo wa uongozi wa dini ya kiyahudi. Kundi hili halikusadiki habari za kuzaliwa kwa Yesu. Je ni nani aliyeleta taarifa hizo Kule Yerusalemu?

Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za Mfalme Herode, tazama mama Jusi wa mashariki walifika Yerusalemu wakisema, yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona Nyota yake Mashariki nasi tumekuja kumsujudia *(Mathayo 2:1-22 Luka 2:8-18)* Makuhani na Walimu wa kiyahudi walikuwa wakishughulika na Dini yao tu huku wakiwatenga Wagiriki na Warumi wakiwalaumu kuwa ni wenye dhambi, walisema kuwa isingewezekana Mungu awapite wao na kuzungumza na Wachungaji wajinga wasiotahiriwa, hawakujishughulisha hata kwenda Bethlehemu kuona kama habari hizo ni za kweli. Hivyo wakawaongoza watu waone kuwa habari za kuzaliwa kwa Yesu ni hadithi tu za kuchekesha. Hapa ndipo ulikuwa mwanzo wa kumkana Yesu kwa Mafarisayo na Marabi. Ukaidi wao ulikua na kuwa chuki ya kumchukia Mwokozi *(DA 61-62, Tumaini La Vizazi Vyote Ukurasa 29-30, GC313)*

2.Swali:- Je ikiwa Makuhani, Marabi na viongozi wa dini hawakuamini habari za kuzaliwa kwa Yesu ni nani angetambulisha huduma ya Yesu?

Yohana alitokea nyikani na kuhubiri Ubatizo wa Toba iletayo ondoleo la dhambi akahubiri akasema, yuaja nyuma yangu aliye na nguvu kuliko mimi ambaye mimi sistahili kuinana na kuilegeza gidamu ya viatu vyake *(Marko1:4,7)* Sauti ilisikika Jangwani ambayo ni kali ya kushtusha lakini imejaa tumaini ikisema, Tubuni kwa maana ufalme wa Mbinguni umekaribia. Yohana alikemea dhambi kwa uwezo wa nguvu za Eliya. Maneno yake yalikuwa dhahiri na yenye nguvu. Taifa lilitaharuki, makundi ya watu walifurika kwenda jangwani (*DA104, Tumaini la vizazi vyote ukurasa 50)*

3. Swali:-Makuhani wa Israeli waliwahi kupoteza maana ya Ukuhani wakatenda maovu huku wakiwaacha wengine kudumu dhambini. Je, Wakati Uovu wa Ahabu na Yezebeli ulipokithiri sana katika Taifa ni nani alitoka nje ya Mifumo ya Dini na kutoa maonyo makali mbele ya Mfalme?

Basi Eliya Mtishibi wa Wageni wa Gileadi akamwambia Ahabu, kama Bwana, Mungu wa Israeli aishivyo ambaye ninasimama mbele zake, hakutakuwa na umande wala mvua kwa miaka hii ila kwa neno langu tena.*1Wafalme 17:1, 18:1-46* Eliya hakujulikana kwa sifa yeyote wala kuishi katika mji maarufu lakini aliingia katika kazi ya Mungu akiwa na Roho

nyenyekevu. Alipoona Waisraeli walivyozidi kuzama maovuni katika Ibada ya Sanamu, Roho yake ilisikitika mno akawa na uchungu mwingi. Katika kinywa chake mlitoka neno la imani na nguvu. (*PK119*)

4. Swali:- Kisa cha Wanawali kumi ni fundisho kwetu. Kwa kuwa Wakati wa usiku wa manane Wanawali wote walikutwa wamelala, Je ni nani kutoka nje aliyewaamsha usiku huo watengeneze taa zao?

Hata Bwana arusi alipokawia wote wakasinzia wakalala usingizi, lakini usiku wa manane pakawa na kelele, haya Bwana arusi tokeni mwende kumlaki, mara wakaondoka wanawali wote wakazitengeneza taa zao. *Mathayo 25:5-7* "Wakati ilipotangazwa kwa sauti kuu usiku wa manane kwamba tazama bwana arusi anakuja tokeni mwende kumlaki na wanawali walipoamka kutoka usingizini, ndipo pande zote zilikabiliwa na kutokujua (kutotegemea) lakini upande mmoja ulikuwa umejiandaa kwa dharura" (*COL 42, Vielelezo vya Mafundisho ya Kristo uk 325)*

5.Swali:- Sauti (kutoka nje) ya kilio cha usiku wa manane inatufundisha nini?

Maana ndugu zangu angalieni mwito wenu ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu. Si wengi wenye cheo walioitwa bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia ili awaaibishe wenye hekima, tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaibishe vyenye Nguvu, tena Mungu alichagua vitu vinyonge vya dunia vinavyodharauliwa, naam vitu ambavyo haviko ili avibatilishe vile vilivyoko. *1Wakorintho 1:26-28, 1wakorintho 3:18-20.* "Katika Madhehebu yote tokea siku za Mitume hakuna Dhehebu lililokuwa huru kutoka katika dhambi na hila za shetani. Watu wa kawaida tu ndiyo walioitikia mwito mara ya kwanza wala sio watu Wataalamu. Wakulima waliacha mavuno yao mashambani, Mafundi wakaacha vyombo vyao wote wakaondoka kwenda kulitangaza neno la Mungu, kwa kawaida Makanisa hayakujali ujumbe huu na wale walioupokea *walifutwa* katika Makanisa hayo. Wale wasioamini waliokuja kujiunga na watu wa marejeo waliona kuwa kuna uwezo mkuu katika ujumbe huu wa haya! Bwana arusi yuaja! *(GC402, Pambano kuu toleo la mwaka 1992 sura ya 22 ukurasa wa 229*.

6. Swali:- Je, Mungu kutumia watu wa tabaka lipi ili wafanye kazi yake?

Wakati huo Yesu akajibu akasema, nakushukuru Baba BWANA wa Mbingu na Nchi kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili ukawafunulia watoto wachanga *Mathayo 11:25,marko 10:21. Mathayo 4:18-22* "Mungu hachagui mtu Mkuu wa Dunia ili awe Nabii au Kuhani, bali huteua watu wa hali ya chini, watu wa kawaida ambao hudharauliwa na watu hata wachungaji kama Amosi, katika kila kizazi watakatifu wa Mungu iliwapasa kukemea hata Wafalme, watu wakuu na Watawala na wenye hekima ili wasiangamie dhambini *(GC142-143,Pambano kuu sura ya 7 ukurasa 84 )*

7.Swali: Kwa nini Mungu hapendelei kuwatumia watu Wakuu ili waifanye kazi yake?

“ Sababu inayofanya Mungu asiwachague watu Wakuu na wenye elimu ili kuongoza watu wake ni kuwa, wao hawamtegemei Mungu ila hutegemea ukuu na elimu yao na kujiona kuwa hawana haja ya kuongozwa naye.Watu ambao wana ujuzi mdogo huitwa mara kwa mara ili waeneze neno lake.Si kwamba hutoelimika kwao ndiko kunampendeza Mungu bali katika hali yao huwa hawana la kujisifia wasifundishwe na Mungu. Unyenyekevu wao na Utii huwafanya kuwa Wakuu. *(GC456, Pambano Kuu sura ya 26 ukurasa wa 262*)

Kama iliyokuwa miaka ya zamani ukweli wa pekee kuhusu wakati huu haupatikani kwa wakuu au viongozi wa Makanisa bali kwa Waume na Wake ambao hawajaelimika kiasi cha kutolijali neno la Mungu.*COL.79.*

8. Swali:Njia pana na njia nyembamba zinatumika Duniani hata sasa. Je, Watu ambao Mungu huwatumia mara zote hupita mapito yapi ambayo kila Mkristo wa kweli atayapitia?

Lakini wengine waliumizwa vibaya hata kuuawa wasikubali ukombozi ili wapate ufufuo ulio bora, wengine walijaribiwa kwa Dhihaka na Mapigo naam kwa Mafungo na kwa kutiwa gerezani, walipigwa kwa Mawe, walikatwa kwa Misumeno, walijaribiwa waliuawa kwa Upanga, walizungukazunguka wakivaa Ngozi wakiteswa na kutendwa mabaya. Watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao, walikuwa wakizungukazunguka katika Milima na katika Mapango na katika Mashimo ya nchi (*Waebrania 11:35-38)*

“Si mapenzi ya Mungu kuwa wachungaji wake wawe Matajiri maana Shina la mabaya yote ni kupenda Fedha. Mchungaji ambaye amejitoa wakfu kabisa kwa Mungu hukataa kujishughulisha na biashara ambayo itamzuia asijishughulishe na mwito Mtakatifu. Hatajipatia heshima au Mali ya Duniani. Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia ili ampendeze yeye aliyemwandikia awe askari. Hata mtu akishindana katika Machezo hapewi taji asiposhindana kwa halali.(*GW339-340, Wajumbe wa Kristo ukurasa 106, 2Timotheo 2:3-5)*

9. Swali:- Ni kitu gani cha kujihadhari alichokisema Yesu kuhusu Manabii wa uongo wa siku za mwisho waliopo kwenye Madhehebu yanayotuzunguka?

Jihadharini na Manabii wa Uongo, Watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo walakini kwa ndani ni Mbwa mwitu Wakali, mtawatambua kwa matunda yao. *Mathayo7:15-16, Yuda 1:4* “Katika njozi ile ya mwisho nilionyeshwa ukweli unaoshangaza sana kwamba ni sehemu iliyo ndogo tu ya wale wanaokiri ukweli ambao wametakaswa nayo na kuokolewa. Niseme nini kuwaamsha watu wetu? Nawaambieni

ni Wachungaji wengi wanaosimama mbele za Watu kufafanua Maandiko walio wachafu. Mikono yao ni michafu, mioyo yao imejaa ufisadi, *(1T608, 5T78)*

10 Swali: Wanaotangaza ujumbe wa kweli wa mwisho watatofautiana na walioasi. Imani, msimamo na mafundisho yatakuwa dhahiri yanayogusa dhambi kama yale ya Eliya, Yohana Mbatizaji na Stefano. Je, Madhehebu yaliyopotoka ya walioasi yatawatenda nini?

Maneno hayo nimewaambia msije mkachukizwa, watawatenga na Masinagogi, naam saa yaja atakapodhania kila awauaye ya kuwa anamtolea Mungu ibada. Na hayo watawatendea kwa sababu hawakumjua Baba wala Mimi, *Yohana16:1-3,14:29,15:18-21* "Mabishano yale yale bado yanaendelea. Kwa wote wanaoeneza ukweli wa neno la Mungu kila mara maswali hutokea, ni nani hawa wanaojidai kutangaza mafundisho haya mapya? Kwanza hawana elimu ni wachache kabisa nao ni Watu duni tu. Hata hivyo wanasema kuwa wanao ukweli na kwamba wamechaguliwa na Mungu. Ni wajinga kabisa na wamedanganyika. Je, Kanisa letu linalinganishwaje nao kwa umaarufu na kwa wingi? Mashindano ya jinsi hii hayatofautiani na yale ya wakati wa Luther. *(GC148,Pambano Kuu sura ya 8 ukurasa 188.)*

FUNDISHO MUHIMU

Kulikuwa na uasi na udanganyifu mwingi katika Madhehebu ya zamani uliopelekea viongozi wao kumkataa Masihi wakati wa kuzaliwa kwake. Uasi huo umerejea tena katika siku zetu kama ulivyokuwa. Mwokozi aliwaacha wayahudi akawageukia watu wengine watakaofanya kazi yake kikamilifu ili ufalme wake ujengwe. Tukio hilo linajirudia sasa kama lilivyokuwa awali, Usisahau kuwa Eliya aliitwa kuwa ni mtaabisha Israel, Yeremia aliitwa ni msaliti, Paulo aliitwa kuwa ni mchafua hekalu. Tangu wakati huo mpaka sasa wale wanaoitetea kweli wamenenwa kuwa ni Wahaini, Wazushi, wenye faraka. Watu walioitwa na Mungu kupelekea ujumbe kwa wanadamu watapata mapingamizi. Wanaotangaza ukweli wa wakati huu wasitazamie kuwa utapokewa na watu wengi zaidi ya ulivyopokewa hapo mwanzo. Mapambano kati ya ukweli na uongo yataendelea mpaka mwisho wa wakati.( *.(GC459, Pambano Kuu sura ya 26 ukurasa 263.)Yohana 15:19-20 Luka 8:26)*

| YALITOKEA ZAMANI | YANATOKEA SASA |
| --- | --- |
| Alikuja kwao lakini hawakumpokea. *Yohana 1:11* | Aliwatumia Biblia lakini wameikataa *2Timotheo 4:3-4* |
| Walivaa mavazi ya kondoo kumbe ni Mbwa mwitu wakali.*Mathayo 7:15-16* | Wanamkiri kwa vinywa tu na kumkana kwa matendo yao. *Tito 1:16* |
| Walipenda giza kuliko nuru. *Yohana 3:19*. | Wanapenda Pesa kuliko Mungu. *2Timotheo 3:2* |
| Waliwaua manabii waliotumwa kwao. *Mathayo 23:37* | Watawatenga, watawasaliti na kuwaua. *Yohana 16:1* |
| Wachungaji Walikula roho za Watu.*Ezekieli 22:25*. | Roho za wanadamu zitafanyiwa biashara.*Ufunuo18:9-13* |
| Ninyi ni wa baba yenu Ibilisi.(*Yohana 8:44)* | Odokeni kwangu siwajui kamwe. *Mathayo 7:22-23* |

Wengi watajiingiza kwenye Msafala wa Mapepo pasipo kujua!!..Mawazo ya wataalam na tafsiri potofu za Biblia wanazoeleza baadhi ya Wanasayansi pamoja na mashauri yanayoamuriwa na mabaraza ya Madhehebu kwa kura za wengi hata mojawapo lisingefikiriwa kuwa ni ushahidi wa mafundisho ya Mbinguni. Sisi tungeshikilia kuwa je, ndivyo asemavyo Bwana?

Tumezungukwa na Mbwamwitu wakali kuliko wakati wowote wa historia ya Dunia hii. Vita baina ya wema na uovu imekaribia sana ukingoni. Yale ambayo shetani alikuwa anayafanya akiwa anatembea sasa anayafanya akiwa anakimbia. Mawakala wa shetani wanapatikana katika mimbari za madhehebu leo wakisimama na kuhubiri udanganyifu na uongo kwa watu wetu *(TM409)*. Hii ina maana gani? maana yake Makao makuu ya shetani sasa yapo katika Ndimi za Wachungaji na Viongozi wa Madhehebu wanaosimama Madhabahuni. Wale wanaowasikiliza tu bila kujisomea wenyewe watajikuta wapo kwenye kundi la wanawali wapumbavu wakilia na kuomboleza. Je, hili litawezekanaje? Vuta usikivu wa historia ya Wayahudi katika fungu lifuatalo kutoka katika Roho ya Unabii.

"Wakati Mungu alipowaacha Wayahudi, wao pamoja na Makuhani wao bado walikuwa wakijihesabu kuwa ni wapendwa wa Mungu. Huduma za Kanisa zilikuwa zinaendeshwa kama kawaida, kila siku waliomba Baraka kwa Mungu kama watu watauwa na hali wamejaa uharibifu wakiwa na hatia ya Damu ya Mwana wa Mungu. Hali kadhalika mstari wa ulimwengu huu utakapokuwa *umepigwa na Kesi yake imekatwa milele*, wenyeji wa ulimwengu *hawatatambua* hata kidogo!, aina za Ibada ambazo hazina msingi zitakuwa zinaendeshwa kimtindo na watu ambao

MUNGU hayumo kati yao. Shetani ndiye atakuwa akiwaongoza ili kukamilisha kusudi lake la udanganyifu.(*GC615, Pambano Kuu sura ya 39 ukurasa 350)*

Ni huzuni inayochoma moyo. Ni huruma ile ile iliyopelekea Yesu kuulilia mji wa Yerusalemu ndiyo tunaihitaji itunusuru, kwa maana Sasa tunaelekea katika wakati huu mkubwa wa historia yetu. Mji wa Yerusalemu ni mfano vile Kanisa litakavyokuwa litakapokataa Nuru iliyotolewa na Mungu. Yerusalemu ndipo Mungu alikuwa amefanya hazina yake. Lakini watu wake walipotosha ukweli na kupuuza Maonyo. Hawakuheshimu mawaidha ya Mungu. *Ellen G. White – Testimonies for the church volume 8 uk 67.*

## SURA YA PILI

## KUCHAGUA NI KUJITENGA

Angalia nimekuwekea leo mbele yako Uzima na Mema, Mauti na Mabaya, nazishuhudia Mbingu na Nchi juu yenu hivi leo kuwa nimekuwekea mbele yako Uzima na Mauti, Baraka na Laana, basi chagua uzima ili uwe hai wewe na uzao wako *(Kumbukumbu la Torati 30:15-19)* Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakayemtumikia kwamba ni Mungu yule ambaye baba zenu walimtumikia ng'ambo ya Mto au kwamba ni miungu ya wale waamori ambao mnakaa katika nchi yao. Lakini Mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana.*(Yoshua 24:15)*

Historia takatifu ni fundisho la vizazi vyote. Katika sura hii tutajifunza kuhusu *uhuru wa kukiri na kuchagua na ulazima wa kujitenga.* Tumepewa uhuru wa kuchagua kumtumikia Mungu au shetani. Shetani atakuwa baba yetu endapo tumeamua kumtumikia, vivyo hivyo Mungu ndiye atakuwa Baba kwetu ikiwa tutachagua kumtumikia. Pande zote mbili zina masharti yake ambayo utalazimika kuyafuata.Uchaguzi ni wa hiari lakini kufuata masharti ya uchaguzi wako ni lazima.Mojawapo ya masharti yanayohusika pande zote ni kujitenga na upande ambao umechagua kuukataa, kutoutumikia, wala kutoutakia mema.

Vita baina ya wema na uovu ni vita baina ya Mungu na shetani ambapo mwanadamu anahusika kufanya uchaguzi wa hiari wa kusimama upande mojawapo. Uchaguzi unafanyika kwa muda mfupi lakini kufuata masharti ya uchaguzi wako ni kazi ya daima. Kadri vita itakavyodumu kupiganwa baina ya Kristo na shetani ndivyo mwanadamu atakavyopaswa kusimama imara katika upande aliouchagua. Moja ya masharti ya askari anayepigana vita ni kutoona huruma na upande wa pili anaopigana nao, Ndivyo ilivyo hata katika vita ya kiroho baina ya Nuru na giza yaani Kristo akiwa na wafuasi wake na shetani na wafuasi wake. Maandiko yameeleza kwa kifupi sana kuhusu maadui hawa wawili walivyoanza kupigana vita na jinsi ambavyo wafuasi wa maadui hawa kamwe hawatajenga Umoja bali watadumisha uadui, watapigana na kushindana huku wakishinda na kushindwa na watatengana daima wasipatane kwa kadri uadui wa mabwana zao utakavyozidi kuwepo.

Kulikuwa na vita Mbinguni, Mikaeli na Malaika zake wakapigana na yule joka. Yule joka akapigana nao pamoja na malaika zake nao hawakushinda wala mahali pao hapakuonekana tena Mbinguni. Yule joka akatupwa yule mkubwa nyoka wa zamani audanganyae ulimwengu wote akatupwa hata nchi na malaika zake wakatupwa pamoja naye *(Ufunuo12:7-9)* Shetani na jeshi lake walitupa lawama ya uasi wao juu ya Kristo kwamba kama wasingeshurutishwa wasingeliasi wakadai kuwa sheria ya Mungu ina kasoro, ni ya kibeberu inayowanyima Viumbe uhuru, akatangaza nia yake ya

kuiondoa sheria hiyo na kuleta sheria yake ambayo ni bora zaidi kuliko ile ya Mungu walakini hata hivyo muasi mkuu na wafuasi wake alifukuzwa Mbinguni. (*GC459-501)*

Hii ndiyo vita ambayo haijulikani ilichukua muda gani huko Mbinguni, Wala hakuna taarifa ya waliokufa huko Mbinguni kutokana na vita hii. Vita hii ni zaidi ya uelewa ulionao kuhusu vita, kuielewa kwake kunahitaji akili inayovuka mipaka ya fikira za kiulimwengu. Utakapofahamu vita ile ya *Har magedoni* na muendelezo wake ndipo utaelewa hatari tuliyonayo kuhusu uadui baina ya Kristo na shetani.

Maneno yaliyotamkwa Mbinguni wakati vita hii imeisha yalionyesha hatari tuliyo nayo huku duniani.*(Ufunuo 12:12)* shetani alishuka kwa kasi kama umeme akiwa na ghadhabu nyingi kwa sababu alitupwa chini *(Luka10:18)* huu si wakati wa kueleza vita hii ilivyokuwa, turudi kwenye somo letu kuwa wafuasi wa hawa wawili watatofautiana na kufanya vita baina yao. Somo hili tutaelezea umuhimu na ulazima wa kujitenga kwa wale waliomchagua Mungu awe kiongozi wao, kuna maonyo, masharti na miiko wakati mtu amechagua kuwa upande wa Mungu.

*1. Swali:* Je, kitu gani cha kwanza ambacho Mungu ametutaka tufanye mara baada ya kuchagua kuwa upande wake?

Mwanadamu; wewe unakaa kati ya Nyumba iliyosi, watu ambao wana macho ya kuona ila hawaoni wana masikio ya kusikia ila hawasikii kwa maana ni *Nyumba iliyoasi. Basi mwanadamu, funga tayari vyombo kwa uhamisho ukahame wakati wa mchana mbele ya macho yao. Nawe utahama toka mahali pako hapa mpaka mahali pengine mbele ya macho yao labda watafahamu wajapokuwa ni *Nyumba iliyoasi *(Ezekieli 12:2-3 kumbuka Nyumba ni kanisa soma 1Timotheo 3:15,Isaya 56:7)*

"Kulikuwepo na kutoka nje utengano wa kujitenga na maovu uliotolewa maamuzi, kukimbia ili kuokoa maisha. Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo ilivyokuwa kwa Lutu, ndivyo ilivyokuwa kwa Wanafunzi wa Yesu muda mfupi kabla ya angamizo la Yerusalemu na ndivyo itakavyokuwa katika siku za mwisho. Sauti ya Mungu yasikika tena ikiwa na ujumbe wa onyo, ikiwataka watu wake wajitenge kutoka katika wimbi la uovu".(*PP166.)*

2.*Swali*:- Kwa nini ni muhimu kujitenga na Nyumba iliyoasi?

Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya *(2Wakorintho5:17)* "Roho inapojitoa kwa kristo huwa ni Ngome yake ambayo anailinda katika ulimwengu ulioasi na anakusudia kuwa hakuna nguvu nyingine inayotawala ndani yake wala mamlaka nyingine isipokuwa yake. *(DA324*.)

*3.Swali:-* Ni mambo gani ya kidini ambayo Mungu amekataa tusishirikiane wala kufanya pamoja na watu walio kinyume na imani yetu?

Nanyi mtakuwa watakatifu kwangu Mimi kwa kuwa Mimi ni Mtakatifu nami nimewatenga ninyi na mataifa ili kwamba muwe wangu (*Mambo ya Walawi 20:26*) Mkajitenge na watu wa Nchi, tena na wanawake wageni *(Ezra 10:11)* usitaje majina ya miungu yao *(Yoshua 23:7)* usifanye agano nao wala kuwahurumia wala usioane nao *(Kumbukumbu la Torati 7:2-3) Kwa kuwa u Taifa takatifu kwa BWANA Mungu wako na BWANA amekuchagua kuwa watu wake hasa kuliko mataifa yote yaliyo juu ya uso wa Nchi (Kumbukumbu la Torati.14:2)* Nami nitawatwaeni kuwa watu wangu nitakuwa Mungu kwenu nanyi Mtajua ya kuwa mimi ni YEHOVA *(Kutoka 6:7).*

Msifungiwe Nira pamoja na wasioamini kwa jinsi isivyo sawasawa . Bali ninyi Mliokuwa kwanza si Taifa bali sasa ni taifa la Mungu *(1Petro 2: 9 – 10)* . Tokeni kati yao Mkatengwe nao Msiguse kitu kilicho kichafu. Sanamu zao za kuchonga za Miungu yao Mtaziteketeza kwa moto. Usitamani Fedha wala dhahabu iliyo juu yao wala usitwae iwe yako usije ukanaswa nayo kwa maana ni machukizo kwa BWANA Mungu wako. Na machukizo hayo usitie ndani ya Nyumba yako usije wewe kuwa kitu cha haramu Mfano wake, Ukichukie kabisa na kukikataa kabisa, kwa kuwa ni kitu kilichoharamishwa *(Kumbukumbu la Torati 7: 25-26)* Nendeni zenu, nendeni zenu, tokeni huko Msiguse kitu kichafu, tokeni kati yake iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya BWANA. *(Isaya 52:11)* Kama mkikubali mtakula mema ya nchi bali kama mkikataa Mtaangamizwa kwa Upanga.

Mungu hagawanyiki. Imeandikwa Bwana mmoja, Imani moja na Ubatizo mmoja. Wale wanaompamba shetani badala ya kupambana naye wanamchukiza Mungu. Nuru na giza havikai pamoja.Mtu aliyejitoa kwa Kristo na kukiri imani yake kuwa ndiyo ya kweli ila wengine wapo upande wa shetani kwa hiyo wamepotea, wanapaswa kuhubiriwa ili watoke kwa shetani ambako roho za mashetani zimefanya makao huko, mtu wa namna hiyo Mungu amemkataza asishirikiane na maadui kufanya mambo yafuatayo ambayo Mungu ayachukia.

- Kufanya sala yeyote pamoja nao. Hakuna sala yeyote ya uzao wa nyoka inayokubaliwa na Mungu. (*Mithali 28:9)*

- Kufungamana kwa mambo yeyote yanayohusu Imani maana wao wana vinywa vya ukaidi (*Mithali 4:24)*
- Kufanya agano lolote linalohusu imani au kuoa na kuoana nao . *Kutoka 34:12-17.*
- Kutaja majina ya miungu yao hata kama kwa kigezo cha kuchukuliana nao. (*Kumbukumbu la Torati 7:25-26)*

- Kuhudhuria au kuingia katika dhehebu hilo kwa kigezo cha *harusi, Michezo au msiba.* Kumbuka unaposhirikiana na wasiomini, wachawi na wenye pepo unatiwa unajisi *(Walawi 19: 37*) Mungu hapatani na uchafu wowote (2*Wakoritho7:1)*
- Kuhudhuria mikutano ya imani yao *(Mithali 4:14-15-25, Mithali 3: 33)*
- Kumuita au kumkaribisha mtu/kiongozi asiye wa imani yako mahali patakatifu kuja kuzindua mradi au kufungua mkutano wako ni kuuweka mradi au mkutano huo chini ya utawala wa shetani/adui.*(2Yohana 1:10-11, 2Wathesalonike 3:6)* Mfalme Costantino aliua kanisa la kwanza kwa kutumia mbinu hii. Ndege wasiofanana hawawezi kuruka pamoja. Haiwezekani Bundi kukaa pamoja na kundi la Njiwa.
- Kutoa sadaka au mchango ili kuendeleza huduma ya Dhehebu lililo kinyume chako (isipokuwa tu kwa ajili ya huduma halali za jamii) ni kumsaidia shetani katika kazi zake za kumpinga Mungu. Mungu huwapinga wale wampingao. Hamuwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani, hamuwezi kushirikiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani (*1Wakoritho 10:20-21*) Je, hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi nivitwae viungo vya kristo na kuvifanya viungovya kahaba? Hasha (*1Wakoritho 6:15*)

*4.Swali:* Kuna ubaya gani nikikaribishwa kwenye sherehe ya dini ya mtu asiye wa imani yangu? Je, nikienda kuhudhulia tu na kufurahi kwenye sikukuu yao nitakuwa nimetenda dhambi gani?

> *Usiwahusudu watu waovu wala usitamani kuwa pamoja nao (Mithali 24:1).Yeye atafutaye furaha kutoka kwa wasiomcha Mungu anajiweka mwenyewe katika uwanja wa shetani na kukaribisha majaribu yake.(PP204)*

Kupokea msaada wowote kutoka kwenye shirika au kampuni yeyote ya shetani na kufanyia mambo ya dini ni kumtia moyo shetani asonge mbele. Umesahau kuwa Danieli alikataa zawadi za mfalme wakati ametafsiri ndoto ile? Danieli 6: 17, Habakuki 2: 9, 12, Kumb. 7: 25 – 26. Ni dhambi hata kuungana na watu wanaositasita katika njia mbili.(*Waebrania 10:38-39*) Mungu hajaruhusu hata wimbo wake uimbwe nchi ya ugeni sembuse kuhudhulia kwenye mikutano yao?*(Zaburi 137:1-4)*

Chochote kinachopingana na Neno la Mungu kinatoka katika kinywa cha Shetani (PP55) Ni dhambi kufanya ibada au ushirika wowote wa kiroho na mtu yeyote mwenye roho ya *Akani,* aliyeficha vitu vya *Babeli* kwa siri ambae anaiendea njia ya Yuda. Kufanya hivi ni sawa na kuwatia moyo Anania na Safira. Kumbuka kuwa kuficha vitu vya Babeli kunakufanya ushindwe kusimama mbele ya adui (*Yoshua 7:1-26*) Ni dhambi kuungana na dhehebu ambalo limemweka mwanadamu kuwa kichwa cha kanisa, Roho ya madhehebu inaenea kwa maraisi wa kanda (conference) shetani anainuliwa

kwa sababu amewavuvia wao sifa zake, nao wanafuata njia ya Urumi *(TM359-362)* Mungu hajatoa kauli yeyote katika neno lake kwamba amemteua mwanadamu yeyote kuwa kichwa cha kanisa. (*4SP53)Kichwa cha kanisa ni Kristo na Kristo ni wa Mungu*. (*1Wakorintho 3:23.)*

*5.Swali:*- Je kuna ushahidi mwingine wowote unaoonyesha kuwa pindi Dhehebu lolote linapoacha ukweli wa Mbinguni na kugeukia mapokeo ya wanadamu uwepo wa Mungu huondolewa na hivyo huduma zote za ibada hugeuka na kuwa dhihaka na kejeli mbele ya Kristo?

Ndiyo!. Ndiyo!.Ndiyo. Nitakuthibitishia hili katika kitabu cha Mathayo hasa kipindi Wayahudi wameikataa huduma ya Kristo. Maneno haya ya Yesu yalikuwa ya mwisho na tangu hapo yeye na wanafunzi walijitenga milele na uwepo wao uliondolewa milele.

Ee Yerusalemu,Yerusalemu uwauaye manabii na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa yake lakini hamkutaka! Angalieni nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa,kwa maana nawaambia *hamtaniona kamwe* tangu sasa hata mtakaposema amebarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana.*(Mathayo23:37-39)* "Katika maombolezo ya Kristo Moyo wa Mungu uliguswa, Hiyo ilikuwa ni kwa heri ya kisirisiri ya uvumilivu na upendo wa Kristo. Akiangalia ndani ya Hekalu kwa mara ya mwisho Yesu alisema kwa huruma na kuomboleza, angalieni nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa. Kama vile mwana wa Mungu alivyozitoka zile kuta, utukufu wa kuwepo kwa Mungu utaondolewa milele. Tamasha zake hazitakuwa na maana, huduma zake zitakuwa dhihaka"*(DA620)*

6.*Swali:*- Kitendo cha Yesu kutamka maneno kuwa "angalieni nyumba yenu mmeachiwa ukiwa kilikuwa na maana gani?

*"Mwokozi aliwaacha wayahudi*
*akawageukia watu wengine watakaofanya*
*kazi yake kikamilifu" (Ellen G white- AA16.)*

Kama Mungu alivyomtenga Nuhu ili aangamize Dunia yote ndivyo alivyomtenga Ibrahim katika nchi ya jamaa zake ili ambariki (*Mwanzo 12:1-3)* kama Mungu alivyomtenga Lutu na maangamizi ya Sodoma. *(Mwanzo 19:12-21)* Ndivyo anayotaka watu wake wajitenge na mifumo yote ya Ibada potofu.

*7.Swali:*- Mungu aliwachagua Israeli akawatenga wawe Taifa teule (*Kumbukumbu 7:1-26*) na takatifu, kipenzi cha Mungu kanisa lake *(Wimbo ulio bora 6:8)* ili wawe bikra safi watakaofuata maelekezo yake tu ili wawe Baraka na barua kwa ulimwengu, lakini walimuacha BWANA wakageukia sanamu na miungu ya kipagani, wakapiga mbio

mahali wasipotumwa wakalivunja agano lake, kanisa lililokuwa kipenzi chake likawa kipenzi cha shetani. Je ni nini kilifuata kwao?

"Nimeiacha nyumba yangu nimeutupa urithi wangu nimemtia mpenzi wangu katika mikono ya adui zake *(Yeremia 12:7)* na watu wa Babeli wakamwendea katika kitanda cha mapenzi wakamtia unajisi kwa uzinzi wao, basi alifunua uzinzi wake na kufunua uchi wake ndipo Roho yangu ikafarakana naye *(Ezekieli 23:17-18)* zaidi ya hayo wakuu wote wa makuhani na watu wakakosa mno sawasawa na machukizo ya mataifa, wakainajisi Nyumba ya Bwana aliyoitakasa katika Yerusalemu, naye Bwana Mungu wa baba zao akatuma kwao kwa *mikono ya wajumbe* wake kwa sababu aliwahurumia watu wake hata ilipozidi ghadhabu ya Bwana juu ya watu wake hata kusiwe na kuponya.*(2Mambo ya Nyakati 36:14-16)* Ndivyo walivyotiwa uchafu kwa kazi zao walifanya uasherati kwa matendo yao*( Zaburi 106:39)* hasira ya Bwana ikawa juu ya Israeli. *Waamuzi 2:20*

8.*Swali:*- Ni onyo gani la kuogopwa ambalo Mungu amelitoa kwetu ikiwa tutaamua kusimama upande wake? Je,haitupasi kuungana kidogo na Madhehebu mengine na kuchukuliana nao taratibu ili labda tuweze kuwavuta? Je, hata kwa hili Mungu amekataza? Roho ya unabii imeandika nini kuhusu hili?

"Ondokeni mwende zenu maana hapa sipo mahala pa raha yenu.Kwa ajili ya uchafu mtaangamizwa naam kwa maangamizo mazito sana *(Mika 2:10)*

"Nilionyeshwa ulazima wa wale wanaoamini kuwa tunao ujumbe wa mwisho wa Rehema wakiwa wamejitenga kutoka kwa wale ambao kila siku wanakunywa makosa mapya, nilionyeshwa kuwa asiwepo mtoto au mtu mzima wa kwenda kuhudhuria mikutano yao kwa maana ni makosa, kufanya hivyo ni kuwatia moyo wakati wanafundisha makosa ambayo ni sumu mbaya ya mauti kwa Roho wanapokuwa wanafundisha mafundisho ambayo ni maagizo ya Wanadamu. MUNGU huchukizwa nasi tunapokwenda kusikiliza makosa bila kuwa tumeagizwa kwenda. Mungu hataweza kutulinda, ulinzi wa Malaika unakoma kwetu na tutaachwa katika misukosuko ya adui ili tujazwe na giza, na Nuru ituzungukayo huchafuliwa na giza (*EW124-125, Maandiko ya Awali Sura ya 31 Ukurasa 126-127)*

9.*Swali:*-Ni nini ambacho Paulo na Barnaba walikifanya wakati kanisa la kiyahudi limetupilia mbali neno la Mungu na kukataa kufanya matengenezo yaletayo toba?

Paulo na Barnaba wakanena kwa ushujaa wakisema ilikuwa lazima neno la Mungu linenwe kwenu kwanza, lakini kwa kuwa mmelisukumia mbali na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele angalieni twawageukia Mataifa.(*Matendo 13:46)*

*10.Swali:-* Je, ni kwa maneno yapi unaweza kuthibitisha kuwa ni kweli Paulo na wenzake walijitenga"

"Akaingia ndani ya sinagogi akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu akihojiana na watu na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu. Lakini wengine walikaidi wakakataa kuamini wakiitukana ile njia mbele ya mkutano basi akaondoka, akawaacha, akawatenga wanafunzi na watu kila siku katika darasa la mtu aliyeitwa Tirano, mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana Wayahudi kwa Wayunani (*Matendo 19:8-10.)*

*11.Swali:* Je, ni fundisho gani tunalipata hasa katika wakati wetu huu wa hatari ambapo mbwa mwitu wanatawala madhehebu?

"Mungu na Kristo na jeshi la Mbinguni wangetaka wamjulishe mwanadamu kuwa ikiwa ataungana na upotofu atanajisika *(Seventh Day Adventist Bible Commentary volume 6 uk 1102)* Tunapaswa kutoka kati yao na kujitenga, na kuwa imara kama mwamba, Kristo ametupatia mfano.*(FE482)* Tunao ukweli wa kupimwa wa kutoa kwa ulimwengu, nimeagizwa kuwaambia watu wetu, tuungane,! tuungane!, tuungane,! lakini *tusiungane* na wale wanaoiacha imani na kusikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani.*(3SM 412)*

*12*. Ni matokeo gani mengine yatampata mtu anayeshupaza shingo asifanye wajibu umpasao?

Mtu anayeshupaza shingo yake asifanye wajibu umpasao mwishowe atapotewa na uwezo wa kupambanua baina ya kweli na makosa, ndipo atatengana na Mungu bila kuwa na habari. Kanisa likisukumia mbali neema ya Mbinguni hubaki katika giza, imani na upendo hupoa na mafarakano hutokea. Mwishowe makanisa hushughulika na mambo ya ulimwengu na wenye dhambi hupoa hata wasione haja ya Kutubu. *(GC 378-379)*

*13.Swali:-* Je msimamo huu wa kujitenga hauwezi kuleta mtafaruku migongano, kutoelewana na chuki miongoni mwetu na wale walio kinyume chetu?

Mtu yeyote asiyeuchukua msalaba wake na kuja nyuma yangu hawezi kuwa mwanafunzi wangu *(Luka 14:27)* Kama mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda walio wake, lakini kwa kuwa ninyi si wa ulimwengu bali mimi naliwachagua katika ulimwengu kwa sababu hiyo ulimwengu huwachukia. Ikiwa waliniudhi mimi watawaudhi ninyi, ikiwa walilishika neno langu watalishika na lenu. Wala msishirikiane na matendo ya giza bali myakemee*(Waefeso5:11) (Yohana 15:18-21*. Hakuna mwisho wowote wa kutunga vitabu na kusoma sana huuchosha mwili, Panda

milimani ukawashe taa yako ili Nuru ya BWANA iwamulikie watu. Neno litasimama daima lisitikisike, Ikiwa nuru imekuangazia chukua hatua. Utengano ulianza Mbinguni kati ya Kristo na shetani na sharti udumishwe baina ya wafuasi wake waliopo duniani.

Ni jambo rahisi kufa kwa ajili ya Neno ambaye Neno alifanyika mwili naye mwenyewe alikufa, ikiwa kuwa na amani kwa kutupilia mbali kanuni za Mungu ndiko kunaleta Umoja basi amani na Umoja wa namna hiyo na upotelee mbali ikilazimu kuwepo na utengano na hata kwa vita. Mtu anayetaka kuwa muhubiri wa neno la Kristo ulimwenguni hana budi atazamie kifo wakati wowote. (*GC45,135,141)*Yatupasa tuchague haki kwa kuwa ni haki ya kumwachia Mungu mengine yote, mtu ashikaye kanuni, mwenye imani, aliye jasiri ndiye anayehitajika ulimwenguni ili alete matengenezo. Mtu au watu wa namna hiyo ndiyo wanaotakiwa wafanye matengenezo kwa wakati huu na kuyaendeleza.*(GC460)*

SURA YA TATU

## MIMI NIKO AMBAYE NIKO

Ni nani huyu atiaye mashauri giza kwa maneno yasiyo na maarifa? Basi jifunge viuno kama mwanaume maana nitakuuliza neno nawe niambie, Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Haya! Sema, kama ukiwa na ufahamu.Je umeziingia chemchemi za bahari au umetembea mahali pa siri pa vilindi? Umeyafahamu mapana ya dunia? Haya! Sema ukiwa unayajua hayo yote, iko wapi njia ya kuyafikia makao ya nuru? Na giza pia mahali pake ni wapi? Je waweza kumwindia simba mke mawindo? au utashibisha njaa ya simba wachanga,waoteapo mapangoni mwao wakaapo mafichoni wapate kuvizia? Ni nani anayempatia kunguru chakula makinda yake wanapomlilia Mungu kwa kutindikiwa na chakula?

Je ulimpa farasi uwezo wake? Au ni wewe uliyemvika shingo yake manyoya yatetemayo? Ndiwe uliyemfanya aruke kama nzige? Fahari ya mlio wake hutisha, huparapara bondeni na kuzifurahia nguvu zake. Hutoka kwenda kukutana na wenye silaha.Yeye hufanyia kicho dhihaka wala hashangai,wala hageuki kurudi nyuma mbele ya upanga. Podo humpigia makelele mkuki ung'aapo kwa fumo. Huimeza Nchi kwa ukali wake na ghadhabu wala hasimami kwa sauti ya baragumu. Kila ipigwapo baragumu yeye husema, aha!. Naye husikia harufu ya vita toka mbali, mshindo wa maakida na makelele.

Je! Mwenye hoja atashindana na Mwenyezi? Mwenye kujadiliana na Mungu na amjibu yeye. Mwangalie huyo kiboko niliyemuumba pamoja nawe,yeye hula majani kama vile ng'ombe. Tazama basi nguvu zake zi katika viuno vyake, na uwezo wake u katika mishipa ya tumbo lake.Yeye hutikisa mkia wake mfano wa mwerezi, mishipa ya mapaja yake yanaungamana pamoja. Hakika milima humtolea chakula hapo wachezapo wanyama wote wa barani. Tazama mto ukifurika yeye hatetemeki. Hujiona yu salama ijapokuwa Yordani hufurika hata vinywani pake.

Je! Waweza kumvua Mamba kwa ndoana? Au kuufunga ulimi wake kwa kamba? Je! Waweza kutia kamba puani mwake? Au kutoboa taya lake kwa kulabu? Je! atakusihi sana? Au atakuambia maneno ya upole? Je! atafanya agano pamoja nawe umtwae kuwa mtumishi wako milele? Je? utamchezea kama ndege? Au kumfunga kwa ajili ya Wasichana wako? *(Ayubu38:2-4,16,18-19,39-41.39:19-25,40:2,15-17,20,23,41:1-5)*

Sasa Jua laenda kuchwa. Vivuli vya giza visogeapo giza laifunika dunia, watu waenda zao kulala wakati popo na bundi wakitoka na kutembea gizani kutafuta mawindo.Usiku waisha mchana tena waingia. Ndipo nitembeapo huku na kule mwangani bila woga

wakati macho yakiona mengi ya dunia. Niyaonayo yafurahisha moyo akili kuburudika moyo uonapo nuru.Kweli nuru ni tamu tena ni jambo la kupendeza macho kutazama jua! Dunia imejaa maajabu mengi yasiyoneneka. Kuna wingi wa Nyota wakati wa usiku. Jua latawala mchana likitoa mwanga wake. Jua linatoa mwanga pia kwa ajili ya Mwezi na Nyota. Mwezi na Nyota vinatawala usiku kwa msaada wa Jua.*(ED24)* Kuna fahari ya ajabu katika anga ambayo imepambwa na utukufu na uzuri kumfurahisha mwanadamu.Fahari hii ya ajabu ndiyo iipambayo Mbingu kwa uzuri hata ikapendeza kwa uasili wake ikizitangaza ajabu za Mungu!.

*" Kuna fahari moja ya Jua na fahari nyingine ya Mwezi na fahari nyingine ya Nyota, maana iko tofauti kati ya fahari hata fahari, kati ya Nyota na Nyota"(IWakorintho 15:41)*

Hivi vyote vyatoa ushahidi kila tuvionapo nasi twajua kuwa mkono wa Mungu ulifanya hayo. Huu ndiyo mkono wa mwanasayansi mkuu aliyefanikiwa kutandaza Mbingu hewani zisianguke! Ndiye pekee atembeaye huku na huko juu na katika vilindi vya bahari! Mengi tuyaonayo ni matokeo ya hekima zake takatifu. Nami napita huku na huko katika mapori na vijiji nikistaajabia ukuu wa Mungu. Katika msitu laonekana pori nene ambapo mbele yake kuna Mlima mkubwa uliojaa Mawe na utajiri wa viumbe wengi kuuzunguka. Sasa nipo katikati ya msitu mnene unaotisha kutembea upweke, hofu yanijia mahali hapa maana kama siyo damu yaweza nukia!. Hali ni tulivu na shwari lakini inayoogofya moyo. Hakuna kelele yoyote inayosikika hapa zaidi ya Nyimbo za Njiwa ambao wanasikika wakimtukuza Muumba wao bila hofu. Wanaimba wakiwa katika matawi wakirukaruka kwa furaha. Katika udongo panaonekana ni sehemu yenye rutuba, Sauti za kwale pia zasikika kwa mbali pindi Jua lituapo.

Hapa anaonekana kinyonga akitembea kwa mwendo wa maringo, macho yake yageuka kila apendapo, mara ajigeuze rangi hata iwe vigumu kumgundua mahali alipo. Lo! Kama mwanadamu naye angegeuka tabia yake afanane na Yesu!. Tabia ya kinyonga ikufundishe ugeuke ukafanane na Yesu kwa Tabia. Ni kinyonga huyu huyu ambaye hana haraka ya safari. Mwendo wake ni wa maringo uliopangiliwa. Yeye anaucheka wakati ujao. Hana haraka hata kama hatari yaja mbele yake. Mwendo wake ni wa pole maringo na madaha mithili ya mwendo wa bibi harusi aliye tayari kukutana na ampendaye. Ni kinyonga huyuhuyu ambaye akitaka kujifungua ndipo hukwea hata juu na kujirusha hata chini ndipo tumbo lake lipasuke na yeye kufa ili wana wake waione dunia.

Nyuma ya maajabu haya kuna mkono wa fundi stadi atendaye haya. Yeye hutenda yote akiamuru hutokea maana yeye ni mweza wa vyote, alisema tu mara ikawa.*(Mwanzo1:24-25)*. Licha ya kuwaona Siafu waliojipanga mstari wakiwa katika moja ya safari zao kuna Kichuguu kikubwa ambacho Mchwa wamejenga kwa ajili ya makazi

yao. Sasa namuona Jongoo akiwa anatembea. Nikimuangalia nastaajabu kumwona kumbe hana macho! Miguu yake mingi yashangaza pindi atembeapo kwa hatua. Wingi wa miguu yake haumpi shida aanzapo safari, mkono uliofanya hivi wanipa funzo. Upepo ukivuma miti haichelewi kumsujudia Mungu. Katika matawi ya miti anaonekana buibui katika nyumba yake. Hii siyo nyumba ya kupanga ni nyumba yake. Buibui haishi nyumba ya kupanga. Ndiyo maana Mungu ametaka wavivu wote wawaendee wadudu hawa wadogo wakajifunze kwao. Je, anamtaka mvivu amwendee nani?

> *" Ewe mvivu mwendee chungu, zitafakari njia zake upate hekima kwa maana yeye hana msimamizi lakini hujiewekea akiba ya chakula wakati wa jua." (Mithali 6:6-7)*

> Kwa yeyote anayejifunza ili kupata mafundisho yaliyomo Maumbile yote huwa yametiwa nuru.Ulimwengu ni kitabu cha kujifunza na maisha huwa shule. *(ED100)* Hii ni kazi ya Mungu aliye juu mwenye uwezo na mamlaka duniani na Mbinguni afanyaye ishara katika Nyota, ambaye nafsi ya kila kilicho hai i mkononi mwake na Pumzi zao wanadamu wote" *(Ayubu 12:10).* "Mungu ni upendo" imeandikwa juu ya kila chipukizi. Juu ya kila jani dogo litokalo ubua wake. Na miti yote hutushuhudia upendo wake. Viumbe vya ulimwenguni vimekuwa kama Mitume kutuletea habari za faraja na utulivu. Kila mti wa miiba una maana yake pia, yaani katika kila shida twaweza kupata baraka za Mungu. Mpangilio wa viumbe vya asili, hayawani wa anga vyote hutufunulia tabia ya Mungu, Wanyama wa mwituni, mimea ndege, wadudu hewa safi, maua na vyote vilivyomo tukiviuliza habari za Mungu vitatujibu vizuri tena kwa usahihi. Je, kuna haja ya kuwauliza wanyama?

*Lakini sasa waulize hao Wanyama nao watakufundisha,na Nyuni wa angani nao watakuambia, nena na Nchi nayo itakufundisha,nao Samaki wa baharini watakutangazia,katika hawa wote ni yupi asiyejua kwamba ni mkono wa BWANA uliofanya haya?(Ayubu 12:7-9)*

Tunapotafakari juu ya Mungu na ijulikane kuwa tunatafakari juu ya yule mwenye kuheshimiwa, mwenye mamlaka na uwezo wote. Tujifunze namna ya kumwendea na kumwabudu kwa Sala na Ibada. Twapaswa kumtii na kujua kuwa tupo mbele za yule anayeheshimiwa ambaye vyote vyatoka kwake. Mungu ni moto ulao kwa wenye dhambi. Hakuna mwenye dhambi awezaye kuuona uso wake; Kumbukeni yaliyotokea mlima Sinai wakati Mungu aliposhuka. Mlima ulitetemeka na kutoa moshi maana Mungu aliteremka katika moto.*(Kutoka 19:17-20)*

Basi jueni ya kuwa BWANA ndiye Mungu wenu ndiye Mungu mwaminifu ashikaye rehema zake kwao wampendao na kuzishika amri zake hata vizazi elfu.*(Kumbukumbu la Torati 7:9)* Tunapaswa kumheshimu Mungu na kumuweka mahali pa kwanza kuliko chochote. Neno lake na lipiganiwe bila kujali kitu chochote. Hakuna mwanadamu anayekufa awezaye kuzuia Mungu asiheshimiwe,maana yeye ni wa kwanza na wa mwisho mtakatifu aliyetukuka sana *(Isaya 57:15 )*mkamilifu ambaye jina lake lapendeza *(Zaburi 13:3)* ambaye macho yake hukimbiakimbia duniani kote, wala hakuna kiumbe kisicho wazi mbele zake,maana vitu vyote vi wazi na kufunuliwa machoni pake yeye aliye na mambo yetu.*Waebrania 14:13*

Kwa sababu ulimwengu na vyote ni mali yake Mungu twajua ya kuwa hakuna mwanadamu mwenye mwili wa kufa awezaye kuondoa, kubadili, kurekebisha au kudharau neno takatifu. Kukataa neno la Mungu kwa sababu ya elimu yako, cheo, busara, kiburi au mali ulizonazo kutakuweka katika nafasi mbaya katika hukumu ambapo matokeo yake wewe mwenyewe utahusika maana kila mtu ataubeba mzigo wake mwenyewe.*(Wagalatia 6:5)*Ikiwa viumbe vya asili vinamtambua na kuijua sauti yake wewe ni nani hata ukashupaza shingo na kumdharau Mungu,ukamfananisha yeye na mwanadamu? Manabii walionya binadamu yoyote asijiinue kuliko Mungu.

> *Zaidi ya viumbe vyote vya dunia,Mungu alikusudia kuwa yeye aliye kazi bora zaidi ya vyote vilivyoumbwa aonyeshe mawazo na kufunua utukufu wake lakini mwanadamu asijitukuze yeye kama Mungu.(8TM264)*

Ni wakati wa kumrudia yeye na kupigania neno lake bila kujali kitu chochote maana ndiye pekee mtoa kauli kwa viumbe vyote akavitiisha navyo vikamtii mara.Aliamuru viumbe wote waingie katika safina wakamtii,alimtuma kunguru amlishe nabii Eliya naye akamtii, *(1Wafalme17:6*) Yupo njiwa ambaye alipotumwa kuangalia maji ya gharika kama yamepungua alimrejea Nuhu akiwa na jani la mzeituni *(Mwanzo 8:11)*Mama Jusi waliitazamia nyota iliyowaelekeza mahali alipozaliwa mtoto (*Mathayo 2:2,7)*Baalamu kwa macho yake alistaajabu alipoona kwa mara ya kwanza punda akiongea alipomwona malaika wa BWANA akisimama mbele wakati Baalamu alipompiga fimbo *(Hesabu 22:28-30)* mwanadamu ni nani mbele zake? Ni Mungu huyuhuyu aliyechoshwa na uovu akamgeuza mfalme Belshaza akawa na moyo wa mnyama na kula majani kama ng'ombe muda wa miaka saba *(Danieli 5:21)* Maana yeye ndiye aketiye juu ya duara ya Dunia na hao wakaao katika dunia huonekana kama panzi *(Isaya 40:22)* ndivyo alivyo Mungu wetu milele habadiliki,mambo yote ya zamani yaonyesha kuwa hakuna aliye kama yeye. Hatupaswi kuyasahau mamboya zamani.

> *Kumbukeni mambo ya zamani za kale maana mimi ni Mungu wala hapana mwingine, nitangazaye mwisho tangu mwanzo na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka*

*bado,nikisema shauli langu litasimama nami nitatenda mapenzi yangu yote.Nikiita ndege mkali toka mashariki, mtu wa shauri langu toka nchi iliyo mbali naam nimenena nami nitatekeleza, nimekusudia naami nitafanya. Isaya 46:9-11*

MWANADAMU MBELE ZA MUNGU

Akisimama mbele za Mungu mtakatifu mwanadamu si kitu,yeye ni kama kivuli ambaye siku zake zapita kama jani *(Zaburi 103:13-16)* Macho yake yalituona kabla hatujakamilika *(Zaburi139:16)*Akayathibitisha kwa kinywa cha nabii Yeremia *(Yeremia1:4)* Ni huruma za BWANA kuwa hatuangamii maana yote tutendayo yapo wazi, Mungu hutuona kila tutendalo. Taarifa zako, mema na mabaya yote yanaandikwa kwa usahihi sana kana kwamba ni wewe pekee uliyepo duniani. Hakuna lugha nzuri wala maelezo ya kutosha kueleweka yatakayosemwa na mwanadamu kudhihirisha jinsi matendo yetu yalivyo wazi kwake.Tunasimama mbele za Mungu katika mizani tukipimwa kila dakika ipitayo.

Mtunga zaburi alipoonyeshwa jambo hili lilivyo aliandika haya, Ee BWANA umenichunguza na kunijua, wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu,umelifahamu wazo langu tokea mbali maana hakuna neno ulimini mwangu usilolijua BWANA, maarifa yako ni ya ajabu yanishinda mimi siwezi kuyafikia. Niende wapi nijiepushe na roho yako? kama ningepanda mbinguni wewe uko. Ningefanya kuzimu kitanda changu wewe uko.kama nikisema hakika giza litanifunika giza nalo halikufichi kitu. Bali usiku huangaza kama mchana.Giza na mwanga kwako ni sawasawa.*(Zaburi 139:1,2,4,6-8,11-12)*

Je! wewe waweza kuuvumbua ukuu wa Mungu? Waweza kuufikilia upeo wa huyo mwenyezi? Ni juu mno kama Mbingu waweza kufanya nini wewe? Ni wenye kina kuliko kuzimuni waweza kujua nini wewe? Cheo chake ni kirefu kuliko dunia, ni kipana zaidi ya bahari.Yeye akipita na kufunga watu ni nani awezaye kumzuia? (*Ayubu 11:7-10)*

Maana yeye anayo mashauri na ufahamu *(Ayubu12:13)* Ndiye pekee awezaye kumfanya mtu kuwa bubu *(Kutoka 4:11)* ambaye nafsi ya kila kilicho hai i mkononi mwake na pumzi zao wanadamu wote *(Ayubu12:10)* Ndiye ajuaye idadi ya masikini wote wanaonyonywa na matajiri, Ni Mungu pekee awezaye kumwinua mnyonge na kumpa riziki yake, ni yeye tu mwenye takwimu ya kweli ajuaye dunia hii ina walevi wangapi, lita zote za pombe ulizokunywa yeye anazijua. Huyu ndiye mwenye idadi ya kweli ya Mimba zilizotolewa Duniani, maneno yote ya uongo uliyosema kwa lugha yako yeye anayajua, Pakiti za sigara ulizovuta zimehesabiwa kwa ajili ya hukumu ya mwisho utakapotoa hesabu ya mapafu uliyounguza kwa ajili ya moshi huo.

Kuna pombe iliyonywewa na mlevi mmoja aliyekunywa akiwa amefurahi baada ya kufundishwa kuwa siku hiyo ilikuwa ni siku ambayo Yesu alizaliwa, akiwa na uchu wa kuandaa sherehe hiyo bosi huyo aliazimu kupunguza mishahara ya vibarua wake ambapo mfanyakazi mmoja aliyekuwa na mgojwa akihitaji kufanyiwa upasuaji alikufa kwa kutokuwa na pesa za kutosha. Mlevi huyo alikusanya pesa kwa ajili ya sherehe hiyo huku kwa unafiki akitoa pole kwa mfiwa huyo akamalizia na kutoa mchango wa sanda. Sherehe ilisherekewa kwa kula kila vyakula licha ya nyumba ya wageni walikopanga kumalizia anasa zao kwa ajili ya kukamilisha sherehe waliyoiita ya kuzaliwa kwa huyo aliyedaiwa ni Yesu. Haya yote yataletwa siku ya hukumu.

Kuna malaika wanaoandika mambo haya kwa usahihi sana ili kuja kuyaleta hukumuni *(Mhubiri 12:14)* Wakati walevi hao wakiwa katika nyumba ya wageni pembeni alikuwepo yule asiyeonekana akiwaangalia kila hatua waliyofanya kwa huruma.Mara kwa mara Mungu amekuita mpenda anasa, akimulika Nuru ya neno njiani mwako ili uone hatari lakini umezidi kwenda katika njia pana mpaka rehema ifungwe kwako. Njia za Mungu ni za haki na sawa. Hukumu itapotolewa juu ya wale wanaoonekana wamepungua kila kinywa kitafumbwa.*(4T435)*

Katika zama hizi ambazo maendeleo yanatafutwa shetani amewaweka watu wake shughulini ili wasahau kuwa kuna Mungu mbinguni na shetani duniani. Sasa wanadamu wamejaa kiburi kilichokuwepo sodoma na Gomora. Mungu atatuma vitu vya asili kutoa funzo. Mvua ilitumika wakati wa Nuhu wanadamu walipoona maisha yana maana kuliko kuingia katika Safina. Mungu alikuwa amehuzunika na kuhangaika nao akijaribu kuwarudisha katika toba. Hapo walipokataa Mungu akaghairi na kugharikisha dunia kwa mvua ya siku arobaini *( Mwanzo 7:4)* Sasa akaapa kuwa hatatuma tena mvua ila anao mitume wengine watakaotumika siku za mwisho.

Dunia hii haitaangamizwa kwa maji tena maadamu ishara aliyomwapia Nuhu ionekanapo katika sayari hii. Wengine hawaelewi ishara hii ambayo kila ionekanapo yatukumbusha kizazi cha Gharika kilivyoteketea. Mungu akasema hii ndiyo ishara ya agano nifanyalo kati yangu na ninyi na kila kiumbe hai kilicho pamoja nanyi Upinde wangu utaonekana winguni nao utakuwa ishara ya agano kati yangu na nchi." Hata itakuwa nikitanda mawingu juu ya nchi upinde ukaonekana winguni nami nitalikumbuka agano langu lililoko kati yangu na ninyi na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili wala maji hayatakuwa gharika tena kuwaharibu wote wenye mwili. Basi huo upinde utakuwa winguni nami nitauangalia nipate kulikumbuka agano la milele lililoko kati ya Mungu na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili kilichoko katika nchi. *(Mwanzo 9:12-16).*

Mungu akafunga kiapo chake kwa kuweka upinde wake. Kila tuonapo twatambua kuwa yeye habadiriki. Ndivyo ilivyo kwa sheria na amri zote alizotoa. Aliyoazimia yote

atayatenda kwa mkono wenye nguvu. Wakati alipoazimu kuwatoa Islaeli ili awapeleke kaanani, Farao alijaribu kufanya kile ambacho Mungu hawezi kufanya. Farao alijaribu kufanya kile ambacho watawala wa leo kwa macho yetu na masikio twashuhudia wakifanya. Roho ya Farao ingali hai katika mioyo ya watawala wa dunia hii kuzuia mpango wa Mungu. Roho ya Farao ingalipo ikimpinga Mungu kupitia vibaraka wake.

Farao alisema Bwana ni nani hata niisikilize sauti yake na kuwapa watu ruhusa waende zao? *(Kutoka5:2.)* Ndipo Mungu aliposimama kushindana na Farao. Viumbe vya asili vilionekana kumtisha Farao hata atambue kuwa kuna Mungu mbinguni. Mungu aligeuzageuza na kupinduapindua na kuonyesha utisho kupitia viumbe vya asili ambavyo vilikuwa shule kwa Farao. Kupitia viumbe vya asili nchi ya Misri iliingiwa na hali ngeni matukio ya ajabu yaliyoambatana na vioja yalionekana kwa wamisri maji ya mito yalipogeuzwa damu samaki na viumbe vyote vyenye uhai vikafa *(Kutoka 7:21)*

Hakukuwepo na marashi yaliyojaa kufunika harufu mbaya kwa ajili ya uvundo wa pigo hilo. Hali ya hewa ilikuwa harufu mbaya iliyokera kila kiumbe chenye uhai. Sasa lililetwa kundi kubwa la vyura waliojaa katika nchi yote ya misri hata isiwepo nafasi kila eneo likajaa vyura pande zote. Mungu alifanya hivi ili kumkomesha mfalme mwenye kiburi. Hali ikawa ni ya hatari kiafya sasa shambani kumejaa vyura, uwanjani kunaonekana vyura wengi mfalme anataka kuingia sebuleni anakuta vyura wengi waliojaa kila kona mpaka katika viti na meza za kulia chakula. Vyura walijaa wakafurika mpaka kwenye kitanda cha mfalme, vyombo vya kulia chakula, uvunguni wa kitanda na katika vyombo vya kupikia. Hali ilikuwa mbaya pande zote zikajaa vyura waliorukaruka kila upande *(Kutoka 8:3-4)* na uwezekano wa kufanya usafi haukuwepo maana vyura wamejaa pande zote.

Aligeuza damu mito yao na vijito wasipate kunywa aliwapeleka mainzi wakawala na vyura wakawaharibu. *(Zaburi 78:44-45)* yule aliyeumba vitu vyote na kuvitiisha kwa uwezo wake ndiye mwenye kauli ya mwisho duniani ndiyo mwenye kuamua nini kitokee leo nani afanye nini na huyu ndiye aliyeweka mawe juu ya kila mlima akayategesha vizuri kwa ajili ya wakati maalum yatakapotumika kwa kusudi maalumu wakati mfupi ujao. Mwanadamu umeshaonywa kuyakimbia mapigo saba yanayokuja juu ya wale wenye chapa ya yule mnyama *(Ufunuo 16:1-21)*

Nchi ya misri ilijaa chawa kila upande mpaka wachawi wakamkiri Mungu! *(Kutoka 8:16-19)* kama hilo halitoshi Mungu alimimina kichupa chake cha majibu yakatokea majipu mabaya yenye kufura na kutumbuka juu ya wanadamu *(Kutoka 9:10)* Majipu hayo mabaya yanayoogofya ndiyo ambayo yameandaliwa muda mfupi yatakapomwagwa tena duniani kwa wanadamu wasiomtii. Haitakuwa historia tena ila kila mtu ataona mwenyewe ghadhabu za Mungu katika mwili wake. Siku hiyo ndiyo utajua ubaya wa dhambi. Historia ya iliyopita ni kauli halisi juu ya kile kijacho punde wakati Yesu

atakapotamka maneno ya huzuni duniani *(Ufunuo 22: 11)* siku ya kwanza wakati Dunia inazaliwa Mungu ndiye aliamuru iwepo Nuru *(Mwanzo 1: 3)* Huyu ndiye alituma tena giza katika nchi ya misri kwa muda wa siku tatu tena mchana na usiku dunia ikawa giza nene jeusi na lenye upana giza, lililofanya uso ukawa mzito kulikabili likawepo Misri siku tatu.

*"Hawakupata kuonana mtu na Mwenzie walahakuondoka*
*Mtu mahali alipokuwa muda wa siku tatu" (Kutoka 10:23)*

Matendo haya yakufikirishe sana juu ya Mungu. Tunapomtaja Mungu au tumwombapo yapasa tumwendee kwa kicho na heshima kuu. Mungu ni wa kuheshimiwa nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu kwa roho na kweli ambaye ndiye mwenye sauti ya mwisho duniani. Kuna watu walioelezea vibaya tabia yake Mungu akaachia mwanya katika nchi aridhi ikawafunika *(Hesabu16:31–32)* Huyu ndiye mshindi asiyeshindwa na chochote, ni mfalme juu ya wote wenye mwili. Wanadamu wana uzoefu na mambo mengi ya maisha duniani lakini hawana uzoefu na kifo. Kufa kunatisha, kifo kinahuzunisha, hakina likizo wala matayarisho. Kifo kimeacha yatima na wajane wengi., Lakini hili ndilo pigo ambalo Mungu alilituma katika Nchi ya Misri. Hili ndilo pigo lililoacha historia katika Nchi ya Misri mpaka Taifa lote likajaa machozi. Katika siku hiyo kulikuwa na msiba kila familia tena msiba wa mzaliwa wa kwanza. Baba aliongoza kwenda kuchimba kaburi na kuzika bila kusubili majirani na ndugu wa marehemu. Kila familia ikazika kwa uchungu mzaliwa wa kwanza wa binadamu na mnyama pia tangu katika nyumba ya mfalme mpaka masikini wa mwisho, (*Kutoka11:4-5)* Nchi ya Misri ikanajisika muda wa siku saba. (*Hesabu 19:11-13)*
Kadri tunavyoelekea mwisho shetani atawatia wanadamu katika giza la kiroho wasijue mpango wa Mungu, Mungu anao msingi wa tabia yake ambao umekuwepo tangu kale na haubadiliki. Hii ndiyo chapa ya tabia yake. Ni msingi udumuo milele. Maendeleo ya mwanadamu hayawezi kugeuza lengo lake. Wingi wa miaka hautageuza neno lake. Hiki ndicho kitabu kitakatifu ambapo pindi tuchunguzapo twapata nuru ya tabia yake. Katika kurasa zake hupatikana historia ya zamani sana, maandiko ya kweli kabisa yapatikana humo. Ndipo mahali ambapo kuna elimu ya maana sana. Utenzi mtamu na bora wenye thamani wapatikana katika biblia.Tunapaswa kumtambua kuwa Mungu ni yuleyule jana leo na hata milele. *(Waebrania13:8).*

*" Shauri ni langu na maarifa yaliyo sahihi. Mimi ni ufahamu mimi nina nguvu kwa msaada wangu wafalme humiliki na wakuu wanahukumu haki, na waungwana, naam, waamuzi wote wa dunia kabla haijawako dunia, kabla milima haijawekwa imara, kabla ya vilima havijazaliwa. Basi wanangu nisikilizeni sasa maana heri hao washikao amri zangu ( Mithali 8:14-16,23,25,32)*

Ili tuweze kuokolewa tunahitaji kuijua Njia kuu. Tunapoingia kuitafuta Njia hii ambayo walimwengu wanapita kando yake tutamwona Mungu akitushindia. Njia hii inapitika na wale tu walioamua, kuacha ya dunia na kuipita,wanaopita njia hii wanatofautiana kila kitu na walimwengu. Wasafiri hawa wanao mvao maalumu unaowatambulisha kama wasafiri, pia wanaye Bwana wao awaongozaye, wanakula chakula alichokula Adamu kule Edeni huku wakitofautiana na mataifa kwa usemi na tabia. Njia hii ni maalumu kwa ajili ya watakatifu.

Sasa twaenda kuiona njia hii kama ilivyo. Tukiwa njiani humo, tutaimba nyimbo za mjini tukiwa na tumaini la kufika. Miguu yetu iwe mizito vipi lakini tutatembea katika njia hiyo, maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni *(Wafilipi 3:20)* Ni Njia ambayo wasafiri wake wanajuana kwa tabia na mwenendo ni njia ya matumaini ya kumwona aliyeianzisha. Ingawa njia hii haipitwi na wengi lakini sisi tutapita njia hiyo. Ingawa mioyo yetu ni migumu lakini tutaizoeya tukiwa na Yesu. Ingawa hatutakuwa wengi, Mungu atakuwa nasi njiani ijapokuwa shetani na watu wake watatudharau tuwapo safarini, lakini Mungu atatuheshimu.

Tutatembea katika njia hiyo ingawa kuna alama za damu kila tupigapo hatua kuonyesha mwisho wa safari yetu ulivyo. Punde tutaona mordekai akisimama mbele ya mfalme ili kukabili mauti.Tayari twasikia sauti za kelele za mbwa mwitu wakipanga njama kumzunguka mordekai huku shetani akichekelea tukio hili pamoja na wafalme wa nchi.Tutamwona Uria mhiti akikabidhiwa barua kwenda kwa Yoabu kuyakabiri mapambano katika mstari wa mbele hata akakata roho. Damu ya John Huss yadhihirisha Njia itakavyokuwa.Yaonekana damu ya Yesu na mitume katika Njia hii, wengi walipita njiani wakidhihakiwa na kutukanwa, wakizungukazunguka katika nyika na tambarare wakiitetea Njia kuu,ni watu ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao, ipo damu ya Stefano aliyepigwa mawe hata akafa akiomba. Ingawa mbele yetu kuna mateso ambayo shetani na watu wake wameyaandaa, sisi tutapita katika Njia hii huku kamanda wetu akiwa msitari wa mbele. Ndiye muasisi wetu atakayeitetemesha hata aipinduepindue dunia hii na kuzikunjakunja mbingu kama ukurasa katika siku na saa ya kuja kwake. Nasi tutatembea na kupita maeneo yote ya hatari hata tuishapo shinda, kwa maana Mungu wetu tunaye mtii na kumtegemea ni mshindi asiyeshindwa tangu kale.

SURA YA NNE

# NJIA KUU

Akishakuwa ametotoa vifaranga vyake sasa hatua ya muhimu sana anayoifanya ni kuwafundisha vifaranga hao namna ya kumtambua adui.Vifaranga hao sasa wanajua kuwa kumbe duniani kuna adui, nao wanapaswa kula na kunywa katika maisha yao huku wakitambua kuwa adui anawanyatia. Sasa mama yao anawaelimisha kuwa "Mkiona kitu chochote kinapita juu yenu pigeni kelele mkimbie na kujificha" hapo vifaranga wanatii agizo hilo na kulikumbuka popote wapitapo wasiliache maana agizo hilo litawalinda na maadui hata mama yao atakapokufa nao watawafundisha watoto wao ili kudumisha kizazi chao.

Tofauti kubwa kama nini kwa binadamu wakati akiwa mtoto bado mama na baba hawakai naye kumfundisha juu ya adui tuliye naye duniani, mtoto anakua na kula na kunywa akiwa ametekwa tayari na shetani maana hajui shetani ni nani, hiki ndicho ambacho sasa wengi wamefikia hatua ya kumuita adui huyo kuwa ndiye Mungu. Kosa kubwa hili limefanya Shetani kutawala kama apendavyo. Kama ni mpira wa miguu shetani anafunga magoli kama apendavyo maana timu yote iko upande wake, hakuna upinzani.

Adui huyu ameipamba dhambi ikapambika ikapata wateja wengi. Wanadamu wanaridhika na ua hili ambalo hata lipambwe kwa gharama lakini sumu yake itaua dunia hii. Tuifananishe dhambi na nini? Je, imefanana na harufu nzuri anayoitoa chatu akitaka kumkamata mbwa ambapo anapoinusa na kuifuata huo huwa ndiyo mwisho wa uhai wake? Je tuifananishe dhambi na mwanajeshi mwenye hekima aliyetengeneza bomu vizuri akalipamba mfano wa keki akawazawadia watoto yatima ambapo walipoikata ili kugawana ukawa ndiyo mwisho wa maisha yao? Lakini dhambi ni mbaya kiasi gani? Je imefanana na mwanamke mjinga aliyeficha maiti ya mumewe katika nyumba yake kwa sababu alimpenda mno asitake kumzika, mwishowe akakimbia na kuihama nyumba kwa sababu ya harufu mbaya inayonuka iliyotoka katika nyumba hiyo? Labda utaniambia dhambi imefanana na moto uliyofichwa katika msitu mzuri unaotegemewa na wengi, lakini moto ulipolipuka ukawa ndiyo mwisho wa msitu huo. Mmoja ataifananisha dhambi na msichana mzuri anayechezea mkia wa mamba katika mto. Ubaya wa dhambi hauelezeki, dhambi inatesa na kuua. Dhambi inaleta huzuni kwa wenye haki. Kama mwanadamu angeelewa matokeo mabaya ya dhambi katika mwili wake angeikimbia kuliko ukoma na kuiogopa kuliko kifo!

Shetani ndiye adui mkubwa wa mwanadamu. Ndiye mwenye umri mkubwa kuliko wakazi wote wa dunia, ni mwenyeji katika dunia hii akiwa na miradi, mashirika na makampuni aliyosambaza dunia nzima. Usishangae shetani ana madhehebu yake naye

anasoma Biblia. Wanadamu wengi wanafanya kazi katika ajira ya shetani bila kujua mmiliki wake. Macho ya wengi yameshatiwa ganzi nao wamemtetea shetani katika ajira, vyuo vya elimu na katika Mabaraza ya kutunga sheria ili mradi wanapata pesa.

Adui huyu halali usingizi, anauma na kupulizia ili usijisikie uchungu na mwisho anakufanya mtumwa wa aibu na kudharauliwa. Ndiye aliyewafanya Taifa la Israeli likavuka mpaka wa maadili na kuiga tabia na mwenendo wa makafiri wakati Taifa hilo likisafiri kuelekea kaanani. Mungu alikuwa amewachagua, akawatakasa na kuwatenga ili wawe watu wa pekee kuitetea nuru duniani. Adui huyu akawarubuni, akawadanganya, akawatawala ufahamu wao na kusimika bendera yake katikati yao nao wasitambue kuwa wako chini ya adui na *bendera* yake inapepea kati yao. Walipomsahau Mungu wakatamani tena kurudi Misri, wengine wakakanusha nuru ile nyuma yao na kusema kuwa siye Mungu aliyekuwa amewaongoza mpaka hapo katika njia hiyo. *(Kumbukumbu la Torati. 31:29).* Nuru ile nyuma yao ikazimika ikiiacha miguu yao gizani nao wakapotoka na kuingia katika giza la maovu. Kwa masikitiko makubwa kama matokeo ya uasi huo watu wawili tu wakaingia katika nchi ile ya ahadi. Wengi waliasi *Njiani* wakamwacha Bwana wakageuka, wakamtumikia shetani ambaye aliwaletea huzuni na mateso mpaka wasiwe tena Taifa teule na mwisho wakawa aibu na dhihaka kwa walimwengu.

Ndivyo itakavyokuwa katika kizazi hiki tena. Maneno haya yakae katika moyo wako tunapoanza kujifunza Njia kuu. Adui ni yule yule hajafa. Kwa masikio yetu tayari tunasikia sauti ya kengere za mbwa mwitu, Kengele inapolia wanaofaidi ni wenye masikio!

Binadamu wote ni wasafiri katika dunia hii. Tunasafiri katika dunia huku tukikanyaga *Njia* hii muda wote tuwapo safarini, tunasafiri kwenda Mbinguni katika mji mtakatifu ambapo safari yetu itaishia hapo. Tunavuka milima na mabonde tukitelemka tambarare, njia ikisonga kila tupigapo hatua hadi tuingie huko ambako tutafika. Msafiri mwenye busara na hekima katika safari yake yampasa kuwa na ramani katika safari yake ama sivyo yapasa aulize mahali alipo kwa kila hatua asafiripo maana yeye ni mgeni vinginevyo atapotea.

Msafiri yampasa pia kuwa na akili ya msafiri akichunga mzigo wake, kujilinda na maadui wanaoibia wasafiri. Msafiri ana nguo anazovaa katika safari ili asichoke maana safari itachukua muda mrefu, anakula chakula cha msafiri akiwa na wazo moja tu la kufika anakoenda.Msafiri hatakiwi kujisahau maana maeneo anayopita yatahatarisha usalama wa uhai wake. Furaha yake itarejea sasa anapoanza kuuona mji anaoundea mbele yake, naye atauingia na kukutana na wapendwa walioachana naye siku nyingi akifurahi kuonana nao tena!.

Ndivyo ilivyo kwa msafiri wa Mbinguni, yeye naye amepewa Biblia kama ramani pamoja na maombi ili vitu hivyo vimsaidie kumfikisha huko Mbinguni. Ramani hiyo ndipo kuna Njia kuu ya kuuingia mji Mtakatifu. Itampasa msafiri awe na akili timamu asafiripo ili asije kapita njia zingine akaiacha njia kuu. Ni njia ambayo wasio safi hawaipiti humo maana pindi waanzapo safari shetani huweka hapo njia kando ya njia kuu. *Na hapo patakuwa na njia kuu, na njia. Nayo itaitwa njia ya utakatifu wasio safi hawatapita juu yake, bali itakuwa kwa ajili ya watu hao wasafirio, wajapokuwa wajinga hawatapotea njia hiyo*. *( Isaya 35:8.*

Musa aliyewaongoza Israel ili wasiiache *njia* alimsihi Mungu amkumbushe na kumfunulia njia hiyo ili Taifa la Israel lifike salama, Musa aliomba, "Basi sasa nakuomba ikiwa nimepata neema mbele yako nionyeshe *njia* yako nipate kukujua ili nipate neema mbele zako. Ukakumbuka kuwa Taifa hilo ndilo watu wako *(Kutoka 33:14.)*Siyo Musa tu aliyeomba bali Daudi pia aliomba Mungu amwonyeshe *njia* yake ili awafundishe wengine *njia* hii. Hili ndilo Daudi aliliomba Ee Bwana unijulishe *njia* yako. Unifundishe mapito yako *(Zaburi 25:4)* Wasafiri wa Mbinguni leo hawatakuwa na hofu ikiwa watakumbuka njia ambamo Mungu amewaongoza maana historia iliyopita yaonyesha Mungu ameshinda siku zote.Hatuna chochote cha kuogopa kwa ajili ya wakati ujao, isipokuwa kama tutasahau njia ambamo Bwana ametuongoza kuipitia na fundisho lake katika historia yetu iliyopita. *(LS196)*

Wasafiri katika njia kuu ndiyo pekee watakaoingia Mbinguni na kuitwa washindi. Safari yao itajaa amani furaha na upendo na uvumilivu bila manung'uniko wawapo njiani. *Njia* hii ndiyo ambayo aliipita Henoko. Ndiyo ambayo Daudi aliomba Mungu amjulishe mapito yake *(Zaburi 143:8)* Ayubu naye alipita katika njia hiyo asikengeuke *(Ayubu 23:11)* wanaopita katika *njia* kuu wanajiepusha na *njia* mbaya *(Zaburi 119:101)* Watakatifu wote wa kale walitembea katika Njia kuu maana *Njia* ya wenye haki yang'aa *(Mithali 4:18)*. Wanaopita katika njia kuu wanakwepa mitego ya shetani *(Zaburi 14:5)* Wokovu unaotafutwa na watu wote unapatikana katika *Njia kuu* (*Matendo 16:17)*

Musa alipata raha na neema akiwa amejulishwa Njia kuu *(Zaburi 103:7)* Akayakubali mausia ya Bwana na kuanza kuongoza Taifa zima hata wakaunywea Mwamba ule wa roho uliowafuata katika *Njia*, na ule mwamba ulikuwa ni KRISTO (*1Wakorintho 10:14)* Kristo alikuwa nao muda wote akiwaongoza katika njia kuu. Yesu ndiye *Njia* ya kweli na uzima *(Yohana 14:6)* "Maandiko ya agano la kale hutoa habari za kristo jinsi alivyosema. Biblia nzima hutoa habarí za Yesu ambaye pasipo yeye hakikufanyika chochote mpaka agano jipya asemapo, tazama naja upesi kumlipa kila mtu" *(SC88)* Huyu ndiye Neno, Kweli, Njia na Mchungaji mwema. Ndiye aliyekuwepo

tangu dunia inaumbwa hata mwisho atakapokuja tena. Israel waliongozwa naye wakiwa kama nguzo ya moto. Ndiye aliyewaongoza Israel njiani, alikuwa tunu ya watu wake Shina la Daudi mwenye kung'aa Nyota ya alfajiri, Ndiye aliyekataliwa na Farao asiwaruhusu Israel waende zao *(DA 51,52)* Ndiye aliyetabiliwa na Musa kuwa atakapokuja kwa jinsi ya mwili asikilizwe (*Kumbukumbu la Torati 18:15)* Huyu ndiye ambaye Petro amekuja akamhubiri kuwa alikuwepo tangu zamani *(Matendo 3:20)*

Aliyemwamuru Ibrahimu ashike agano lake na sheria zake na kumwamuru atahiriwe alipokuwa hata na umri wa miaka 99 sasa ndiye huyu aliyetoa maagizo ya *msafiri* kuwa mtoto atahiriwe siku ya nane *(Mwanzo 17:10,11,12,24)* Ndiye huyo huyo ambaye alikuja kutimiza agizo hilo hilo aliloliweka yeye mwenyewe wakati alipokuja duniani kwa jinsi ya mwili *(Luka 2:21)* Mama yake akatengwa kwa muda ambao Torati iliagiza atengwe hata atakapotakasika *(Luka2:22)* Ndiye aliyemuita Ibrahimu kuwa ni baba wa Imani, kwa sababu Ibrahimu alisikia Sauti yangu akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu na sheria zangu *(Mwanzo 26:5)*

Yesu aliyekuwa na Musa katika *Njia* zake zote ndiye huyuhuyu ambaye ni *Njia* ya kweli na uzima *(Yohana14:6)* Haiwezekani kumtenganisha Yesu na *Njia* ile ambayo Musa alijulishwa. "Musa alipata kile kilichoambatana naye miaka yote ya taabú na masumbufu ya maisha ya utambuzi wa kuwepo kwa yule Mtakatifu. Hakutazamia tu zama za kufunuliwa kwa kristo katika mwili bali alimwona Kristo akiambatana na majeshi ya waisraeli katika safari zao zote." *(ED63)* Wala hajainuka tena katika Israelí nabii kama Musa ambaye Bwana alimjua uso kwa uso. (*Kumbukumbu la Torati. 34:10)*

Baada ya kifo cha Musa maagizo ya *Torati* hayakubadilika. Kuiba kuliendelea kuwa dhambi, kuzini kuliendelea kuwa dhambi mpaka kuja kwa Yesu katika agano jipya. Musa aliwafundisha Israeli na kusisitiza juu ya *Torati* na umuhimu wake, kwamba watu wasiasi kwa sababu ni agano kati ya Mungu na watu wake, wangepaswa kutii ili wawe wakamilifu nao hawakupaswa kuiacha *Njia hii kuu*. Fundísho hili liliendelea daima. Kila nabii wa Mungu aliyeinuka alifundisha *Njia kuu*. Maagizo haya yaliendelea mbele daima huku wakipokezana na kurithishana tangu Musa, Yoshua, Samweli, Nehemia, Daudi hata wakati wa agano jipya.

Yesu alikuja kuwarudisha watu kurudi katika Njia kuu baada ya wengi kuasi na kupenda dini kuliko maagizo ya Manabií.Moja ya kazi ya Yeremia aliyopewa na Mungu ni kuwaonya watu walioiacha *Njia* hii na kuwasihi wairudie. Aliwaonya wairudie wakawaulize wenzao walimopita wazee wa Imani yaani Musa, Ibrahimu, Isaka na Yakobo, lakini walikataa. Je, walikubali? *Bwana asema hivi simameni katika Njia Kuu mkaone, mkaulize mapito ya zamani, i wapi Njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo*

*nanyi mtajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema hatutaki. Nami naliweka walinzi juu yenu lakini walisema hatutaki. (Yeremia 6: 16 – 17.)*

Je, Njia Kuu ambayo Yeremia alifundisha watu warudi ni nini? Mapito waliyopita watu wa zamani walipita wakiwa katika mwongozo gani? Njia hii kuu ni nini nayo yatuhusu nini? "Yeremia alivuta usikivu kwa mausia yaliyotolewa katika Kumbukumbu la *Torati* zaidi ya Manabîi wengine alikazia mafundisho ya *Sheria ya Musa* na kueleza jinsi sheria hizi zinavyoweza kuletea Taifa mibaraka ya pekee kwa roho ya kila mtu binafsi, ili watafakari, kutii na kuifuata *Torati* usiku na mchana". Hii ndiyo *Njia Kuu* waliyopita wazee wa Imani. Wakatafakari *Njia* hiyo mchana na usiku (*Yoshua 1:7)* Hawakuruhusu kitu chochote kuwatenga na *Njia* hii *(Yoshua 1:8)* Maana hii ndiyo *Njia* ya utakatifu ambayo muasisi wake ni Yesu mwenyewe.

"Kristo aliwapa wanafunzi ujumbe wake akisema wafundisheni watu kuyashika yote niliyowaamuru ninyi. Yale aliyoyasema siyo kwa mdomo tu, bali katika *Agano la Kale* yanahusika hapa. Hakuna nafasi ya hadithi na mapokeo, mawazo ya watu au sheria zilizopitishwa na mamlaka ya kidini. *"Torati na Manabii*" pamoja na maneno na matendo yake ndiyo hazina inayopaswa kupelekwa ulimwenguni"*(DA826)*

Hatuna Mungu mpya, ni yule yule tangu kale, hatuna njia mpya ni ileile tangu kale, hatuna Biblia mpya, ni ileile ambayo ni Takatifu. Hatupaswi kudanganyika sheria ya Mungu na maagizo ya Torati ni takatifu kama kiti chake cha enzi kilivyo. Huu ndiyo ukweli wa kupeleka ulimwenguni. Mfereji wa pekee ambao kwa huo Roho hutenda kazi ni ule wa ukweli (*2SM 49)* Tuna wajibu mkubwa kuufuata mfereji huu. Kuna hatari kujiita muumini wakati maagizo aliyotoa muumbaji unayakataa. Ni rahisi kujiwekea utaratibu utakaowatukuza watu kama tutaacha Njia hii inayoturudisha kwa Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yokobo ambaye aliagiza kuwa ndivyo atakavyoitwa milele. (*Kutoka 3:15)*

Utukufu ulioangaza katika kipaji cha uso wa Musa ulikuwa ni mng'ao wa haki ya Kristo. Katika Kristo tu ndimo ulimo uzima, katika kusoma Torati watu wangepata akili na hekima na Mungu angekuwa karibu nao. Torati haikutolewa ili itumike kwa dhuluma na uonevu. Udhaifu unaoonekana leo katika Madhehebu ni kwa sababu Njia kuu imeachwa *(Kumbukumbu la Torati 4: 5 – 8)*

Waliopewa maagizo haya walikuwa ni watu kama ulivyo wewe, na wengine waliokataa walikuwa wanadamu kama ulivyo wewe. Kuna haja ya kurudi katika Njia kuu. Ni kweli tunaokolewa kwa neema lakini hakuna neema inaoturuhusu kukataa sheria ya Mungu kwa maana Musa aliandika juu ya haki itokayo kwa sheria yake ya kuwa mtu afanyaye hiyo ataishi kwa hiyo.*(Warumi10:5)* Kuiacha Torati kunatufanya tutengane na

Kristo aliyetoka kwa Waisraeli. *(Warumi 9:5)* Ni Kristo yule yule Jana leo na hata milele ndiye aliyempa Musa torati.

Ikiwa tutamhubiri kristo bila Torati hakuna mtu atakayevutwa kwa Yesu. Watu watajaa tu katika Madhehebu lakini hawatatakasika kwa sababu ni Sheria tu inayotuvuta sisi wadhambi kwa Kristo *(1SM 241)* Kwa sababu Utukufu wa Kristo unadhihirika katika sheria ambayo ni nakala ya tabia yake *(1SM240)* Je, Ni wapi Kristo na Sheria hukutana pamoja? Ni pale msalabani.! *(1SM 240 – 241, SDA Bible Commentary vol 5 ukurasa 1133)* Ni pale Msalabani ndipo mdhambi anapomuona Kristo na kustaajabu, kwa nini mtu huyu mwenye haki aliuawa? *Ni kwa sababu ya Dhambi,* Dhambi gani? *Uasi wa sheria*. Tusemeje basi Torati ni Dhambi? Hasha walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria *(Warumi 7:7)* Basi Torati ni takatifu na ile Amri ni takatifu na haki na njema *(Warumi 7:10)* Hivyo basi torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo ili tuhesabiwe haki kwa Imani *(Wagalatia 3:24)*

Injili inayohubiriwa bila Torati hailengi kuinua maagizo ya Yesu yaliyopo katika *Agano la kale* ambalo Njia kuu imeanzia huko. Hatutaeleza sana zaidi ya hapa. Hii ni nuru kidogo tu kukufunulia kile kilichoachwa. Ukweli zaidi juu ya nuru hii rejea katika Biblia na nukuu ambazo zimewekwa wazi sana juu ya Njia hii katika 1SM211-225,PP 363 – 373, 49, 63,64, 66, 70,349, 67, 102, 104.

Kuiacha njia hii ni kumkataa Yesu. Wakati wa uhai wake Musa alifundisha kuwa ikiwa watu wamepotea katika safari ya kumtafuta Mungu warudi kuuliza mababu wa kale mle walimopita. Maneno haya yanatuhusu leo pia. Migogoro na kutoelewana katika madhehebu ni matokeo ya kuiacha Njia kuu je tufanye nini tuwe salama? Je ninani leo atatuonyesha Njia?*"Kumbuka siku za kale, tafakari miaka ya vizazi vingi muulize baba yako naye atakuonyesha. Wazee wako nao watakuambia". (Kumbukumbu la Torati. 32:7)*

Wamissionari walioleta Injili Afrika walituletea ikiwa na mapungufu, Walifundisha kuwa Torati inayoelezwa ni Amri Kumi tu, lakini Torati inajumuisha Mausia, Baraka, Maagizo, Amri, Sheria, na Hukumu kama tulivyoona Mwanzo. Kuna maneno ambayo Yesu alizungumza mwenyewe kuhusu Torati *(Mathayo 5: 17 – 19)* akasisitiza kuhusu Njia kuu ilipoachwa. Muda umefika ukubali kuwa tumeiacha Njia kuu.

Ninaanza kukuonyesha baadhi ya mafundisho ya Njia Kuu. Siogopi kueleza Njia hii kwa sababu watu wengi hawaifuati. Siogopi kuifunua Njia hii ambayo kundi Kubwa la wakristo limeikanyaga na kuiacha. Sishindwi kuiandika habarí zake eti kwa sababu wewe usiyejua utashangaa mno na kupinga ili kutetea msimamo wako. Siandiki juu ya *Njia* hii ili kukuudhi wewe usiyeitaka au kukuomba uipite wala sikuombei utakaposoma uikatae. Najua kuwa

shetani anao mawakala wake kila dhehebu ili kuhakikisha Njia hii haifundishwi. Kukataa kwako kuifuata Njia hii hakunitishi kwa sababu wewe sio wa kwanza kuikataa na wala wewe sio mzuri sana kwa Mungu kuliko wale wachache waliokubali kuifuata.

Njia hii inafunuliwa kwako ili kukuandaa kwa ajili ya saa ya hukumu ya mwisho. Malaika sasa wanatangaza kwa maumbo ya wanadamu kuwa watu wamrudie Mungu maana saa ya hukumu yake imekuja *(Ufunuo 14:6)*. Hukumu ya Mungu haiwezi kutangazwa ikiwa duniani hakuna *wahalifu* wa sheria Takatifu. Ujumbe huu umekufikia ili ukubali au ukatae kwa ajili ya tukio kuu la hukumu kuu ya haki inayokuja. Siku utakapoitwa hukumuni ujumbe huu utaletwa mbele yako kama ushahidi wa maamuzi yako. Hapo katika siku hiyo ndiyo utakapokumbuka thamani ya ujumbe huu kukufikia wewe. Hakika siku hiyo ipo karibu!

Biblia ni kitabu kinachoaminiwa na watu wa Mungu wote duniani. Biblia ndiyo Sauti ya Mungu duniani, Sauti hii haipingwi kamwe! Kitabu hiki kimejengwa juu ya msingi Imara wa upendo ambao umedhihirishwa katika Torati, tunaposema Torati tuna maana vitabu vile vitano vya Musa yaani Mwanzo, Kutoka, Mambo ya walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati. Njia kuu ambayo itapeleka watu mbinguni imefunuliwa humo. Ni njia ambayo msafiri upitapo hupaswi kuchepuka kushoto wala kulia *(Yoshua 1:7–8)* maana muasisi wake ni Mungu *(Kumbukumbu la Torati 9:10)* Wahubiri wote walipita huku wakihubiri juu ya Njia kuu bila kuacha. Tangu Musa mwenyewe hata Yoshua mpaka Samweli walihubiri Torati na Sheria. Daudi akikaribia kufa kamuusia mwanawe Sulemani aitii Torati asiidharau *(1Wafalme 2: 1-3)* hekima na mafanikio ya Sulemani ni kwa sababu alishika torati hata Mungu akambariki. Waisraeli walipata nakala ya Torati kwa Makuhani ambao walikuwa walimu wa Torati *(Kumbukumbu la Torati. 17: 18 – 20)* ili wafundishe vizazi vyote njia kuu itakayoleta wokovu.

Kuna wakati watu waliacha kusoma Torati ikapotea hata wasijue mahali ilipo. Mfalme Yosia alipomtuma mtumishi kwenda kwa kuhani, mtumishi alirudi na kitabu cha Torati ambapo walipokisoma mfalme Yosia alirarua mavazi yake baada ya kugundua maovu yaliyoingia kwa kuasi Torati. Kwa kuacha Torati ni maovu gani yaliingia katika Israeli?

*Watu waliabudu Jua, Mwezi na Nyota kinyume na Njia kuu, na kuruhusu Ibada ya Mungu Mke, Mashoga nao wakakaribishwa na kuhudumu katika Nyumba za Ibada soma 2 wafalme sura ya 22 na 23.* Mambo haya ndiyo tunayoyaona leo katika madhehebu. Kuiacha njia kuu kunawapofusha watu maana dhambi inajulikana tu kwa njia ya kusoma Torati *(Warumi 7:7)*

Nehemia akiungama dhambi za Taifa alisimama katika mimbali na kuisoma Torati ambapo watu waliposikia yaliyomo katika Torati walilia machozi *(Nehemia 8: 4,9)* Nehemia akathibitisha umuhimu wa Torati kwamba inapaswa kuheshimiwa pamoja na maagizo, Sheria, na hukumu. *(Nehemia 1: 7 – 10)* Wakati wa Makambi wana wa Israel wakiongozwa na Nehemia walifanya kutaniko Kubwa wakiwa makini kuisikiliza Torati *(Nehemia 8: 18)* Kuna wakati walisoma kitabu cha Torati masaa manne wakiwa wamefunga na kuomba ili wamkaribie Mungu *(Nehemia 9: 1– 3)*

Ayubu yule mtu wa Mungu aliitwa mkamilifu kwa sababu alifuata njia ya Bwana *(Ayubu 1: 1 – 5)* hata alipoambiwa na mkewe amkufuru Mungu akakataa *(Ayubu 2:9)* Ayubu hakukengeuka katika Njia kuu aliyatunza maneno ya Mungu na kuzishika amri zaidi ya riziki yake *(Ayubu 23: 11 – 12)*

Mfalme Ahasuero alipompandisha cheo Haman yule mwagagi, watumishi wote walianza kumsujudia maana ndivyo alivyowaamuru. Hapa kuna shujaa aliyeitwa Mordekai, Huyu ni Masalio aliyesoma Torati akakataa kumsujudu mwanadamu maana aliisoma amri ya Pili. Hata Haman alipoona Mordekai hainami wala kumsujudia alighadhabika sana akaazimu kuwaangamiza Wayahudi wote. Ndipo Hamani alipo mweleza Ahasuero juu ya Masalio wengine wasiokubali kutii sheria za wanadamu. Watu hao walitawanyika kila mahali kama ilivyo leo. Sheria ikapitishwa Mordekai na wengine wanaoifuata Njia kuu wauawe. Amri ikatiwa muhuri tayari mauaji kuanza. Mji wa Shushani ukafadhaika. Kulikuwa na mauaji ya kutisha kwa wayahudi hao mpaka Mungu alipoingilia kati. Soma kisa hiki katika Esta 3:14, 4: 1 – 5: 14. Njia kuu imeendelea hata wakati wa Isaya na Yeremia aliyetumwa na Mungu kuwarejesha Israel katika Njia kuu *(Yeremia 6: 16 – 17)* Yeremia aliithibitisha torati hata nabii Ezekieli aliyedumisha Torati akiweka pamoja maagizo yatakayodumu milele ikiwa ni pamoja na kutomkaribia mwanamke akiwa katika kutengwa kwake, pamoja na kuwapa wenye njaa chakula kuwa ni maagizo matakatifu ambayo mzizi wake upo katika Njia kuu *(Ezekieli 18: 5 – 9)* Huyu ni nabii aliyesisitiza Utunzaji wa Sabato ambayo ipo katika Njia kuu na kwamba wanaomwabudu Mungu ni wajibu kwao kutotia unajisi vitu vitakatifu *(Ezekiel 22: 25 – 26)* maana duniani kuna shetani ambaye amekuwa akirarua waumini kwa kutumia Manabí wa uongo. *(Ezekiel 34: 1 – 10).*

Ni kosa kuweka utaratibu wa Ibada ambao hauko katika Njia kuu. Wana wa Israel ni mfano wa kanisa la mwisho. Paulo anaeleza akithibitisha kile Mungu alichowapa kuwa walikabidhiwa maagizo, Torati na ahadi zake. *(Warumi 9:4.*Njia kuu tunaiona ikiendelea tangu mwanzo mpaka wakati Daniel anapofunuliwa njozi ya wanyama watakaoinuka na kupinduana mpaka kipindi cha mnyama wa nne, atakayewatesa watakatifu kama katika kipindi cha Mordekai.

Njia Kuu imeendelelea mpaka wakati wa agano jipya. Mahubiri ya Yona yalilenga kuwarudisha watu katika Njia kuu. Mfalme wa Ninawi alitii Torati akasalimika na Taifa lake lote. Amini nawambieni Mfalme wa ninawi anahitajika leo kuwatubisha walimwengu maana Njia kuu imeachwa! Nabii Zekaria anatuambia kitakacho tokea muda mfupi ujao kwa wale wanaofuata Njia kuu *(Zekaria 8:23)* Malaki anayefunga kurasa za agano la kale anasisiza Torati na kwamba kabla ya kuja kwa Yesu Mungu atainua watu wenye Roho ya Eliya kwa ajili ya kuitengeneza Njia kuu iliyoachwa ili pawepo na Masalio wa Mungu watakaorudisha Nuru yote iliyopotea *(Malaki 4: 4–5)*.

Tumetoka katika agano la kale na njia hii sasa tunaingia nayo katika agano Jipya. Njia kuu inatoka katika unabii wa Malaki na kuingia katika agano jipya. Kitu cha kwanza kinachohubiriwa muda mfupi kabla ya kuja kwa Yesu ni kuitengeneza *Njia* Kuu. Yohana mbatizaji alimjua Kristo kupitia vitabu vya Manabii *(8T331–332)* Yohana mbatizaji alikuja akiwasihi watu watengeneze Njia ya Bwana na kunyosha mapito yake.

Njia Kuu ni Njia ya BWANA ambayo ilitabiriwa na Isaya mwana wa Amozi aliyeishika Torati ya Musa hata Mungu akamfunulia yatakayotokea wakati wa kuzaliwa kwa Yesu *(Isaya 40: 3 -5)* Yohana mbatizaji anawahubiria watu wafuate Njia hii mpaka Yesu anapokuja kuwadhihirisha kuwa yeye mwenyewe ndiye muasisi wa *Njia hiyo* na ndiye aliyeianzisha! Kumbe wasafiri waliokuwa wanasafiri wakipita Njia hiyo walikuwa wanamfuata Yesu! Sasa Yesu anawaambia *mimi ndimi Njia ya kweli na uzima (Yohana 14: 16)* hakuna atakaye mwona Mungu pasipo kupita Njia hiyo kuu.

Akiwatahadharisha watu wa leo kwa kinywa chake kuhusu Njia hiyo ya kale, Yesu anakataa kuwa hakuja kuifuta hiyo Njia ila itaendelea mpaka mwisho wa dunia. Yesu anajifunua na kusema *"msidhani ya kuwa nalikuja kuitangua Torati au Manabii la, bali kutimiliza, kwa maana amini nawaambia mpaka Mbingu na Nchi zitakapoondoka Yodi moja wala nukta moja ya Torati haitaondoka hata yote yatimie. (Mathayo 5:17–18)* Hivi ndivyo wasafiri na wabebaji wa nuru duniani walivyopokezana wakikabidhiana huku wakiwa katika Njia kuu bila kuikwepa.

Gari moshi linapopita katika njia yake hupita likiwa katika hali yake na rangi ile ile na abiria wale wale walioingia katika Gari moshi. Kuna wakati Gari moshi hulazimika kupita na kuingia katika pango ambamo mna njia yake. Hii ni kwa sababu ya jinsi lilivyoundwa kwamba huwa halipandi mlima. Kwa hiyo linapoingia katika pango linasafiri mpaka linapokuja kutokeza upande wa Pili wa pango au shimo ambalo njia imetokeza, lakini linapotokeza hutokeza likiwa na rangi ile ile, dereva yule yule, abiria wale wale wenye umri ule ule na injini ile ile.

Hii ni tofauti kubwa sana  ambayo inatia kinyaa kwa Yesu muasisi wa Njia hiyo. Wakristo wa leo ni tofauti kubwa na wale wa kale kama nini! Kama Ibrahimu angefufuka leo na kuwaona wanaodai ni wakristo huenda angerudia usemi ule wa Yesu kuwa ninyi ni wa baba yenu Ibilisi. Kama angefufuka leo Henoko yule aliyeishi miaka 300 bila kutenda dhambi angeingia kanisani na kusikiliza watu wanao daiwa kuwa wamejazwa na roho katika madhehebu, bila shaka angejua kuwa  *Njia kuu imeachwa.* Ikiwa leo Musa angefufuka na kudai amri za Mungu katika maisha ya wakristo wengi wangeaibika kuonekana kumbe hata amri zenyewe zilishabadirishwa siku nyingi bila wao kujua *(Kutoka 20:1 – 17)*

Ikiwa Nehemia yule mwanamatengenezo mzuri wa kweli ambaye ndiye aliyeirejesha Njia kuu baada ya wengi kuiacha angefufuka leo angeshangaa kuyaona yanayotokea. Nehemia alikuwa na njozi ya kujenga ukuta na kutengeneza mji licha ya upinzani mkubwa alioupata kwa San balati, Mhoroni na Tobia lakini alisimama imara katika Njia kuu asitikisike. Aligombana na *mashehe* baada ya kuiacha nyumba ya Bwana. *Nehemia ndiye aliyerudisha ule msingi Mtakatifu wa Sabato ya kweli isiyobadilika baada ya watu kuendelea kuuza na kununua hata masaa ya sabato(Nehemia 13: 18 – 19)* Huyu ndiye aliyekemea tabia ya watu wa Mungu kuoa binti wa kigeni, akaonya dhambi aliyoifanya Sulemani isirudiwe tena na wote  wanaopita Njia kuu. Je, njia  Kuu inapoachwa watu wa Mungu wafanye nini? Je kanisa linapoacha Njia na  kuamua kurudi Misri badala ya kwenda Mbinguni kazi ya Mungu itafanywaje? Watu wa Mungu wafanye nini? *Ni kurudi kwenye Njia Kuu.* Je amani upendo na furaha vitapatikanaje katika madhehebu ya leo licha ya migogoro iliyopo? *Ni kurudi katika Njia kuu*. Kuanzia  hapa na kuendelea nitaanza kuonyesha baadhi tu ya ukweli wa thamani wa milele ambao ni msingi wa  kila msafiri anayepita Njia kuu.

## AFYA

"Au hamjui ya kuwa miili yenu ni hekalu la Roho mtakatifu aliye ndani yenu mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe maana mlinunuliwa kwa thamani, basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu *(1Wakorintho 6:19–20)* Lishe ya Mungu katika Njia kuu imetolewa katika Mwanzo 1:29. Mungu akasema tazama nimewapa kila mche utoao mbegu na kila mti ambao matunda yake yana mbegu vitakuwa ndicho chakula chenu.  Mungu pia aliwapa Israeli lishe kutoka mbinguni ambayo ipo katika kutoka 16:4-35. Mungu alipoongoza Israeli katika njia kuu wakienda kaanani alifuata mpango wake akiwa na lengo kuwafanya watakatifu wenye furaha na wenye afya.

Danieni  pia na rafiki zake ni mfano wa Biblia kuhusu asili ya lishe bora. Msimamo wao mtakatifu wa kweli na mnyoofu usiopinda ni kemeo la daima kwa kila msafiri wa mbinguni. Na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza mfalme akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake.

(Danieli1:8–20) Mungu anatuongoza hatua kwa hatua katika Njia hii kwenda mpaka kwenye mpango wake. wa awali kwamba mtu ataishi kwa kula mazao ya asili ya nchi.

Nafaka, kokwa, na mboga za majani ndiyo lishe aliyotuchagulia Mungu. Vyakula hivi rahisi vinaleta afya na lishe ambayo haiwezi kuletwa na chakula cha mchanganyiko kinachousisimua mwili. Biblia inataja kuwa chakula ni kile kinachotoka ardhini yaani kile alichotoa yeye.Katika ardhi ndimo kitokamo chakula na chini yake hupinduliwa kama kwa moto. Huyameesha majani kwa mboga kwa matumizi ya mwanadamu. Ili atoe chakula katika nchi. *(Ayubu 28:5, Zaburi 104:14)*

Tangu Mwanzo Mungu alichagua mazao ya nchi kuwa ndiyo lishe bora. Aliruhusu kutumia mboga hata kabla ya dhambi *(Mwanzo 3:18)* Miili yetu ni mali ya Kristo, maana ameinunua kwa thamani, kutii kanuni za afya ni wajibu wa kila mmoja. Mwache Mungu ayapange mambo ya maisha yako. Kama mtoto mdogo yakupasa kuyatumaini maongozi yake ambaye atailinda miguu ya watakatifu wake *(1Samweli 2:9)*

Upishi si elimu ya kudharauliwa. Ni kazi muhimu zaidi katika maisha ya kila siku. Kila mke ambaye hajui kupika chakula kinacholeta afya yampasa kujifunza juu ya jambo hili. Hii ndiyo elimu takatifu ya awali ambayo kila msichana anapaswa kujifunza. Chakula kilichopikwa vibaya kuharibu mwili daima kwa kudhoofisha viungo vinavyotengeneza damu, huchafua mwili na kuleta ugonjwa na hali ya harara ya kukasirika upesi. Maelfu ya watu wanakufa kwa sababu ya upishi mbaya.Watu wengi wanakufa kwa upishi mbaya.

Wale waliozoea kutumia vyakula vilivyokaangwa na kuchanganywa na viungo vingi vyenye kuchochea viungo vya mwili kuharakisha mwendo wa damu wana tamaa ya kula isiyo ya kawaida. Hawawezi kupendezwa na chakula kisichololezwa kilichopikwa kawaida. Itamchukua muda mrefu mtu kama huyu apendezwe na chakula cha kawaida na tumbo lake lipone na matumizi haya Mabaya. Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula? Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha? Nisikilizeni kwa bidii mle kilicho chema na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono. *(Isaya 55:2*) Wajibu wetu wa kwanza ambao tutadaiwa na Mungu na wanadamu wenzetu ni kuzitii sheria za Mungu ambazo ni pamoja na sheria za afya *(3T164)*

Hata hivyo mahali bora pa kupata afya ni kuishi Mbali na miji mikubwa. Sio mapenzi ya Mungu kuwa watu wake waishi katika miji ambapo daima kuna makelele ghasia na machafuko. Watoto wanapaswa kuepushwa na jambo hili kwa maana mfumo mzima unaharibiwa kimaadili haraka pamoja na msongamano wa watu Magari na makelele *(2SM357)*

Kwa wengi waishio mijini bila hata ya kuwa na mahali padogo pa majani na kijani kibichi wakaweka miguu juu yake ambao wamezoea kuona mahali pachafu, penye uozo, vichochoro vifinyu yenye mavumbi na moshi kama wangepelekwa Mbali na miji hiyo sehemu ya mashamba ya rangi ya kijani, misitu na vilima na vijito na anga wazi na safi, hewa safi ya vijijini kwao jambo hili lingeonekana ni sawa na kuona Mbingu mpya.Tengeneza kazi yako huko nje jifanyizie kazi yako tayari shambani ukiisha jenga nyumba yako *(Mithali 24:27)*

## UHUSIANO

Tazama jinsi ilivyo vyema na kupendeza ndugu wakae pamoja kwa umoja! *(Zaburi 133: 1)*.Ni mpango wa Mungu kuwepo na upendo na amani katika umoja miongoni mwa wanadamu kama ilivyo kwa Kristo na kanisa lake. Uhusiano huu ni maandalizi tu ya uhusiano mwema ujao wa umilele . Hakuna anayepaswa kumchukia ndugu yake anayemuona na kudai kumpenda Mungu asiyeonekana. Katika njia ya haki kuna uhai hakuna mauti katika mapito yake *(Mithali 12:28)* Upendo furaha na amani ndiyo tabia ya Masalio katika Njia Kuu. Hakuna nafasi ya kugombana Njiani, maana sisi wenyeji wetu uko Mbinguni *(Wafilipi 3: 20)*

Msiibe wala msidanganye, usimchukie ndugu yako usimdhulumu jirani yako, usitende yasiyo haki*(Mambo ya walawi19:9-18)* Usimtukane Mungu wala usimlaani mkuu wa watu wa*(Kutoka 22:28)* ko Ukimwona Ng'ombe wa adui yako au Punda wake amepotea sharti umrudishie mwenyewe *(Kutoka 23:4)* Nawe fanya yaliyo sawa na mema machoni pa Bwana ili mpate kufanikiwa nawe upate kuingia na kuimiliki nchi nzuri Bwana aliyowaapia baba zako *(Kumbukumbu la Torati6:18)*.

Umkopeshapo jirani yako chochote kikopeshwacho usiingie katika nyumba yake kwenda kutwaa rehani kwake. Simama nje yule umkopeshaye akuletee nje ile rehani. Naye akiwa ni masikini usilale na rehani sharti umrudishie *(Kumbukumbu la Torati24:10–13)* Kiota cha ndege kikitukia kuwa mbele yako njiani katika mti wowote au chini chenye makinda au mayai naye koo ameatamia juu ya makinda au juu ya mayai, usimtwae yule koo pamoja na makinda.Sharti umwache yule koo aende zake lakini makinda waweza kuyatwaa uwe nayo ili upate kufanikiwa ufanye siku zako kuwa nyingi.*(Kumbukumbu la Torati 22:6 -7)*

Msifuate miungu mingine katika miungu ya mataifa wawazungukao *(Kumbukumbu la Torati 6:14)*. Maneno haya ninayokuamuru leo ya takuwa katika moyo wako nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii na kuyanena uketipo katika nyumba yako na utembeapo Njiani, ulalapo na uondokapo *(Kumbukumbu la Torati 6: 4 – 8)*

Mungu aliyemuumba mwanadamu alijua pasipo kumwonyesha Njia ni lazima angepotea. Huzuni malumbano vingepungua sana ikiwa Watu wangerudi katika Torati ili wajue maagizo ya Bwana. Upendo, amani na maendeleo ya kweli vinapatikana kwa kumcha Mungu aliyeagiza watu wawe na umoja. Nanyi msiende kwa kuziandama desturi za Taifa niitoayo mbele yenu kwa kuwa wao walifanya mambo maovu na kwa ajili ya hayo niliwachukia *(Mambo ya Walawi 20:23)*

Usimdhurumu jirani yako wala kumnyang'anya mali yake. Ijara yake aliyeajiliwa isikae kwako usiku kucha hata asubuhi. Usimlaani kiziwi wala usitie kwazo mbele ya Kipofu bali umche Mungu wako. Mimi ndimi Bwana, usifanye kisasi wala kuwa na kinyongo juu ya wana wa watu wako, bali umpende jirani yako kama nafsi yako. Mimi ndimi Bwana. (*Mambo ya Walawi 19: 13 – 18.)*

"Utupu wa Baba yako wala utupu wa Mama yako usiufunue maana ndiye Mama yako. Utupu wa Umbu lako, binti ya Baba yako au binti ya Mama yako kwamba alizaliwa Nyumbani kwenu au alizaliwa kwingine, utupu wa hao usiufunue.Utupu wa binti ya Mwanao Mume au binti ya binti yako utupu wa hao usifunue kwa maana ndiyo utupu wako mwenyewe. Utupu wa binti wa mkwe wa Baba yako aliyezaliwa na Baba yako yeye ni umbu lako usifunue utupu wake. Usifunue utupu wa Umbu lake, maana yeye ni jamaa aliye karibu.

Usifunue utupu wa Umbu la mama yako wa karibu. Usifunue utupu wa ndugu ya baba yako. Usimkaribie mkewe huyo yeye ni Shangazi yako. Usifunue utupu wa Mkweo mwanamke yeye ni mke wa mwanao usifunue utupu wake huyo. Usifunue utupu wa mke wa nduguyo maana ni utupu wa Nduguyo. Usifunue utupu wa Mwanamke na binti yake. Usimtwae binti ya mwanawe mume au binti yake ili kufunua utupu wake yaani jamaa ya karibu maana ni uovu mkuu.

Nawe usimkaribie mwanamke kufunua utupu wake wakati wa kutengwa kwa ajili ya unajisi wake. Usilale na mke wa mwenzio ukajitia unajisi naye. Usilale na Mwanaume mfano wa kulala na Mwanamke ni Machukizo, wala usilale na Mnyama yeyote ili kujitia unajisi kwake wala Mwanamke asisimame mbele ya Mnyama ili kulala naye ni machukizo" *(Mambo ya Walawi 18:7–23)*

Nawe usipokee Rushwa kwani hiyo Rushwa huwapotosha macho hao waonao na kuyapotosha maneno ya wenye haki *(Kutoka 23:8)* Kwa maana Bwana Mungu wenu

yeye ndiye Mungu wa Miungu na Bwana wa mabwana Mungu mkuu mwenye kuogofya asiyependelea nyuso za watu wala hapokei Rushwa. *(Kumbukumbu la Torati10:17)*

## KAZI

Adamu alipoumbwa alipewa kazi ya kuilima na kuitunza bustani ya Edéni *(Mwanzo2:8–15)* Baada ya gharikaNuhu alianza kuwa mkulima *(Mwanzo 9: 20)* Mojawapo ya amri iliyoandikwa kwa chanda cha Mungu ni kufanya kazi siku sita katika juma *(Kutoka20:9)*

Mibaraka inayokuja bila kufanya kazi haitoki kwa Mungu. Yesu ndiye kielelezo chetu. Yeye hakuwa mzembe katika shughuli hata kushika vyombo vya useremala. Alikuwa kamili katika kazi kama alivyokuwa kamili katika tabia. Aliweka kielelezo kuwa kazi yapaswa kufanywa kwa ukamilifu maana kazi ni kitu cha heshima. Mungu aliweka kazi kuwa kitu cha Mbaraka. Ni mfanyakazi hodari tu ndiye anayepata furaha maishani.*(DA72)*

Katika maisha ya kuuendea utakatifu ilimpendeza Mungu kutoa agizo la kufanya kazi kama moja ya kumuenzi aliyeumba Mbingu na nchi kwa siku 6. Katika kazi kuna ponyaji wa Mungu uletao afya. Sifa na heshima katika uumbaji pale Edén zingedhihirishwa katika siku zetu ikiwa elimu ya kweli ingetolewa kupitia Njia Kuu. Sura ya Mungu tungeiona kupitia katika maua ya kondeni wadudu, anga, miti na mazao ya asili. Kupitia kazi hizo nzuri za Mungu tungemfahamu aliye yote na kumtumikia.

Wakati unaotumika kwa mambo ya kubuni yenye mwelekeo wa Sodoma ungefaa sana kutafakari kazi za Mungu Takatifu katika viumbe vya asili. Elimu hii takatifu kupitia viumbe ilimfanya Henoko akatembea na Mungu Miaka mitatu bila kufanya dhambi naye akatembea katika wajibu wake miaka yote hiyo bila kutenda dhambi *(Mwanzo5:22–23)* Kuna maajabu mengi katika njia kuu ambayo kielelezo cha Henoko ni mfano mzuri wa kuigwa kwa wasafiri wa Mbinguni.

Mungu anahitaji watu watakaofuata kielelezo cha Henoko. Henoko alitembea na Mungu kwa miaka mia tatu kabla ya kuhamishwa kwake kwenda Mbinguni. Hali ulimwengu wa wakati ule ilichafuka kuliko ilivyo sasa, aliielimisha akili yake na moyo wake kuwa daima alikataa kufuata mwenendo mbaya akamweka Mungu mbele asije akamfanyia kosa. Sasa Henoko alikuwa anawakilisha wale watakaohamishwa katika dunia hii pasipo kuonja mauti wakati Kristo atakapo kuja. *Ellen. G WHITE- Sermons and Talks Volume 1 P. 32.*

<u>IBADA</u>

Kanuni ile ile iliyofuatwa na watu wa Mungu siku za Musa na siku za Daudi ndiyo itashikwa na Kanisa la Mungu popote litakapofunguliwa. Mpango uliofuatwa katika agano la kale ndiyo uliyofuatwa na agano jipya na utakaofuatwa na kanisa la Mungu pia. *(AA95)*

Watu wa Mungu wa zamani walimwogopa Mungu wakampa heshima wakiamini neno lake kuwa ndiyo Sauti yake duniani, wakamsifu na kumtii kila walipokwenda tangu katika familia hata katika ibada. Hawakumdharau kwa mavazi yao kana kwamba dini ni kitu cha kudharauliwa. Wakati wa ibada neno la onyo lililolewa, dhambi ikitajwa kwa jina hata watu wakafanya toba ya Dhambi. Kwa ujumla Nyumba ya Mungu iheshimiwa.

Tofauti Kubwa kiasi gani na siku zetu, Ibada za leo zimeingiliwa na Utandawazi wa mawasiliano na mifumo mipya ya mavazi ambayo ni chukizo kwa Mungu. Mwana Humheshimu baba yake na mtumishi humcha bwana wake basi kama mimi ni Baba yenu heshima yangu iko wapi? Na kama mimi ni Bwana wenu kicho changu ki wapi? Bwana wa majeshi awauliza ninyi. *(Malaki 1:6)*

Waumini wengi waliojeruhiwa na adui wanaenda kisimani kuona kama labda watapata faraja lakini wachungaji wengi wamegeukia njia nyingine. Badala ya kutoa neno lenye uzima wamesimama kutetea msimamo wa dini kama mtu ajibuye hoja. Wengi wamekosa faraja. Kuna kundi Kubwa la watu ambao wameanza kusali majumbani mwao. Kwa sababu ya ibada kuharibiwa na sera na dogma. Watu hawa wanaolia usiku kucha kwa ajili ya dhambi zinazofanyika hekaluni siku moja Mungu atasikia kilio chao.Waumini wengi sasa wanaangaliana kama Mbwa na Paka. Upendo ule wa agape umechukuliwa na masengenyo na kiburi mpaka ibada imekosa mvuto wake. Makanisa yaliyoanguka hayaoni tofauti yoyote na kundi la Mungu.

Hakuna andiko katika Biblia linaloruhusu mtu asiye na kasoro *kuomba* akiwa amekaa, au amelala wala kusimama mbele za Mungu. Kwa kuwa Bwana ni mkuu na mfalme mkuu katika miungu yote. Njooni tuabudu, tusujudu, tupige magoti mbele za Bwana aliyetuuumba *(Zaburi 95:6)* Hakuna makosa katika kusujudu mbele za Mungu maana ni ishara ya heshima kwake. Kusujudu na kupiga magoti mbele za Mungu kulifanywa hata na Manabii waliopita.

Roho ya unabii imeandika hivi kuhusu ibada. "Tukisali katika chumba chetu au kanisani inatulazimu kupiga magoti mbele za Mungu. Popote tuombapo ni haki kupiga magoti. Yesu ambaye ni kielelezo chetu akapiga magoti akaomba. *(Luka 22:41)* Kuhusu wanafunzi wake imeandikwa " Hata Petro akapiga magoti akaomba *(Matendo 9:40)* Paulo anasema "Kwa hiyo nampigia baba magoti *(Waefeso 3:14)* Ezra alipokuwa akiungama dhambi za Israel alipiga magoti akaomba *(Ezra 9:5)* Daniel alikuwa akipiga magoti mara tatu kila siku akasali akashukuru mbele za Mungu wake *(Danieli 6:10)*

*Mahali pa sala na wakati wa sala ni vitu vitakatifu vyenye kuheshimiwa kwa sababu Mungu yupo hapo. Malaika wanapolitaja jina hilo hufunika nyuso zao. Je, sisi wenye dhambi tulioanguka tunalitajaje jina hilo kuu? (PK48–49).*

Mungu alichagua watu maalum wa kumuwakilisha katika madhabahu. kumbuka uchafu na doa lolote la kukiuka maandiko lina uwezo wa kuondoa utakatifu *(Mambo ya Walawi 11: 43 – 45, 22:1 -3)* Sura ya kumi na moja ya Mambo ya Walawi ndiyo inayotofautisha kati ya vyakula safi na vyakula najisi. lakini wale wanaotii agizo hili leo wakumbuke pia fundísho unajisi ambalo linahusika na ibada katika sura hiyo. Utakaso sio kazi ya dakika ni kazi ya kila wakati muda wote katika maisha yetu. Kujisafisha roho na mwili ndiyo agizo la vijana pia, jinsi gani kijana aisafishe njia yake? Kwa kutii akilifuata neno lako *(Zaburi119:10)*.Si kila mtu anaweza kuwa mwalimu wa neno la Mungu kwenye Mimbari *(4T118)* Hakuna mtu anayefa kusimama katika mimbari mpaka awe ameguswa na neno la Mungu katika moyo wake. *(4T526, 527)*

Kama mchungaji ni mpuuzi asiyejali na mwenye dhihaka hayuko tayari kutimiza jukumu alilopewa na Bwana, maneno yake ya upuuzi na mzaha yanayopelekea watu kucheka yameshutumiwa na neno la Mungu hayastahiri popote katika Mimbari takatifu labda wachungaji wawe wameongoka la sivyo makanisa yatakuwa dhaifu tayari kufa. *(EV643)* Meza au Deski katika Madhabahu ni takatifu. usilete mambo ya vichekesho. *(EV641)*

## UCHAFU MAHALI PA IBADA

*(Tafadhali usisome sehemu hii kabla hujasoma visa vya wanawake wawili katika mafungu yafuatayo kwa sababu mwisho wa sura hii unawajibika kujibu swali muhimu ambalo litakuongezea uwezo wa kuelewa.)*

| | |
|---|---|
| *1.* | Mwanamke mwenye kutokwa na damu miaka kumi na miwili - Marko 5:25-34 |
| 2. | Mwanamke aliyempaka yesu mafuta na kumfuta kwa nywele zake – Luka 7:36-50 |

Sasa tunaingia mahali panapohusu miili yetu ili kuiweka wakfu wakati wa kumwendea Mungu. Roho mtakatifu anakaa katika hekalu la miili hii. Hapa inakupasa ulegeze akili moyo na roho ili kuruhusu usikivu wa pekee. Ni wajibu wako kuelewa na kuchukua jukumu kuhusiana na utakatifu ambao hakuna mtu atakaye mwona Mungu asipokuwa nao. (*Waebrania 12: 14)*

Nia ya shetani ni kuwafanya watu wadharau patakatifu na kupafananisha na sehemu ya watu wa siasa. Shetani amefanya kichaka na kujengea mafungu mengi ili kuonekana kuwa agizo la kuwa safi mahali patakatifu liliishia msalabani, kudharau agizo ni kukataa

ahadi, kukataa ahadi ni kuchagua adhabu. Kuna adhabu kwa wale wanaodharau mahali patakatifu. Rejea kisa cha Yeroboam *(1Wafalme 13: 1 -10)*

Sheria za damu za kafara ya wanyama ziliishia msalabani. Pia Sheria zinazohusu jicho kwa jicho, jino kwa jino wameachiwa watu wa Serikali, Serikali wamepewa jukumu hilo. Lakini Maandiko ya Torati yanayohusu maisha ya kawaida ya kuwa mtakatifu,maonyo matukufu, Kanuni za afya ya mwanadamu, ahadi zote baraka na laana hazikuishia msalabani bali yanaendelea kutumika nayo ni ya muhimu sana.

Maneno haya "uchafu" na "unajisi" yote yana maana moja katika Biblia. Duniani kumejaa Uchafu wa kila aina. Kila mtu huuchukia uchafu. Serikali zinatenga Pesa nyingi kwa ajili ya kupambana na uchafu hasa katika Miji mikubwa. Kuna uchafu wa mazingira, Uchafu wa mwili na Uchafu wa Roho. Ni jukumu la kila mtu na jamii kwa ujumla kuuondoa Uchafu wa mazingira na kuyaweka katika hali njema. Mungu atawaharibu wote waiharibuo Nchi. Uchafu wa Roho unasafishwa kwa damu ya Yesu kwa njia ya Toba.

Uchafu wa mwili ni jukumu la kila wenye mwili kuuondoa na kujilinda na kuendelea daima kujisafisha ili kudumisha usafi wa mwili. Mungu hapatani na uchafu wowote. Kamwe Muhuri wa Mungu hautagongwa katika Kipaji cha uso wa Mwanamume au Mwanamke asiye Safi.*(5ST216)*

MUNGU HAPATANI NA UNAJISI

| UCHAFU WA ROHO | UCHAFU WA MAZINGIRA | UCHAFU WA MWILI |
|---|---|---|
| Ni Suala La Imani | Ni Suala La Mazingira | Ni Suala Binafsi |
| Unasafishwa Kwa Toba | Unasafishwa Kwa Kuuondoa | Unasafishwa Kwa Maji. |
| Hausababishi Magonjwa | Unasababisha Magonjwa | Unasababisha Harufu Mbaya |
| Binadamu peke yake hauondoi | Jamii inaweza kuuondoa | Ni jukumu la Mtu binafsi. |
| Ni dhambi Mtu Mchafu kugusa vitu Vitakatifu au kwenda katika Ibada Takatifu. Epuka kunajisi vitu vitakatifu. Ni dhambi kuingia mahali patakatifu ukiwa mchafu. | | |

Kumuabudu Mungu mtakatifu ni hiari ya mtu. Kamwe Mungu hamlazimishi mtu yeyote amtumikie, lakini mara unapokuwa umehiari kumwabudu Mungu mtakatifu basi kufuata mashari ya Ibada yake ni lazima. Kwa nini? Kwa sababu ahadi za Mungu huendana na

masharti ya utii. Ibada isiyo na utii kwa Mungu mtakatifu ni chombo cha Shetani tu maana katika mizani ya Mungu utii una uzito mkubwa kuliko ibada. Huwezi kufanya ibada kabla ya kutii agizo.

Uchafu wa Roho una uhusiano na kifo cha Yesu pale msalabani, Lakini uchafu wa mwili hauna uhusiano na huduma ya pale Msalabani. Kwa nini? Kwa nini? Kwa sababu uchafu wa Roho unasafishwa kwa damu ya Yesu kwa njia ya Toba ya kweli wakati Uchafu wa mwili unasafishwa kwa Maji safi na sabuni. Kisiwepo chochote kinachotia unajisi mahali ambapo Mungu mtakatifu anaabudiwa. Usiende mahali pachafu kwa lengo la Kumuabudu Mungu mtakatifu. "Mara kwa mara mahali palipowekwa wakfu kwa madhumuni ya kumuabudu Mungu hunajisiwa kwa tafrija wakiuza na kununua vinywaji na kujifurahisha. Mipaka ya kujizuia hudhoofishwa na nguvu ya kujipenda nafsi, anasa na kujionyesha huongezeka" *(COL33)*

Mungu hapatani na uchafu wowote. Mungu ni msafi na Mtakatifu. Wote waendao mbele zake watajisafisha miili, mioyo na nguo zao ili Mungu asije kuwaacha. Mungu hugeuka na kumuacha mtu mchafu. Mtu yoyote asiyezingatia usafi wa mazingira, nyumba anayoishi na mwili wake Mungu atamuacha maana vitu hivi vinahusika sana na mambo ya utakatifu *(soma 2Wakorintho 7:1, Waefeso5:3)*

*Tena uwe na mahali nje ya kituo kwa kutoka nje, nawe uwe na jembe dogo katika silaha zako, napo uotamapo nje uchimbe kwa lile jembe na kugeuka na kukifunika kikutokacho. Kwa kuwa Bwana Mungu yuatembea katika kituo chako akuokoe na kukutolea adui zako mbele yako, kwa hiyo na kiwe kitakatifu kituo chako, asije akaona kitu kisichokuwa safi akageuka na kukuacha. (Kumbukumbu la torati. 23:12 – 14.)*

"Mtu yeyote kama akitoka shahawa yake ndipo ataoga mwili wake majini naye atakuwa najisi hata jioni. Na kila nguo na kila ngozi ambayo ina shahawa itafuliwa kwa maji nayo itakuwa najisi hata jioni. Huyo mwanamke naye ambaye mtu mume amelala naye kwa shahawa wote wawili wataoga majini, wote watakuwa najisi hata jioni.

Historia ya huduma za hema ya kukutania ya wakati wa Israeli ni fundisho la daima kwetu nalo litabakia hai kadri Mungu atakavyodumu. Je ni kiwango gani cha usafi mahali patakatifu tunachojifunza kupitia hema takatifu ya wakati huo? Imeandikwa hivi katika Roho ya Unabii:-

"Katika kichaka kilichokuwa kinawaka Moto Musa aliambiwa avue viatu vyake maana mahali aliposimama ni patakatifu. Hivyo makuhani hawakuweza kuingia ndani ya hema takatifu wakiwa na viatu miguuni mwao. Chembe ya vumbi waliyokuwa nayo ingeweza kupachafua mahali patakatifu. Walitakiwa kuacha viatu vyao katika ua wao kabla ya kuingia katika hema takatifu, na pia kuosha mikono na miguu yao kabla ya kuhudumu katika hema takatifu au madhabahu ya kutolea kafara. Hivyo somo la kwamba uchafu

wote lazima uondolewe  kutoka kwa wale wanaokaribia uwepo wa Mungu lilidumu kufundishwa"*(PP350)*

Mwanamke yeyote kama anatokwa na kitu na kitu chake alichokuwa nacho mwilini mwake ni damu, ataketi katika kutengwa kwake muda wa siku saba, na mtu yeyote atakayemgusa atakuwa najisi hata jioni. Na kitu chochote akilaliacho katika kutengwa kwake kitakuwa najisi, na kila kitu akiketiacho kitakuwa najisi. Na mtu yeyote atakayelala na mwanamke na unajisi ukawa juu yake atakuwa Najisi  *(Mambo ya Walawi 15: 19 – 24)*

Hakuna anayepaswa kupuuza agizo hilo. Mwanamume na mwanamke kila mtu kwa upande wake amepewa agizo. Shahawa zipo, damu za hedí zipo na agizo lipo. Mambo haya matatu yapo na yanaendelea. Ikiwa shahawa bado ipo basi na damu za hedhi zipo na agizo lipo. Vyote vitatu vinadumu. Huwezi ukatoa agizo wakati damu ya hedhi na shahawa bado vipo. Wengi watawakosesha wanawake kuukosa uzima kwa kuwafariji waache fundisho hili. Maandiko yanaonya wakati huu mtu asikaribie patakatifu wala kugusa vitu vitakatifu.*(soma Mambo ya Walawi 22:1–8)*

Pia laana ya uzazi inaambatana na unajisi (*Mambo ya Walawi 12: 1 -5*) Laana hizo hazikuishia msalabani Yesu alipokufa. Maana mwanamke angali akizaa kwa uchungu. Kilichobadilika ni kutotoa sadaka ya kuteketezwa lakini uchafu unaotoka mwilini bado upo na agizo bado lipo.

Ikiwa damu ya hedhi sio uchafu basi na kinyesi sio uchafu maana vyote hutoka ndani ya mwili. Ni mpango wa shetani kusingizia kifo cha Yesu ili kuwafanya watu wanajisi mahali pa ibada kwa kuingia wakiwa wachafu.  Ndani ya shahawa kuna mbegu takatifu ambazo husafirishwa na maji ambapo yanapogusana na hewa yatokapo nje huwa uchafu. Muda wa kutengwa unatofautiana ambapo shahawa ni siku moja wakati damu ya hedhi ni siku saba. Muda huu wa kutengwa hakuna ruhusa ya kugusa vitu vitakatifu. Huu ndio wakati ambao mtume Paulo alieleza vizuri habari zake *(soma1Wakorintho7:1–5)*Jambo hili ni miongoni mwa mambo ambayo mwanamke ameahidiwa  baraka kama atayatii. Kitendo cha kuumbwa tu mwanamke kiliambatana na ahadi ya kuokolewa ikiwa atatii.

Kuna watu ambao hawaruhusiwi kutoa huduma ya kiroho mahali patakatifu *(soma Mambo ya Walawi 21:16–21)* Jambo hili lilianza tangu mwanzo wa Njia kuu. "Umakini na usafi pamoja na msisitizo wa utaratibu katika vituo vyote vya mikutano na umuhimu wake vilielezwa na kusisitizwa kupitia sheria zilizohusiana na huduma ya hema takatifu. Kila mtu aliyekuwa najisi kwa hali yeyote hakuruhusiwa kuingia katika mkutano au kambini. Maagizo yalikuwa muhimu ili kuhifadhi afya kati ya watu wengi walio pamoja ili kudumisha utaratibu na utakatifu ili Israel waendelee kufurahia kuwepo kwa Mungu kati yao"*(PP375)*

Siku zote sheria za afya zilisisitizwa. Zilikuwa sio tu kwa ajili ya afya bali masharti ya kudumisha kuwepo kwa yule aliye mtakatifu kati yao. Kwa mamlaka takatifu Musa aliwatangazia "kwa kuwa Bwana Mungu yuatembea katika kituo chako akuokoe na kiwe kitakatifu kituo chako *(ED38)*

Maagizo haya hayakuishia msalabani kwani hedhi ya mwanamke na shahawa kwa mwanamume havihusiani na dhambi bali ni matokeo ya uumbaji wa Mungu mwenyewe. Ndiyo maana katika nyumba zetu tunapaswa kuwa na mahali maalum pa ibada. Chumbani, kitandani, si mahali muafaka pa kufanyia ibada. Wengine wamemwendea Mungu huku wakiwa na yale yaliyowatoka, wakanajisi kanisa, vitabu vitatakatifu, viti vya kukalia na watu waliokaa pamoja nao, wengine wamenajisi hata madhabahu. Hatushangai tena mwanamke ambaye hakupewa kazi ya ukuhani tunapoona akiingia katika madhabahu na kunajisi jina la Mungu na kugeuza mpango wa Mungu. Ni nani asiyejua kuwa dhambi hizi ndizo zilifanya majini kuingia madhabahuni na kuongoza ibada enzi za Mfalme Yosia? (*2Wafalme 22:1 –20, 23: 1- 37)*

Wakati huo Wanawake walipanda madhabahuni na kumleta Mungu mke ambaye anauhusiano sana leo na Mpinga kristo, Mashoga pia (Hanithi) wanaosumbua makanisa leo walikaribishwa baada ya wanawake hao kupindua mpango wa Mungu. Mwisho majini yaliongoza ibada bila watu kujua mpaka Torati iliposomwa. Ndivyo itakavyokuwa katika wakati wetu. Kuiacha Njia kuu kumeleta uasi ambao dawa ya kuuondoa ni kurudi kwenye Njia kuu.

Yesu hatakuja kuchukua walioasi neno lake wakadharau utakatifu. Ndiye aliyeagiza usafi akamwambia Musa siku tatu wajitakase kabla ya kuonana naye, ili kudumisha usafi. Mungu akaamuru wajitakase siku tatu wasimkaribie mwanamke *(Kutoka 19:15)* kwa nini wasimkaribie mwanamke wakati wanaenda mbele za Mungu? "Wakati wa siku hizi zilizoingia kati wote walipaswa kuutumia wakati wao kwa kujiandaa kwa Ibada na kuonekana mbele za Mungu. Utu wao na Nguo zao zilipaswa zisiwe na Uchafu wowote. Naye Musa alipowaonyesha dhambi zao walipaswa kuutumia wakati wao kwa kujinyenyekeza wenyewe, kufunga na kuomba ili mioyo yao itakaswe na Uchafu wote" *(PP304.)*

Tamaa mbaya, uchu wa uasherati na mawazo mabaya yaliyojaa katika vichwa vya watu yamewafanya waamini kuwa haiwezekani tena kwa dunia ya leo mwili na roho vikabaki safi. Kuamini mawazo hayo ni kukataa kuwa Injili ni uweza wa Mungu uletao wokovu. Mtego huu umetegwa kwa wale wanaojidai kumngoja Bwana ajapo siku watakapohama dunia hii. Ole kwa kizazi hiki, kisipojitakasa. Kutotubu na ugumu wa mioyo kutapelekea wengi kukataa nuru hatimaye kuja kuhangaika katika siku kuu ile ya uchungu.

Mungu huchukizwa na ibada za mitindo zisizofuata kanuni Takatifu. Mungu hatakuja kuchukua watu wasioheshimu mahusia yake. Wengi wananukia sana kwa nje lakini kwa sababu ya uasi miili yao inanuka. Wengi wanatembea huku wakiwa maiti mbele za Mungu ingawa yaonekana miili yao kwenye makanisa. Maiti hizi hutoa sadaka, na kuimba nyimbo za sifa kwa mdomo tu bali kwa kila tendo jema hawafai, miili yao ina kila sifa ya marehemu ingawa bado wanapumua. Kutojizuia kutawapoteza wengi. *(1Timotheo5:6)*

Manabii waliandika haya kuhusu kuwa na kiasi katika tendo la ndoa, "Enyi wanaume na wanawake, siku moja mtafahamu tamaa ya mwili ilivyo na matokeo ya kutimiza bila kujizuia. Ashiki inayostahili iliyo ya kawaida huweza kupatikana katika ndoa sawa na nje ya umoja huo. Matokeo ya kutimiza tamaa mbaya bila kujizuia ni nini? Chumba cha kulalia mahali ambapo malaika wa Mungu wangeongoza mazoea hunajisiwa na mazoeya haya mabaya.

Kwa sababu ya desturi hizi mbaya za kinyama zenye kuaibisha miili imeharibiwa. Kile Mungu alichokitoa kiwe baraka kimefanywa kuwa laana. Hebu wanaume na wanawake wamchao Mungu wajue wajibu wao. Hakuna mtu ampendaye kweli mkewe atakayemkubalia awe mtumwa na mhudumiaji wa tamaa zake mbovu za mwili. Watu hawa ni wabaya kuliko wanyama wa mwitu, ni mashetani walio katika umbo la mwanadamu, hawafahamu mafundisho ya kweli yenye kuikuza hali ya kuadilisha wala upendo mtakatifu"*(AH124 – 125)*

Mungu hatakaa mahali pachafu. Ndoa ni takatifu, sabato ni takatifu, na nyumba ya ibada na wakati wa ibada ni vitu vitakatifu. Baraka ya ndoa takatifu haivuki mipaka ya neno takatifu na kukuruhusu uingie katika mahali pa sala ukiwa mchafu. Watu wengi leo wanatembea nje ya mstari kando ya Njia Kuu.

Mkumbukeni Daudi yule shujaa. Pamoja na kazi takatifu aliyoifanya kuhani wake hakumruhusu kula mikate mitakatifu mpaka kwanza amejitenga na wanawake siku tatu *(1samweli21:4)* Wenye hekima watakapojitambua hali zao hawatakaribia eneo takatifu wakiwa wachafu *(Hesabu 5: 1 -4)*

Wengine hawaelewi kwa nini wale kumi wenye ukoma walipomwona Yesu walisimama kwa mbali wakapaza sauti *(Luka17:12 –13)* Yesu alipokuwa katikati ya makutano wengi alimtambua mwanamke aliyekuwa na tatizo la kutokwa na damu kuwa amemgusa. Je waweza jua kwanini nguvu zilimtoka Yesu? *(Marko5:25–31)* Wachungaji, Mapadre na Mashehe wasiwapoteze waumini wao katika Jehanamu kwa kutowafundisha kutenganisha baina ya vitu safi na vichafu visivyostahili mahali patakatifu *(Ezekieli 22: 26)*.

Mkumbukeni Labani katika enzi za uhai wake. Tafakari njia zake upate hekima, Labani alikuwa mwabudu sanamu asiyemjua Mungu katika maisha yake. Ni Labani huyu huyu aliyekuwa na vinyago ambavyo alivitumia katika ibada zake za kipagani. Siku moja binti yake Raheli aliviiba vinyago vile akasafiri navyo mbali wakiwa na Yakobo mmewe. Labani alipojua kuwa vinyago vimeibiwa na Raheli alimfuata kwa hasira mpaka akamkuta. Laheli alikuwa ameiba vinyago vya baba yake. Sasa Baba amekuja kuvichukua lakini anamkuta Laheli na vinyago vile akiwa yuko katika hali ya kutengwa kwake yaani wakati wa damu ya hedhi. Labani pamoja na upagani wake alipojua kuwa binti yule alikuwa na yale mambo ya kike alimwacha, hakumgusa wala kuchukua vinyago vile. *Mwanzo 31: 17 – 35*

Labani hakuhesabu gharama za safari aliyotumia kuvitafuta. Kule kujua tu kuwa aliyevichukua alikuwa katika unajisi kulitosha kumrudisha nyumbani bila vinyago. Ingawa Vinyago vyake vilikuwa ni vya kipagani hakutaka upagani wake unajisiwe na yale mambo ya kike.

Fundisho kuu kama nini kwa watu wanaomhitaji Mungu leo? Wakristo wa leo wanadharau fundisho ambalo hata wapagani wa zamani waliliheshimu?. Je wapagani wa zamani waliyajua maandiko ya Mungu kuliko wewe Mkristo wa leo? Huenda ikiwa Labani yule mpagani angefufuka leo asingeingia katika nyumba za ibada kwa sababu ya unajisi ulioachwa tu bila kukemewa. Je ikiwa Labani asingeingia katika madhehebu kwa sababu ya uchafu iweje Mungu mtakatifu aliyetoa agizo hilo awepo katika dhehebu lililonajisiwa?

Mungu alitoa agizo hili kwa watu ambao walikuwa kama sisi na walikabiliana na changamoto kama tunazoziona leo. Mungu hatajali wewe umenajisiwa kwa sababu chumba unachokaa mko wengi. Mungu hatajali wewe umenajisiwa kwa sababu unapokea hela katika mikono ya watu wengi muda wote. Mungu hatakubali ubaki mchafu eti kwa sababu unafanya kazi katika chumba cha kuhifadhia maiti ambacho ni najisi muda wote. Agizo hili halijali wewe gari unalo panda lina watu tofauti tofauti kiasi gani. Mungu hajalegeza kamba hii kwa sababu wewe una majukumu mengi ya kiroho, chama na Serikali. Mtego huu ni miongoni mwa mitego iliyonasa dunia nzima wakati wa gharika wakabaki familia moja tu ya mzee Nuhu walioonekana kutii sheria yake.

Mungu ametoa agizo hili zuri rahisi na jema ili kuwaandaa watu jinsi watakavyokuwa watakapovikwa miili mipya huko mbinguni Mungu asingetoa sheria ambayo mwanadamu hawezi kuitii maana huku ndiko kumpenda Mungu kwamba tuzishike amri zake wala amri zake si nzito *(1Yohana5:3)*

Wale wanaodhani kuwa agizo hili liliishia msalabani mkumbuke kuwa agizo hili limewekwa katikati ya maagizo yatakayodumu mpaka mwisho wa dunia (*Ezekieli 18:5–9)*

Ukiulizwa leo. Kwanini kuiba ni dhambi? Kwanini kuzini ni dhambi? Kwanini watu mnatunza sabato leo? Kwanini leo kaka na dada hawaoani? Majibu yote ya maswali haya mzizi wake ni katika Torati ambako na kanuni za kujitakasa zimeandikwa huko. Moja haliwezi kuishia msalabani na mengine yakaendelea wakati yote yana husika na miili yetu. Wale wanaomsingizia Yesu kuwa aliyaondoa wakasome maneno yake katika *Mathayo 5: 17 – 19, Yohana 5: 45 – 47*

Ellen G White Nabii wa kweli wa mwisho, Nyota ya mwisho ya Rehema kwa ulimwengu, Zawadi ya thamani kwa wanadamu kupitia vitabu vyake vya Roho ya unabii *(Ufunuo19:10)* Nabii huyu alipovuviwa njozi kuhusiana na nyumba za ibada aliandika haya,

*"Tupo hatarini kuwa dada kwa Babeli kwa kuruhusu makanisa yetu kunajisiwa na kujazwa na kila roho mchafu,ngome ya kila ndege mchafu achukizae" Wote waendao mbele zake lazima Miili na Nguo zao zikubaliwe mbele zake. Mbinguni ni mahali patakatifu na Mungu ni mtakatifu na Msafi. Wote wamfuatao lazima miili yao na nguo zao viwe katika hali ya usafi wakijiheshimu wao wenyewe na Mungu pia. Mungu huangalia mambo haya. Wote wafanyao hivyo hawataheshimu jina lake takatifu wakimwabudu huku Mavazi na Mioyo yao ni Michafu. Yeye huzingatia moyo uliotayarishwa, mawazo na mwonekano safi kwa wote wamwabuduo M.S 126 (1901).*

*Mungu hajabadilika, Yeye ni mkamilifu hakika katika mausia yake sasa kama alivyo kuwa katika siku za Musa. Lakini ibada za leo katika Nyimbo, Sifa, Maombi na mafundisho madhabahuni hakuna ule uvuvio wa Roho wa kweli. Badala ya kuhubili ukweli mtakatifu ule wa Roho, Biblia imefundishwa pamoja na sala zilizochanganywa na uvundo Mchafu wa Sigara! Uvumba (Ibada) kama huu shetani hupokea! Huu ni udanganyifu wa kutisha! Huu ni ukosefu mbele za Mungu. Ni matusi kiasi gani kumtukana aliye mtakatifu aishie mahali pa haki pasipo karibiwa! (Ellen G White- Review and Herald March 25,1875)*

Daudi alimtamani Bathsheba yule mke wa Uria akapanga kufanya naye zinaa, lakini pamoja na dhambi hiyo bado Daudi alisubili mpaka mwanamke yule ametakasika ndipo alipomkosea Mungu *(2Samweli 11:4)* Pamoja na dhambi ya uzinzi kulikuwa na mipaka ambayo hata wapagani wa zamani hawakuivuka. Ni fundisho kuu kama nini kwa vijana wa leo wanaotamani kuzini barabarani ingawa wakiruhusiwa wataua dunia hii kabla ya mwisho wake!

Wapo wengi wasioelewa ukweli wa maandiko haya. Ukikataa torati unalaaniwa *(Kumbukumbu la Torati 27: 26)* Wakati watu walipoasi walimrudia Mungu na kumgeukia kwa kusoma torati *(Yoshua 8: 34 – 38)* Wanaosema kuwa torati iliishia msalabani eleweni kuwa Yesu asingekuwa na faida kuja maana kutambua dhambi huja kwa njia ya torati *(Warumi7:7,12,11)* Kwamba mtu afanyae hayo ataishi .*(Warumi 10:5)* Hata Yesu aliihukumu dhambi ili maagizo ya Torati yatimizwe ndani yetu sisi *(Warumi 8:3 – 4)* ndiyo

maana Torati inapatana na ahadi za Mungu *(Wagalatia 3:20)* Hivyo Torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo *(Wagalatia 3: 24)*. Heri walio kamili Njia zao waendao katika sheria za Bwana. Wana amani nyingi waipendao sheria yako wala hawana la kuwakwaza. *(Zaburi119:165)*

Mungu alipochagua Israel watangaze makusudi yake aliweka utukufu juu yao na kuwakuza mno kuliko mataifa yote. Waisrael hawakuomba wafanyiwe hivyo ila ilikuwa ni kusudi la Mungu *(Warumi 9: 14 – 28)* Mungu anajiita Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo (Waisrael) Ni jina lake vizazi vyote *(Kutoka19:15)*

Mungu anapojenga mji mbinguni anauita Yerusalemu ambalo ni jina la mji wa Wayahudi duniani *(Ufunuo 21: 1 -2)* Misingi ile ilikuwa na majina kumi na mbili ya mitume (Israeli) *(Ufunuo 21:14)* Gari lililoshuka toka Mbinguni kumchukua Eliya liliitwa gari la Israeli *(2Wafalme 2: 11 -12)*. Wengine hawaelewi kuwa Yesu ametoka kwa wayahudi *(Yohana 4:22)*

Hatushangai kuona watu wa leo kujiita majina ya wayahudi kama Petro, Daudi, Musa Danieli na wengine. Hii ina maana gani? Maana yake ahadi ambazo Israeli walipewa ndizo ahadi zetu na maagizo ambayo walipewa ndiyo maagizo yetu pia. Kuikataa Njia kuu ni kukataa ukweli, kukataa ukweli ni kukaribisha laana. *(Mwanzo 12:3)*

Hatushangai tena kusikia baadhi ya wale wanaodai ni Wakristo wakikataa Njia kuu. Wingi wa watu hao unathibitisha kile ambacho Yesu alikisema *(Mathayo 7: 13 – 14)* Wanadai Njia hii takatifu iliishia pale kalvary wakati Yesu aliposema "Imekwisha" lakini wanawachanganganya watu wanapowafundisha wasile vyakula najisi na kuhubiri sana juu ya amri za Mungu wakati mambo haya yote yapo katika Njia Kuu.

Wengine watajitetea kwa kusema hawako chini ya sheria, wameokolewa kwa neema kwa hiyo hawana haja ya sheria. Shetani hajaishia hapo tu, amewatumia wengi kuhubiri kuwa torati na patakatifu pa duniani vilihusika tu na wakati ule mbuzi yule wa Azazeri na yule wa Bwana walipowakilisha kuja kwake yule mwenye haki. Watu kama hao watapinga watatudharau na kutukejeli lakini mwisho wataaibika, katika siku ile ya uchungu. Ndipo wakiwa wamechelewa watakapokumbuka umuhimu wa sheria kwamba bila sheria hakuna dhambi. Wakati wakiwa wamechelewa watakumbuka maneno ya wenye hekima kuwa yeye aligeuzae sikio lake asiisikie sheria hata sala yake ni chukizo *(Mithali 28:9)*

Ni aibu mtoto mdogo asiyejua hata kujisafisha akitoka haja kumpandisha madhabahuni ili arukeruke kwa kisingizio cha kutoa huduma ya kiroho.Yote haya yataendelea kadri tunavyosogea mwisho wa wakati maana sauti ya onyo imezimwa, mbwa wameacha

kupiga kelele. Pasipo maono watu huangamia. Roho ya unabii inapodharauliwa tutashuhudia maovu yakingia kwa nguvu na kubarikiwa na mbwa mwitu wenye mavazi ya mwanakondoo.

Mtu mmoja aliyekuwa na pengo la juu na la chini yake wakati alipokuwa akicheka aliwafanya watu wacheke kumzidi yeye. Hii ni kwa sababu ya pengo la meno yake lilivyochekesha kuona. Hayo ndiyo tunayoyaona katika macho yetu miongoni mwa wa-Laodikia waliotayari kutapikwa huku wakijigamba kuwa wako katika Njia ya kweli.

Ni nini Yesu anachohisi moyoni kama si damu yake kupotea bure? Ni nani atakayeziba pengo la maonyo yaliyoachwa wakati ndiyo linazidi kupanuka? Je makanisa haya ambayo wakati wa Nuhu yaliongoza kumkataa mjumbe wa haki yanawatakia mema waumini wake? Kwani madhehebu kuchana vazi la harusi wakati mwanakondoo yu karibu! Mbona talaka imetolewa wakati ambapo watoto wanahitaji upendo kwa Kristo? Iweje makuhani wapasue mtungi wakati huu wa ukame ambapo maji ni muhimu sana? Kwani kondoo kulishwa tumbaku wakati huu wa mnada ambapo unene wahitajika? Ni mchungaji yupi ajitoe uhai wake kwa ajili ya kondoo katika wakati huu wa unabii wa chembe ya ngano kufukiwa ili itoe mazao tele?

Ni kondoo yupi atakayesimamia ukweli wakati huu wa kuchelewa milele ambapo mbwa mwitu wameshika madaraka kanisani na kurarua kundi? Ninapoona nuru hii ikidharauliwa na wengi napata faraja kuamini kile Yesu alichosema kwa huzuni sana kuhusu wakati wa mwisho *(Luka 18:8)*.

Njia hii ndiyo iliwaudhi mafarisayo wakamkamata Yesu na kumtupa nje ya sinagogi.Yesu alikataa mapokeo ya dini akafuata elimu hii takatifu aliyofundishwa katika maandiko ambayo waasisi walipita Njia kuu. Je, Yesu alipokea elimu hii takatifu toka wapi? "Yesu alipokea elimu hii kutoka kwa mariamu na Yusufu. Mtoto akakua kiroho na kimwili huku akishika sheria za Mungu. Yesu hakufundishwa na walimu wa masinagogi. Mama yake alimfundisha mambo ya manabii, zaidi ya mafundisho ya mdomo aliyopata lakini pia Yesu alisoma maandiko ya agano la kale, akili zake zilikuzwa katika sala, na masomo kutoka katika historia ya Israeli *(DA68,69,70)*

Neno la Mungu limejaa utajiri wa kweli ambamo wanawake wa zamani walipita. Walikuwa na kila sifa ya kuitwa heri.Yusufu akiwa nyumbani kwa potifa alishinda dhambi ya zinaa kwa sababu ya elimu aliyofundishwa na Mama yake. Sara yule mke mwema wa Ibrahimu ni kielelzo cha wanawake wa kizazi hiki wanaotafuta unyenyekevu. Musa alipata elimu takatifu toka kwa Mama yake, elimu hiyo ilimsaidia akawa imara hata wakati wa utu uzima. Wanawake wote wajifunze kwa wanawake hawa. Niseme nini tena juu ya wanawake wa biblia. Esta yule shujaa wa Bwana, Miriamu akiwa kando ya bahari, nani asiyejua jinsi mke wa Manoa alivyoitii Torati akapita Njia kuu akimfundisha mwanawe Samsoni tangu utoto wake? Nani asiyejua unyenyekevu wa Elizabeti mama

wa Yohana mbatizaji? Mariamu mama wa Yesu alipita katika njia zote za agano la kale akifuata kila kanuni ya ibada akimheshimu mumewe na kumjali huku akijifurahisha katika Torati mpaka Mbingu zikamtangaza kama mbarikiwa.

Wanawake na wasichana wa leo watasimama hukumuni wakihukumiwa kadri ya ukaidi katika Torati. Miriamu, Anna, Elizabeth na Mariamu ni mifano hai ya vile dada zetu wangekuwa. Bathsheba yule mke wa Uria na mke wa Potifa yule muasherati watasimama hukumuni pamoja na wanawake wa kizazi hiki ikiwa wanawake wa leo wataidharau Njia kuu. Kuna watu ambao mpaka sasa wanamuabudu Mungu bure nao ni Machukizo kwa Mungu. *Mungu hana haja na Ibada yako kuliko ambavyo ana haja na utii wako kwake.Utii kwa Mungu ni bora kuliko Ibada yeyote duniani.*

- ❖ SWALI MUHIMU. Baada ya kusoma Marko 5:25-34 na Luka 7:36-50 jibu maswali yafuatayo:-
  - A. *Tofautisha na kuwalinganisha wanawake hao ambao wote walimwendea Yesu kwa imani.*
  - B. *Mwanamke mwenye kutoka damu alikuwa najisi ndiyo maana Yesu aliuliza ni nani amemgusa. Kwa nini yesu aliuliza hivyo?*
  - C. *Kwa kutumia mafungu ya Biblia elezea ni kwa vipi Unajisi ndicho kitu pekee kinachowatofautisha wanawake hawa?*

SURA YA TANO

# HILA ZA SHETANI

## UTANGULIZI

Tarumbeta imeanza kupigwa watu waingie karamuni huku walioalikwa wakitoa udhuru kwa nia moja. Kuhani anakaribia kutamka neno la mwisho lakini wadhambi hawajali nafasi yao ya pekee. Kwetu sisi tuna umbu mdogo wala hana maziwa, tumfanyeje umbu letu siku atakapoposwa? Mkulima ameustawisha mmea, akautilia samadi mara tatu lakini mmea hauonyeshi dalili ya kuzaa matunda.

Lutu yupo mlangoni pa Sodoma akiwaharakisha wenyeji wakimbie lakini wao wakiendelea na mkakati wa kuinua uchumi na kumwinua mwanamke, ambapo ni dakika chache tu Sodoma itachomwa. Kelele inapigwa kuwaamsha wanawali juu ya ujio wa Bwana arusi lakini hakuna anayekumbuka kutengeneza taa yake.

Tunaishi wakati wa pekee wa thamani ambapo tunapaswa kuamua hatima ya maisha ya milele kabla rehema haijafungwa. Gari la mawingu linaonekana angani likiwa tayari huku wasafiri wakiendelea kula na kunywa na kusahau ujio huo wa pekee. Kuchelewa! Kuchelewa!, Kuchelewa!.

Wakati huu ni wakati wa kusisimua mno kwa kila mwenye mwili. Joka amempa uwezo mnyama. Mnyama amekasirika akijiandaa kutoa amri ya kutouza wala kununua. Roho tatu za uchafu tayari kuwaendea wakuu wa dunia huku dhamiri za watu zikiwa zimetekwa. Hakika mwisho utakuwa wa huzuni. wenye dunia wanataka kufanya kitu chao na dunia. Wapangaji kaeni mkao wa kuihama nyumba maana gharama itakuwa ni kumsujudu mnyama ndipo uwe raia halali wa dunia.

Hivi karibuni kitatokea kitu cha kusisimua sana. Malumbano yale ya zamani yataanza tena. Karani wa shetani sasa yupo ofisini akiratibu hatima ya mwisho kwa wale watakaoikataa bendera yake. Karani ametengeneza kadi ambayo nakala zake zitasambazwa dunia nzima. Wakati hayo yanaendelea Malaika wa rehema nao wanakunja mabawa kuondoka zao. Picha halisi itakapoanza itafanya watu wajute kwa nini hawakufa mapema. Mkono unaosukuma hayo ni wa shetani kupitia Ukristo bandia. Injili inayopelekwa ulimwenguni sasa si ile ambayo Yesu aliiagiza tuipeleke. Kuna Injili ya shetani inahubiriwa duniani.

Wale wanaofanya juhudi kuibadilisha katiba ya nchi na kujipatia nafasi ya kutunga sheria inayolazimisha utunzaji wa Jumapili hawatambui hata kidogo matokeo yake yatakavyokuwa. Ni muhimu mno kila mmoja kuujua Ukristo wa shetani. Jifunzeni Biblia namna ambavyo kamwe hamjapata kujifunza namna hiyo katika siku za nyuma.

## MITEGO YA SHETANI

Katika kipindi hiki cha maovu yaliyotapakaa kila mahali twaweza kujua kuwa hatari kubwa ya mwisho imekaribia. Mawakala wa uovu wanayaunganisha majeshi yao na kuyaimarisha. Mabadiliko ya haraka haraka yanatokea kwa ajili ya utimizo wa mwisho wa unabii. Dhoruba imejikusanya kwa ajili ya kulipuka katika dunia. Dhoruba inakuja ikiwa na mwako wa ghadhabu pasipo huruma. Tufani inakuja ikiambatana na matukio ya kupotea milele kwa wale watakaoshindwa kusoma alama za nyakati na kusimama upande ulio salama.

Madanganyifu ya shetani ni makubwa duniani kiasi ambacho ulimwengu umelogwa kwa uchawi wake hata kujisahau kuwa duniani kuna vita kati ya wema na uovu vinaendelea. Mungu amefunua kile kinachotokea siku hizi za mwisho ili mwanadamu ujiweke tayari na kuepuka madanganyifu ya shetani.

Mwisho wa kila mwenye mwili unatunyemelea huku mlango wa rehema ukifungwa kimya kimya kwa umilele pasipo watu kutazamia. Tunaishi katika dakika za kukata shauri huku wengi wakichagua kupotea milele kwa kutojua huu ni wakati gani. Jukumu kubwa limekabidhiwa kwa wanaume na wanawake ili wapaze sauti kwa maombi kupeleka dua kwa Mungu ili afagilie nyuma wingu hili la maovu na kutupatia miaka michache zaidi ya kufanya kazi ya Bwana. Mungu anawaita watu ambao watawatayarisha watu kusimama katika siku kuu ile ya Bwana.

Wajibu wa kuonya watu warekebishe mapito ni juu yetu watenda kazi wa Mungu yawapasa wawe na ufahamu mkubwa kuhusu kazi ya shetani na wamjue jinsi alivyo. Tunapaswa kuijua picha halisi ya shetani, lugha yake, matendo yake na jinsi alivyotawala wengi. Tunapaswa kuujua ukristo halisi wa shetani, hila zake mitego yake na mahali anapoishi. Tahadhari imeshatolewa kwa kila mwenye mwili, "hofu na shimo na mitego vi juu yako ewe mwenye kukaa duniani". (*Isaya 24:17)*

Watenda kazi wa Mungu wanapaswa kujua mitego ya shetani na kuwatahadharisha watu wajihadhari na adui huyo. Mtendakazi wa Mungu atakayeingia kazini pasipo kutambua hila za shetani na jinsi anavyofanya kazi ni lazima atapotea. Watu kwa hakika wanapaswa wamjue shetani wakiwafundisha wengine jinsi alivyo, umbo lake, sifa zake, mavazi yake, mapambo yake, lugha yake, nyimbo zake, mitume wake, makanisa yake na viongozi wa shetani katika dunia hii. Kwa hakika shetani ana madhehebu yaliyotapakaa kila kona ya dunia. Haya yataendelea kumtaja Mungu na kumkiri kwa midomo huku lakini yakiuteka ulimwengu na kuiga kila tendo la shetani. Mwanadamu ujitambue kwa hakika kuwa unapaswa kufanya uhakiki wa mwenendo upya. Ubongo wako, mawazo yako, maneno, mavazi, chakula chako, vinywaji vyako na utu wako

vinapaswa kulindwa na vingine kuviepuka. Kupitia njia hiyo shetani amefaulu kusimika hila zake katikati yako. Mwe na kiasi na kukesha maana ibilisi kama Simba huzunguka zunguka akitafuta mtu ammeze. *(1 Petro 5:8)*

Tunakaribia mwisho wa historia ya dunia hii na shetani anatenda kazi kwa bidii ambavyo hajawahi kufanya. Anajitahidi sana kutenda kama Mkurugenzi wa ulimwengu wa Ukristo kwa juhudi zisizo za kawaida anafanya miujiza na madanganyo yote. Anatamani kuujumuisha ulimwengu mzima katika umoja ili kufanikisha njama zake huku akijificha upotofu wake ndani ya vazi la ukristo, kujifanya mkristo na hata kujidai kuwa yeye ndiye Kristo mwenyewe, Je ni kwanini watu hawafundishwi juu ya hatari hii? Sababu yake ni kuwa shetani ametawala madhehebu na kuwafumba midomo watendakazi wa Mungu.

Sasa watendakazi wamepewa ujumbe mpya wa amani badala ya kile alichosema Yesu. (Mathayo 10:34). Wanadamu wamepewa chakula ambacho hakina virutubisho vyovyote. Chakula hiki (mafundisho) hakiwezi kuyaamsha madhehebu na hivyo kupitia madhehebu ujumbe wa kweli utapuuzwa na kukejeliwa.

Kwa kadri roho za mashetani zitakavyojidai kuiamini Biblia na kuonyesha heshima kwa kanuni na desturi za kanisa, kazi yao itapokelewa na kukubaliwa kama vile ni mafunuo ya nguvu za Mungu. Shetani anafanya kazi bega kwa bega na wakristo wanaokiri imani lakini ni maskini wa utambuzi wa kiroho kiasi kwamba hawamgundui.

Shetani hushauriana na malaika wake jinsi anavyoweza kuharibu imani ya watu wa Mungu. Anaona kuwa makanisa yanayopendwa na watu wengi yamelazwa na uwezo wa udanganyifu wake. Kwa akili zake za kupendeza na ajabu za kudanganya anaweza kuendelea kutawala. Hivyo shetani huwaongoza malaika wake kutega mitego yao hasa kwa wakati wanapotazamia kurudi kwa Kristo mara ya pili na kuzishika amri za Mungu.

Maumbo ya watu waliokufa yataonekana kwa njia ya udanganyifu mkuu wa shetani na yataungana na yeye aupendae uongo na kuufanya. Wengi watasikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani; na kwa kupitia kwao ukweli wa Mungu utatukanwa. Kazi ya ajabu itafanyika, Wachungaji, madaktari na wanasheria ambao wameruhusu uongo huu kutawala watakuwa wadanganyifu wao wenyewe wakiungana na waliodanganywa.

Mdanganyifu asema, "lazima tuwaangalie watu wanaowaambia watu washike sabato ya Yehova, maana watawaongoza wengi kuiona sheria ya Mungu inavyotaka, na nuru ile inayoonyesha pia huduma ya Kristo katika hekalu la Mbinguni na inavyoonyesha pia kuwa kazi ya mwisho ya wokovu wa mwanadamu inaendelea mbele.

Shikilia mawazo ya watu yawe gizani mpaka kazi hiyo itakapomalizika nasi tutauteka ulimwengu na kanisa pia. Sabato ndiyo suala kuu litakaloamua mwelekeo wa roho za watu. Lazima tuitie nguvu sabato yetu tuliyoianzisha. Tumeshaifanya ipokelewe na watu wote duniani na waumini wa kanisa, sasa lazima kanisa lielekezwe kuungana na dunia kwa kupatiwa misaada.

Tuifanye kazi kwa kutumia ishara na miujiza ili tuyafumbe macho yao juu ya ukweli na tuwavute ili waachane na maswali juu ya ukweli hata wasimuogope Mungu ili wafuate mila na desturi tu. Lakini hasa kusudi letu ni kulinyamazisha kundi hili la watunza sabato. Lazima tuanzishe chuki kuu kinyume chao.

Tutawatafuta watu mashuhuri na wenye hekima wawe upande wetu; tutwapatia madaraka ili watekeleze makusudi yetu. Ndipo sabato niliyoianzisha italazimishwa na kukuzwa ikiwekewa sheria kali. Wale watakao ivunja watafukuzwa wateseke kwa njaa na umasikini. Tutakaposhika madaraka tutawaonyesha jinsi ya kuwatenda wale ambao watakuwa bado hawajakana utiifu wao kwa kanuni za Mungu.

Tumelitumia kanisa la Rumi kuwakamata, kuwafunga, kuwatesa na kuwaua wale waliokataa kujisalimisha chini ya sheria zake na sasa tunayaleta makanisa ya Kiprotestant ili yafanane na dunia maana huo ndiyo mkono wetu wa kulia wenye nguvu. Mwisho tutaweka sheria kuwaangamiza wale wote watakaokataa kujisalimisha chini ya mamlaka yetu.

Wakati adhabu ya kifo itakapopitishwa ndipo wengi walio katika nyadhifa watakapokimbilia upande wetu. Nitawatumia wachungaji mashuhuri wenye mvuto ili waugeuze mvuto wa wasikilizaji wao na kuwatoa kwenye amri za Mungu. Pale maandiko matakatifu yanapokiri sheria kamili ya uhuru itaonekana kama ni nira ya utumwa. Watu watayapokea maelezo ya maandiko matakatifu yanayotafsiriwa na viongozi wao hivyo kwa kuwatumia viongozi nitawatawala watu kama nipendavyo.

Lakini kabla hatujawachukulia hatua hizo kali ni lazima tutumie hekima ya juu kuwadanganya na kuwanasa wale wanaotunza sabato ya kweli. Tutaweza kuwatenga wengi kutoka kwa Kristo ikiwa tutawaletea mambo ya kidunia, tamaa, na majivuno wao watajidhania wapo salama kwa kule tu kuamini ukweli. Kwa kuzama katika tama ya uchu wa chakula na misisimko vitawachanganya hata wasiweze kufanya uchaguzi mzuri na ndipo tutawafanya wengi waanguke.

Lazima tuwachunge kwa hali zote wale wanaomtumikia Mungu ili wasiwe na mali yoyote itakayowasaidia kuwapatia njia kinyume chetu. Ziwekeni fedha mikononi mwa watu

wakubwa watu wa upande wetu.  Kadri wanavyopata mali ndivyo watakavyouharibu ufalme wetu.

Wafanyeni watu wapende fedha zaidi ya kujenga ufalme wa Kristo ambao sisi tunauchukia na hatuhitaji kuuogopa mvuto wao maana kila mbinafsi na mchoyo ataanguka chini ya nguvu zetu na hatimaye atatengwa na watu wa Mungu … Wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu ni wasaidizi wetu kuliko wote, wenye mfano wa utaua lakini hawana nguvu zozote za Mungu tutawatumia kama vibaraka wetu ili tuwavute wenzao waangukie kwenye mitego yetu.

Wengi hawataogopa mvuto wao kwa sababu wanaamini na kushiriki imani moja … na kwa kufanana na dunia watayajaza makanisa mvuto mkuu wa mambo ya kidunia. Hapo hawatakuwa na nguvu ya kupingana na nguvu zetu, kisha wataurudia udhaifu waliokuwa nao zamani wa kutokuomba, Lazima tuhudhurie kila mikutano yao wanapokusanyika.  Lazima tupeleke upinzani mkubwa na kuweka mambo yatakayozuia roho zao zisiusikie ukweli.

Nitajipatia watu wawe ni watumishi wangu wa siri wale walio tayari kupokea mafundisho ya uongo na ukweli wa kutosha wauchanganye ili kuzidanganya roho za watu. Nitawatumia watu wasioamini miongoni mwao ili waelekeze na kuleta mashaka kuhusu ujumbe wa Bwana wenye onyo kwa kanisa lake.  Kama watu watasoma na kuamini maonyo hayo basi tutakuwa na matumaini kidogo sana ya kuwashinda.  Kama tutaupindua mvuto wao wasifuatilie maonyo hayo watabaki katika giza la nguvu zetu za ujinga na kutokuamini na hatimaye tutawapatia vyeo vyetu mwishowe.

Mungu hataruhusu maneno yake kuchanganywa na takataka, ikiwa tutazivuta roho za watu gizani baadaye rehema ya Mungu itawaacha na hapo ndipo atatuachia uwezo kamili ili tuwatawale.

Lazima tusababishe ugomvi, na migawanyiko lazima tuharibu ule uchu wa kupenda mambo ya kiroho ili tuwafanye wawe wabishi, wagomvi, kushtakiana na kuhukumiana ili wadumishe uchoyo na uadui, kwa dhambi hizo Mungu alitufukuza mbele zake, wote watakaofuata mfano wetu yatawapata yale yaliyotupata”  *(TM472 – 475)*

SURA YA SITA

# LUGHA YA SHETANI

Shutumu kubwa limetupiwa kwa kazi na Roho Mtakatifu kwa njia ya watu wanaotangatanga huku na huku wakidai kwamba wanaongozwa na Roho Mtakatifu wakisema kwamba hiyo ndiyo sauti ya roho katika mioyo yao. Lakini hali hiyo inayowatawala siyo Roho wa Mungu. Kule kujisikia msisimko kukifuatwa huishia katika machafuko udanganyifu na uharibifu.

Hali hiyo huendeleza tu kazi ya mwovu. Kwa kuwa kazi ya Roho Mtakatifu ni muhimu sana katika kanisa la Kristo, ni makusudi ya shetani kubuni mbinu za uongo kwa njia ya wakorofi wanao tangatanga na kujipendekeza kwamba wanaongozwa na Roho ili kuchafua kazi ya Roho na kuwafanya watu wa Mungu wasijali maandiko ambayo ndiyo njia iliyowekwa na Bwana mwenyewe.

Basi roho anena waziwazi kwamba Nyakati za mwisho wengi watajitenga na imani wakisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani *(1 Timotheo 4: 1)* Mafundisho haya ya mashetani yamejaa udanganyifu kiasi ambacho Yesu atakapokuja hataikuta imani tena duniani *(Luka 18:8).* Kwa maana kumezuka makristo wa uongo na manabii wa uongo wanaofanya ishara na maajabu yamkini wawapotoshe hata walio wateule *(Mathayo 24: 24).* Katika pambano hili la mwisho shetani anatumia njia ile ile kama ilivyokuwa zamani, isipokuwa pambano lililopo ni kali mno la kutisha ambalo ulimwengu haujaliona. Madanganyo ya shetani ni ya hila mno na werevu mwingi.

Shetani alipoanza kuongea na mwanadamu alitumia lugha ambayo matokeo yake yalisababisha uasi na hata kifo. Vivyo hivyo leo twaona katika onekano la kibinadamu ukafiri wa hali ya makanisa vimeungana pamoja na kuwa katika hatia kupitia lugha ya shetani. Lugha yake ni ya mwanakondoo lakini ikiwa na matokeo ya kifo cha umilele. Kuna lugha inayonenwa na watu wakati wa kuomba ikidhaniwa ni lugha ya Mbinguni. Huu ni Mtego wa Shetani ulionasa wengi.

Lugha hii imejipenyeza kwa siri katika madhehebu kwa mwavuli wa karama za Roho. Roho Mtakatifu hakutolewa ili kuchukua nafasi ya biblia. Shetani amemwaga lugha hii isiyo na maana huku ikidaiwa ni lugha ya Mbinguni. Aidha amewapotosha na msisimko huu wanaoudai ni wa Roho Mtakatifu, kule kujisikia msisimko hufuatia kuishia katika machafuko, udanganyifu na uharibifu.

Hali hiyo huendeleza tu kazi ya mwovu. Shetani anasoma maandiko naye anajua kuwa wale watakaokutwa na uwezo huu hawataokolewa. Lugha hii imetawanywa makusudi

ili kuuhadaa ulimwengu wakati huu, ulokole, msisimko bandia, unenaji lugha bandia na matendo ya makelele vimechukulia kama vipawa ambavyo Mungu amewiweka kanisani. Wengi wamedanganywa hapa.

Wengi hawatosheki kuendesha mkutano mpaka wapate kipindi chenye msisimko na furaha, lakini wakati msisimko na furaha unapokuwa umetoweka wao husononeka zaidi ya walivyokuwa kabla ya mkutano kwa sababu furaha yao haikutoka kwenye chanzo sahihi. Hivi punde kutakuwa na msisimko wa kishetani wenye mchanganyiko wa ukweli ili kupotosha watu. Katika makanisa yale awezayo kuyaweka chini ya nguvu zake za udanganyifu atafanya ionekane kuwa baraka maalum zimemwagwa juu yao haya yanaonekana machoni petu huku wengi wakikimbilia huko watakapopotea.

Lugha ya Mbinguni ni lugha takatifu. Lugha ya Mbinguni inajulikana na viumbe walioko Mbinguni. Mungu anapowasiliana na malaika anatumia lugha inayoeleweka na malaika. Malaika wanapowasiliana na Mungu wanatumia lugha ambayo inafahamika na Mungu pia. Mbinguni hakuna Kreoli wala Pigini. Lugha ya Mbinguni haiathiriwi na mabadiliko wala Misimu. Ni lugha isiyobadilika kama Mungu asivyobadilika. Wanadamu wamepewa lugha zao ili ziwasaidie kuwasiliana, Mungu pia hutumia lugha za wanadamu ili wanadamu wapate kumuelewa.

Mungu alipomtokea Adamu alizungumza kwa lugha ambayo Adamu aliielewa *(Mwanzo3:9– 13)* Mungu alizungumza na Kaini, akazungumza na Nuhu ili ajenge Safina, mawasiliano yalifanyika kwa lugha inayoeleweka *(Mwanzo 6: 13 – 22)* akizungumza lugha inayoeleweka. Musa aliyemuona Mungu alizungumza naye uso kwa uso wakielewana. Ibrahimu asingemtoa Isaka kafara kama Mungu angezungumza kwa lugha isiyoeleweka. Tuseme nini tena kuhusu mawasiliano ya Mungu na Daudi, Sulemani, Ayubu, Isaya, Manoa, Samweli, Danieli na Eliya? Wote hawa walizungumza na Mungu wao kwa lugha inayoeleweka kama mzazi na watoto wake. Amri kumi zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu *(Kumbukumbu la Torati. 9:10)* ziliandikwa kuwadhihirishia wanadamu kuwa hakuna lugha isiyoeleweka ambayo Mungu ataitumia na kamwe hataitumia. Yesu alipokuja duniani alisifu, akaomba na kuhubiri kwa lugha za wanadamu. Kuna ombi ambalo Yesu aliliomba, *(Yohana 17)* kuna sala aliyofundisha. Vyote hivi vinaeleweka wazi. Biblia imeandikwa kwa lugha za wanadamu zinazoeleweka na wanaoandika walijazwa na Roho Mtakatifu.

Tofauti kubwa na lugha za Mashetani zinapopandikizwa kwa waumini, ambapo wale wanaonena nao hawajui wanachonena hata kama wanamtukana Mungu. Shetani amewafundisha kuwa wakati yote hayo yanafanyika wao waseme wamejazwa na Roho

Mtakatifu. Shetani amemwaga uwezo wake kanisa zima kinyume hata na biblia, amevuka mpaka wa kipawa ambacho Mungu hajatenda hivyo katika kanisa kila mtu ana kipawa chake. "Na Mungu ameweka katika kanisa wa kwanza Mitume wa pili Manabii wa tatu waalimu kisha miujiza, kisha karama ya kuponya wagonjwa na masaidiano na maongozi na aina za lugha. Je wote ni mitume? Je wote ni Manabii? Je wote ni walimu? Je wote wanatenda miujiza? (*I Wakorintho 12: 28 29)*

Hakuna aliyejazwa na Roho Mtakatifu atakaye nena lugha zisizoeleweka. Mungu si Mungu wa machafuko. Yesu ambaye ndiye kielelezo chetu alipojazwa na Roho Mtakatifu hakunena kwa lugha. *(Mathayo 3: 16,17)* Shetani hujigeuza geuza na kutenda matendo mema ili kuwachanganya watu lakini ni yule yule. Ameleta dini nyepesi inayopendwa na wengi huku dini ya kujikana ikikataliwa.

Shetani amewaridhisha na jina hili la wokovu na msisimko akawapa uwezo wake wa ajabu, katika uwezo huu mna mamlaka, nguvu lakini hakuna upendo. Uwezo wa kunena kwa lugha unaambatana na maana halisi ya lugha. Basi nisipoijua ile maana halisi ya lugha nitakuwa kama mjinga kwake anenaye naye atakuwa mjinga kwangu *(1Wakorintho 14:11)* Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kutafsiri *(1Wakorintho 14:13)* Kwa maana wewe ukibariki kwa roho yeye aketiye mahali pa mjinga ataitikaje amina ikiwa hajui uyasemayo? *(1Wakorintho14:16)*

Vipawa hivi vya kishetani vimetawanywa duniani pote vikianzia kwa Wazungu ambao nao wametapeliwa. Wengi wanadhani shetani hawezi kumdanganya Mzungu, Je Mzungu ana akili kuliko Malaika ambao waliodanganywa na shetani kule Mbinguni? Shetani huwatumia wanaodhaniwa wana akili ili kuwavuta wengi kwake. Wakati wa Gharika dunia yote waliangamia wakiwamo na Wazungu, wanaodhaniwa leo wana akili kumzidi shetani.

Nguvu za shetani zimewaletea wanadamu magonjwa mengi. Mikutano mingi ya Injili inaandaliwa kwa nguvu hizi. Mahali Fulani ambao shetani na watu wake watafanya mkutano, nguvu hizi hutangulia na kumwaga magonjwa ya kila aina halafu huwasogeza wagonjwa hao katika mkutano wake. Ndipo kupitia maombi ya kishetani huwaondolea magonjwa hayo nao hujisikia wamepona. Mikutano mingi inayofanyika ni kwa uwezo wake. Shetani ana watu wake ambao wamejitoa kufanya kazi hiyo kwa kutumia Roho mchafu. Mtu wa Mungu hatashiriki katika udanganyifu huo.

"Maana watu hao ni mitume wa uongo watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa Mitume wa Kristo. Wala si ajabu maana shetani mwenyewe hujigeuza awe

mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao" *(2Wakorintho 11:13-15)*

Watu wakiwa chini ya uwezo wa roho wachafu watatenda miujiza. Watafanya watu wawe wagonjwa kwa kuwadumaza kwa uchawi halafu watawaondolea uchawi na nguvu hizo na kuwaongoza watu wengi kusema wameponywa kimiujiza jambo hili shetani amelifanya tena na tena" *(2SM 53)*

Namna ambayo kwayo Kristo alitenda miujiza ilikuwa kulihubiri neno na kuwapa ahueni wagonjwa wenye kutaabika kwa kufanya miujiza ya uponyaji. Lakini nimeelekezwa kuwa hatuwezi sasa kutenda kazi kwa namna hii kwa maana shetani atatumia uwezo wake kutenda miujiza. Watumishi wa Mungu hawawezi kufanya kazi ya Mungu kwa njia ya miujiza kwa sababu matendo bandia ya uponyaji yakidaiwa kuwa yametoka Mbinguni yatafanywa *(2SM54)*. Watu wa Mungu hawatakuwa salama kwa njia ya kutenda miujiza maana shetani ataigiza watakavyofanya. *(9T16)*

Eliya alipokuwa amesimama mbele za Bwana tazama Bwana akapita, upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima ukaivunja vunja miamba lakini Bwana hakuwemo katika upepo ule. Na baada ya upepo tetemeko la nchi, lakini BWANA hakuwepo katika tetemeko lile. Na baada ya tetemeko kukawa moto lakini Bwana hakuwepo katika moto ule. Na baada ya moto ndipo ikatokea sauti ya Mungu. Sauti ndogo naya utulivu *(1Wafalme 19:11-12)* Hivi ndivyo Mungu anavyojifunua kwa watu wake. Tofauti kubwa kama nini kwa wanaodaiwa kushukiwa uwezo huo leo! Kuna kelele za fujo zinazoambatana na vurugu za kurusha mikono na maneno ya kufoka yasiyostahili mbele za Mungu. Wengi hufanya haya wakiwa wamesimama tofauti na agizo la Mungu. Wengi pia wamekataa sehemu ya biblia hata baadhi ya amri za Mungu huku wakijitangaza kuwa wameokoka kinyume na biblia *(Mhubiri 7:20)* Hizo ndizo roho za Mashetani.*"Haya ikiwa kanisa lote limekusanyika pamoja na wote wanene kwa lugha kisha ikawa wameingia wajinga au wasioamini, je hawatasema kuwa mna wazimu? (1Wakorintho 14:23) Mbona Mungu amekataa wanawake kunena na bado wanafanya hivyo? (1 Wakorintho14:34) katika Torati kuna kazi ambayo wanawake waliopita walitoa mfano kwa wanawake wa kizazi hiki. Mungu atamhukumu kila mmoja kwa wajibu aliopewa na hakufanya.*

Maumbo ya watu waliokufa yataonekana kwa njia ya udanganyifu mkuu wa shetani; nao wataungana nayeye aupendaye uongo na kuufanya. Nina waonya watu wetu kuwa miongoni mwetu wengine watajitenga na imani *(1Timotheo 4:1)* wakisikiliza Roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani. Na kupitia kwao ukweli utatukanwa, *(Mathayo 24:24)* Wachungaji madaktari, wanasheria ambao wameruhusu uongo huu

kutawala mawazo yao ya utambuzi watageuka na kuwa wadanganyifu wao wenyewe wakiungana na waliowadanganya. Ulevi wa kiroho utawamiliki *(UL317*)

Shetani anajua kuwa wote wanaofuata imani hiyo wapo chini ya udanganyifu wake Mungu anapotuma shuhuda hizi anakutaka ubadilike; utoke katika gereza la shetani ujitenge na uchafu ili uandaliwe kwa kazi takatifu Mungu anakutaka uelewe kuwa kupitia kunena lugha isiyojulikana Mungu atakuhukumia adhabu. Kwa maana kila neno lisilo maana watakalolinena wanadamu watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu *(Mathayo12:36)*

Mungu anayataka madhehebu yafanye mabadiliko. Uzima au mauti vi juu yenu. wengi watadharau shuhuda hizi na kuendelea kubaki dhambini. Mungu atawahukumu kulingana na vile walivyopuuza maana walikubali kumgeukia Yesu lakini wakazidi kudumu dhambini wakizungumza lugha ya shetani. Tabia zao zinazidi kuchafuka kila siku huku shetani akiwatwisha mizigo inayowalemea. Kundi hili litalia na kuomboleza wakati moto utakapo kula miili yao wakati wa kiama, kwa maana wanakiri ya kwamba wanamjua Mungu bali kwa matendo yao wanamkana, ni wenye machukizo, waasi, wala kwa kila tendo jema hawafai. *(Tito 1:16)*

SURA YA SABA

# UREMBO WA KWELI

Dada zetu wanajichubua ngozi yao ya nje ili kubaki na majeraha mwilini wanayoyaita urembo. Akina dada hawa wamedharau kusudi takatifu la Mungu aliyewapatia ngozi ngumu nyeusi ya kiafrika kwa kusudi maalum. Ee binadamu wewe u nani umjibuye Mungu? Je kitu kilichoumbwa kimwambie yeye aliyekiumba kwani kuniumba hivi? *(Warumi 9:20)*

Dada zetu wamedharau nywele ndefu walizopewa na Mungu wakajivika mizigo mizito ya manyoya ya wanyama ambao wengine ni najisi waliokufa katika vichwa vyao wanayoyaita nywele. Wengi wameumwa kwa ajili ya mizigo hii wanayojitwisha ili mradi wafanane na Wazungu ambao walishaharibika kwa kiasi kikubwa. kwa kufanya hivyo wanajikana wenyewe utu wao, uafrika wao na Mungu ambaye ndiye chanzo cha uumbaji wao. Au mfinyanzi, je! hana amri juu ya udongo kwa fungu moja la udongo kuumba chombo kimoja kiwe cha heshima na kimoja kiwe hakina heshima? *(Warumi 9:21)*.

Dada zetu hawataishi miaka mingi kwa sababu ya uchafu wanaouita maendeleo ya urembo. Hakuna kiwanda cha kutengeneza uzuri katika mwili ambao umeumbwa na Mungu. Mungu anatutaka tubaki jinsi tulivyoumbwa na atukute hivyo tukiwa safi katika miili na roho zetu.

Dawa inayopakwa kichwani ili kuharibu miili ya asili ina harufu yake kutokana na kule ilikotengenezwa na jinsi ilivyobuniwa. Harufu hiyo siyo hewa safi nayo yaweza kusababisha magonjwa. Dada zetu hawaelewi sawasawa vitu vinavyotumika kutengenezea sumu hizo. Wengi hawaelewi asili ya uchovu wa miili yao. Maandiko yalionya juu ya ubaya wa dhambi hiyo inayopendwa na wengi. Shetani anafanya kazi bega kwa bega katika saluni fulani ambazo wengi hawaelewi kusudi la kuanzishwa kwake.

Dada zetu wanajikondesha kupunguza uzito ili wafanane na umbo la senene wakati wao ni binadamu. Tunakwenda kuingia katika hatari ambapo utu na uasili wetu wote utapotea. Kupitia mtego huu wengi wamenaswa na shetani hasa wale wanaojidanganya kuwa wanamjua Yesu. Mungu ni Mtakatifu na Mkamilifu, kamwe Mungu hatakaa katika dhehebu ambalo muumini wake ananuka uvundo huo ambao binadamu anauita Urembo. Shetani hushangilia anapoona wanawake wakiingia katika ibada na uchafu huo.Tumejifunza vizuri kuhusu usafi katika sura iliyopita.Uvaaji wa nywele bandia huambatana na uchafu wa kutoziosha kitu ambacho ni chukizo kwa Mungu.

Wengine hawaelewi kuwa mwaka 1951 wakati ndugu Eric Morley na Mke wake kwa mara ya kwanza walipobuni mashindano ya mrembo wa Dunia hawakuwa na wazo la Mwafrika kichwani wala mambo haya hayakukusudiwa kwa ajili ya mwafrika. Kuna matendo potofu ambayo watu wa Mungu hawapaswi kuiga.

Wakati dada Mary Quant aliyebuni vazi la Mini-skirt alipohojiwa mwaka 1964 katika mahojiano hayo alisema "kusudi la kuibuni nguo hii ni kuchochea ngono ifanyike zaidi hata wakati wa mchana" Mwafrika hakuhitaji kuonywa juu ya jambo hili maana yeye hata bila kusoma alilijua hili tangu milele zote. Hatukuwahi hata kuota ndoto kuwa siku moja na sisi lingetukuta licha ya utajiri wa maadili tuliokuwa nayo ambao leo yanaitwa ushamba.

Mkristo wa kweli ataiga tabia ya Kristo. Maisha ya kutoiga mambo ya kubuni na ya ovyo huwa na maana sana kwa watoto na kuchunguza viumbe vya Mungu hupanua mawazo zaidi yanayo jenga Roho.Dhambi inapozoeleka hatimaye hisia ya ubaya hupotea moyoni na watu kuzama maovuni.Unaweza kuchukia ukweli huu baada ya kusoma lakini kamwe halitakuwa suluhisho la kutokuangamia usipotubu na kuacha.

Dada zetu wameacha mshono ule mzuri wa heshima katika mavazi yao. wengi wanatembea kwa taabu kulingana na mavazi yao waliyovaa. Mungu alitoa agizo suruali yeyote isivaliwe na Mwanamke Mcha Mungu. Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanaume wala mwanaume asivae mavazi yampasayo mwanamke kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa BWANA Mungu wako. *(Kumbukumbu la Torati.22:5)*

Mwonekano wa nje ni ishara kuonyesha jinsi moyo wa mtu ulivyo.Mungu ataka sana mvao wetu uwe safi na wenye kutia afya tena mzuri unaolifanya vazi na mshono wake mwilini kuwa elezo la hali ya mtu alivyo. Mwanamke mwenye adabu atavaa kwa adabu. Hebu dada zetu wavae pasipo urembo, kama wengi wafanyavyo wakiwa na mavazi mazuri ya vitambaa vidumuvyo.

Tena mavazi yasiwe jambo kubwa mawazoni. yapasa wajivike nguo za adabu kusetiri aibu ya uchi na kwa kiasi. wapeni walimwengu kielelezo cha nguvu cha kujipamba kwa neema ya Mungu.*(CG413-415)*

Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi. Si kwa kusuka nywele wala kwa Dhahabu na Lulu wala kwa Nguo za thamani bali kwa Matendo mema kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu *(1Timotheo 2:9 – 10)*

Msijisumbue wakati wote kwa kujaribu kuigiza namna zote za mavazi zisizofaa. Vaa vizuri lakini usijionyeshe ama kwa kuvaa maridadi au kwa kuvaa vibaya kwa uzembe. Tenda

kana kwamba jicho la Mungu linakutazama. Dhahabu au Lulu na Nguo za thamani kubwa ni vyenye thamani ndogo sana vikilinganishwa na Upole na Uzuri wa Kristo katika Moyo wako. Urembo mzuri nikuwa na Yesu Kristo ndani ya Moyo.

Mavazi mepesi yasiyo na mapambo mengi yatakuwa sifa njema kwa dada zangu. Vijana hamwezi kuiacha nuru iangaze kwa wengine kuliko kwa njia hii ya mavazi yasiyo na mapambo mengi na mwenendo mzuri. Mwaweza kuwaonyesha wote kuwa mwayathamini maisha haya pamoja na yale ya uzima wa milele *(3T376)*

Heri mtu yule amchaye BWANA apendezwaye sana na maagizo yake *(Zaburi 112:1)* Upendeleo hudanganya na uzuri ni ubatili bali mwanamke amchaye Bwana ndiye atakayesifiwa *(Mithali31:30)* Mavazi yasiyo ya kujipamba pamoja na adabu nzuri vitafanya Mungu kumzungushia Msichana usetiri mtakatifu ambao kwake utakuwa ngao ya kumkinga na maelfu ya hatari. *(CG417)*

Vijana wapendwa nia mlionayo ya kuvaa kama ulivyo mtindo wa siku hizi na kuvaa vazi jembamba na mapambo ya dhahabu na vitu vya kuigiza kwa urembo haitashuhudia kwa wengine dini yenu wala neno la kweli mnalolikiri. Watu wenye akili watahesabu kujipamba kwenu kwa nje kama nia mliyo nayo na mioyo ya kiburi. *(CG421)*

Vaeni kama iwapasavyo watu wa Mungu pasipo mapambo jitengeneze kama wanawake wengine na wasafiri wa mbinguni (maana sisi wenyeji wetu uko mbinguni. *(Wafilipi 3:20)* Mavazi yasiyo na mapambo mengi yatamfanya mwanamke mwenye akili kuonekana bora sana. Mungu ataleta hukumuni kila kazi na kila tendo likiwa jema au baya. *(Muhubiri 12:13-14)*

Wengine wataonekana wamepungua katika mizani ya Mbinguni kwa sababu ya urembo. Kuna adhabu kali inakuja kwa wale waliothamini mambo ya kuiga. Dunia hii itajaa uvundo na harufu mbaya wakati wa mapigo saba ambayo yataanza punde duniani. Wanawali wazuri na wavulana waliothamini Dunia kuliko Mungu ni katika siku hiyo watakapozimia kwa kukosa msaada. Muda mwingi unaotumika kujipamba ungetumika Kufanya mambo matakatifu

pamoja na kupeleka ujumbe wa onyo ili Dunia ijue kile kinachokuja. Nabii Isaya alionyeshwa haya:, Siku hiyo Bwana atawaondolea uzuri wa Njuga zao na Kaya zao, na Pete za masikio na Vikuku na taji zao na Dusumali na Mafurungu na Vitambi na Vibweta vya na Matalasimu na Pete za azama na mavazi ya Sikukuu na Debwani na shari na Vifuko na vioo vidogo na Kitani nzuri na Kilemba na Utaji.

Hata itakuwa badala ya manukato mazuri utakuwa Uvundo na badala ya mishipi Kamba, na badala ya nywele zilizosukwa vizuri Upaa, na badala ya kisibau mavazi ya

kigunia na kutia alama mwilini kwa moto badala ya uzuri. *(Isaya 3:18-24)* Wengi hutumia fedha nyingi kwa mapicha kuwapa rafiki zao ambazo hupigwa kupita kiasi na kuwa aina ya kuabudu sanamu. Inampendeza Mungu kiasi gani ikiwa fedha hizi zingeangaliwa kwa kazi takatifu.

## TUFUATE MILA NA DESTURI AU NENO LA MUNGU?

Mila na desturi za kisasa hushindana na mambo yanayohusika na uzima. Anasa zinazokuza desturi hizi za kisasa huzidi kuzipunguza nguvu za ubongo na za mwili na kuleta taabu kwa watu wa dunia. Licha ya uhalifu, ulevi na maradhi lakini pia mavazi yaliyopo sasa ni yale yenye mwelekeo wa Sodoma. Matengenezo ya kweli ya kiroho yanategemea sana misingi na kanuni za asili. Kama misingi ikiharibiwa mwenye haki atafanya nini? *(Zaburi11:3)* Katika kawaida za dini zilizofuatana na waisraeli wa zamani ambazo zilikuwa mfano wa injili ilikuwa haramu kuleta kafara yenye kilema madhabahuni pa Mungu *(Mambo ya Walawi 21:20)* Vivyo hivyo dhabihu ya Kristo ni lazima iwe safi bila mawaa. Na suala la mavazi Mungu huliangalia. Wale wamwendeao Mungu kwa heshima mavazi yao hayatakuwa na Kasoro wala mvuto mbaya muda wote waishipo duniani.

Matokeo mabaya sana yanayoshangaza dunia hii ni yale ya kupotewa na uwezo wa kujitawala nafsi. Tamaa za miili yetu zisipotawaliwa kwa dhati zitaleta uharibifu na kifo. Ni lazima dhamiri ijulishwe matakwa ya Mungu na kuepukana na kila aina ya mavazi na Urembo usiofaa. Hatuwezi kuyaacha mazoea haya mabaya isipokuwa tumeichukia dhambi na kuiacha kwa msaada wa Mungu.

Maisha ya Mwokozi wakati wa ujana wake ni mfano mkubwa kwa vijana wa siku hizi, pia ni mfano kwa wazazi ambao wangeelimisha watoto wao. Yesu ndiye kielelezo chetu. Hakujihusisha na michezo ambayo ingeharibu utukufu wala hakuvaa mavazi ya aibu na anasa kama ilivyo kwa vijana na wazee wa kizazi hiki. Bali aliishi kama mmoja wetu akishiriki maisha ya nyumbani . Katika nyumba ya kimasikini alimolelewa alishiriki mambo yote yanayowapata wanadamu, akizitenda kazi zote kwa adabu na heshima kama kijana ili atuachie kielelezo. Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo akimpendeza Mungu na wanadamu *(Luka 2:52)*

Wakati wetu hapa duniani ni mfupi, maisha yetu yanapita hima, muda mfupi tutaingia Mbinguni tukishinda, tunapaswa kuitunza miili ili Roho mtakatifu akae nasi. Mavazi yetu yanaweza kuzuia roho mtakatifu asikae nasi. Mungu angependa kuona wanadamu

walio kamili katika mavazi kama walivyo kamili katika tabia. Kwa kila pigo la moyo damu ingepitishwa upesi kwa sehemu zote za mwili. Mzunguko huu wa damu usizuiwe na mavazi yanayobana sana wala Vikuku na Bangili za urembo au mavazi yasiyofunika vizuri viungo vyote vya mwili.

Kitu chochote kinachozuia safari ya damu hurudisha damu kwenye viungo vinavyohusika na uhai na kufanya mavilio ya damu na kusababisha kuumwa na kichwa, kukohoa kupigapiga kwa moyo au kuleta maumivu ya tumbo na kutokuweza kula chakula. Mungu aliagiza miili yetu isiharibiwe na mavazi wala mapambo na mavazi yenye mwelekeo mbaya yatakayoharibu kanuni za heshima na afya ya mwili.

Mungu ataka mwili na roho vitunzwe kwa uangalifu ili kutimiza masharti ya utakatifu "Basi wapenzi wangu kwa kuwa tuna ahadi hizo na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu *(2Wakorintho 7:1)*.Miili yetu ni mali ya Kristo naye ameinunua kwa thamani nasi hatuna ruhusa kuitendea kama tupendavyo. Mtu anayempenda Kristo hataharibu mwili wake kwa kuweka vitu katika mwili ambavyo Yesu amevikataa.

Alama ya dini ya Kikristo siyo kitu cha nje kama vile kuvaa sanamu ya msalaba na mikufu au taji na kuionyesha kwa nje bali ni utii wa neno la Mungu takatifu litakalotuwezesha kusimama bila mawaa mbele za Mungu siku ya hukumu.Yesu alifundisha watu kuwa na kiasi kwa kila jambo alifundisha juu ya hatari za kuungana na ulimwengu katika mafundisho machafu na kuwa na kiasi kwa mambo yote na kwamba muda mwingi usitumike kuyasumbukia mavazi kuliko kuutafuta unyenyekevu ambao ni wa thamani kuliko mavazi ya kitambaa.

Na mavazi ya nini kuyasumbukia? *(Mathayo 6:28)* basi kila asikiaye maneno hayo na kuyafanya atafananishwa na mtu mwenye akili aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba. Mvua ikanyesha mafuriko yakaja, Pepo zikavuma zikaipiga Nyumba ile isianguke maana imewekwa juu ya mwamba.

Kama walimwengu wakianzisha namna ya mavazi ya adabu ya kufaa na yenye kutia afya yanayopatana na Biblia haitadhuru uhusiano wetu na Mungu. Wakristo wamwige Kristo kwa mvao wao wakinyenyekea bila kujali sifa wala lawama. Vaa safi bila kujionyesha umaridadi wala usivae vibaya maana ndivyo walivyofanya wakristo na mitume wa zamani.

## MVUTO MBAYA

Mavazi ya kujionyesha ya bei kubwa mara nyingi huzidisha tamaa ya mwili moyoni mwa mvaaji na kuamsha tamaa moyoni mwa mtazamaji. Mungu aona kuwa uharibifu wa tabia mara nyingi hutanguliwa na kuendekeza kiburi na umaridadi usio na maana. Huona kuwa Mavazi ya bei kubwa huzimisha tamaa ya kutenda mema.*(4T645)* Kama hujioni upo hatarini katika mavazi hayo na ikiwa huombi kwa Mungu msaada na nguvu ya kuyapinga majaribu bila shaka utapotea. Kutojali wajibu wako kutaonyeshwa katika kitabu cha Mbinguni nawe utaonekana umepungua siku ile ya kupimwa. wapo wengi ambao walimsahau Yesu wakavuka mstari huu wa mavazi wakajipendelea, wakasifiwa isivyostahili na kutukuzwa isivyostahili mpaka wameharibika hata hawafai tena mbele za Mungu.

Wengi huvaa kama walimwengu ili kuwa na mvuto kwa wale wasioamini. kufanya hivyo ni kosa baya. Wakipenda kuwa na mvuto wa kweli na waonyeshe imani yao kwa matendo ya haki maishani. Ndipo mvuto mtakatifu utaenezwa kwa wote wawazungukao *(4T633,635)*

## AGIZO LA BIBLIA

Wanawake wengi watasimama hukumuni katika hukumu ya mwisho kwa kudharau utakatifu katika mavazi yao. Mungu alimuumba mwanaume kwa utukufu wa Mungu akamfanya mwanamke ili amsaidie mwanamume. Mwanaume ni utukufu wa Mungu na mwanamke ni utukufu wa mwanaume. Kama mwezi unavyong'aa kwa msaada wa jua ndivyo utukufu wa ubavu unavyong'aa kwa msaada wa kichwa maana kila kichwa cha mwanaume ni Kristo na kila kichwa cha mwanamke ni Mwanaume. Kuna pambo la utukufu ambalo akina dada leo wamelikanyaga. Agizo hilo litawafanya wengi wakwame mbinguni kwa sababu ya kujiaibisha. Ni agizo takatifu mwanamke ambaye ni utukufu wa mwanamume afunike kichwa chake popote. Agizo hili ni jema takatifu lisilokosewa. Hivyo imewapasa wanawake wamchao Bwana kutoacha vichwa vyao wazi maana kufanya hivyo ni makosa. Mungu ametoa agizo hili ili kudumisha uwepo wake na kanuni yake takatifu.

Fundisho hili limedharauliwa na wengi wanaojidai kumjua Yesu huku wanawake wanaodhaniwa kuwa wapagani wakiliheshimu ndiyo maana Yesu alipoona kwa darubini ya kinabii akasema kuwa wa kwanza watakuwa wa mwisho na wa mwisho watakuwa wa kwanza. Ni agizo la Mbinguni mwanamke asiache kichwa chake wazi. *(1Wakorintho 11:15)* Kwa maana kweli haimpasi mwanaume kufunika kichwa kwa sababu yeye ni mfano wa Utukufu wa Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanaume maana mwanamume hakutoka katika mwanamke bali mwanamke katika mwanamume wala

mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke bali mwanamke kwa ajili ya mwanamume. Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani kwa ajili ya Malaika. *(1Wakorintho 11:7-10)*.

Mkijua wajibu wenu kwa Mungu mtaona moyoni mwenu haja ya uaminifu katika kuomba na uaminifu ili kujiandaa kwa uhamisho ambapo punde tutaihama dunia hii. Mtamuomba Mungu awafunulie siri za shetani ili kuwaepusha katika majaribu. *Ikiwa wewe ni Mkristo wa kweli utayatii maonyo ya Mungu na kufanana na Yesu kwa mavazi. Moyo wako utapenda zaidi kuhuzunikia giza la shetani lililopo badala ya kujifurahisha kwa anasa na kiburi cha bure cha mavazi.*

Elimu ya kweli ni uwezo wa kutumia akili ili kupata matokeo mema yenye faida. Mbona basi dini tunaifurahia kidogo sana huku mambo ya ulimwengu yakiwa na nguvu Ubongoni, Mifupani na kwenye Misuri? Tumejishughulisha katika mambo ya kidunia mpaka tumesahau kuangalia vitu vya milele?

Dada na Kaka zangu, kuna siku ya kuhukumiwa juu ya jambo hili. Kupimwa katika mizani na kuonekana kuwa umepungua siku hiyo litakuwa jambo la kutisha kwa kila mtu mwenye mwili. Litaonekana tena wakati dunia yote itakapo kuwa kimya hukumuni, Je jina lako litapatikana katika kitabu cha Mungu ?

## SHETANI KATIKA PETE

Kati ya vitu ambavyo wanadamu wamepewa na shetani ni mapambo ambayo hawakuzaliwa nayo. kwa kuvaa,katika mwili aidha kwa kujua au kutokujua shetani amepata mafanikio na kuteka wengi. Watu tusipoamka na kukumbuka kuwa duniani kuna shetani hakika ni wachache watakaookolewa. Leo mapambo yamechukua mahali pa utakatifu na tayari yameanza kuabudiwa. Pete zimetengenezwa kwa madini mbalimbali kwa ajili ya kuvaa. Wengi huvaa katika vidole vya mikono, Miguuni na masikioni. Mwanzoni Pete ilitumika kama alama ya mamlaka. Wafalme wengi walizitumia kama muhuri wao. Baadaye Pete zikaanza kutumika kwa makusudi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mapambo. Wakati Papa anapochaguliwa hukabidhiwa Pete iliyo na sanamu ya Mt.Petro akiwa katika mashua ya uvuvi. Anapokufa Pete ile huharibiwa na nyingine hutengenezwa kwa ajili ya Papa mpya anayechaguliwa.

Polepole pete ilianza kutumika kama ishara ya muungano wa Ndoa. Pete ya Uchumba na ya Ndoa kwa mara ya kwanza ilivaliwa na Warumi *( World Book volume 16 uk 342 )* Kuna pete zilizotumika kama kinga ya majini na ugonjwa *(Every Man's Encyloparedia uk 355)* Wengi leo wamezaliwa wakiikuta Pete inavaliwa na wakaiga bila kujua historia yake ilikotoka na maana yake.

Hakuna andiko takatifu linaloruhusu uvaaji wa Pete, wale wanaovaa Pete huvaa kwa ajili ya urembo lakini pia pete ni kitambulisho kujieleza mtu alivyo. Pete ni lugha ya fumbo kwa wengi. Kuna Pete zinazoonyesha mvaaji ni mchawi. Mawasiliano wakati mwingine hufanywa kwa njia ya Pete. Mashoga pia wana Pete zao zinazowatambulisha jinsi walivyo. Pete au Heleni inayovaliwa na wanaume sikio moja ni lugha ya fumbo na ina maana yake. Kuna wanaume wanaovaa pete au Heleni masikio yote lakini wakiwa wamesuka nywele. Wengine wanafanya hivyo wanaiga tu bila kujua.

Wapo wanawake wanaovaa Pete mguuni wakiashiria maana halisi ya vile walivyo, uvaaji wa Pete mwingine humaanisha kuwa mhusika anashiriki tendo la ngono kinyume na maumbile. Waabudu shetani wana aina zao za Pete maalum zinazowatambulisha. Agizo la kuvaa pete halipatikani katika Biblia ila mzizi wake upo katika historia ya kale ya kipagani ambao uliingilia Rumi na kuingizwa katika madhehebu kama sehemu ya mwongozo wa dini.

Popote Pete inapopovaliwa pana maana kubwa kwa shetani. Pambo ambalo Mungu hajaruhusu lina maana kubwa kwa shetani; Mungu hajalegeza dhambi hii kwa sababu wengi wanaitenda

Zipo Pete za Ndoa, Uchumba, kutafuta utajiri, Vyeo na kujilinda na maadui. Pete zingine ni kwa ajili ya viongozi wa dini. Wengi wamemwakilisha shetani huku wakiwalazimisha waumini wazibusu pete kama ishara ya Baraka.Dunia hii inahitaji maonyo kwa sababu msimamo wa madhehebu mengi leo haufai. Maonyo yasipotolewa watu wa Mungu watapotea.

Unaweza kuchukia baada ya kusoma ukweli huu lakini kamwe uongo hautageuka kuwa ukweli kwa sababu wengi wamekubali. Maandiko yanaonya juu ya uvaaji wa mapambo kuwa, Kujipamba kwenu kusiwe ni kujipamba kwa nje yaani kusuka nywele na kujitia dhahabu na kuvalia mavazi bali kuwe utu wa moyoni usioonekana katika mapambo yasiyoharibika yaani roho ya upole na utulivu iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. Maana ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa amani waliomtumaini Mungu na kuwatii waume zao .*(1 Petro 3: 3- 5)* Wanaofundisha kuwa Mungu anaangalia moyo watapoteza wengi maana aonavyo mtu nafsini mwake ndivyo alivyo *( Mithali 23:7)* Hakuna kitu kinachotendwa nje ya mwili ambacho hakitoki moyoni. Kumbuka moyo huwa mdanganyifu kuliko vyote *(Yeremia 17:9) soma pia katika 1 Timotheo 2:9 -10)*

Yakobo aliwaambia watu wake waondoe miungu migeni wajisafishe na kubadili nguo ili waende Betheli kumfanyia Mungu madhabahu.Nao wakampa Yakobo miungu yote na Pete za masikioni naye Yakobo akazificha chini ya mwaloni ulioko shekemu.*(Mwanzo 35:4- 5)*

Mahali pa kukutana na Mungu paliitwa shekemu.Shekemu yetu leo ni mahali pa ibada. je ni mara ngapi tumeingia shekemu na mapambo ambayo ni ibada kwa shetani? Wale wanaovaa Pete ya ndoa kama ishara ya kuoa au kuolewa kumbukeni kuwa katika arusi ya Kana ambayo Yesu alihudhuria hawakuvalishwa Pete *(Yohana 2: 1- 5)*

*Historia Fupi ya Pete.*

Mwandishi Edivard Westermark analeza kuwa Pete za harusi zilitumika na wazee wa wa kale wa Kihindi na baadaye familia tajiri za Warumi zikaiga mila hii katika sherehe za harusi ambapo Bwana harusi huvisha pete katika kidole cha kati cha bibi harusi wakati wa Uchumba na Ndoa. Pete zilizotumika zilitengenezwa kwa madini ya chuma. Kuwepo kwa Pete hizi kulianza zamani na umaarufu wake ulidhihirisha kutwaliwa kwa mwanamke anayeolewa wakati wa himaya ya Kirumi. Pete ya kirumi ilitolewa kama ahadi. Kutolewa kwa Pete ya Ndoa kulitokana na tabia ya utamaduni huu ambao mwishowe ulipata baraka na kanisa la Rumi. *(Every man's Encylopeadia ukurasa 355)*

Mwandishi mwingine Bernard Mustein anaelezea kuwa Wakristo wa kwanza walifuatisha na kuigiza mila za kirumi. Wakati wa sherehe za Ndoa na pete hizo shamrashamra za kistaarabu ziliruhusiwa. Lakini ulevi na vinywaji na michezo ya utamaduni kama ambavyo ilikuwa ikifanywa na Wagiriki na Warumi haikuruhusiwa.Wakristo wa kwanza walifuatisha na kuigiza jinsi harusi za wapagani waliowazunguka zilivyofungwa. (*Mustein 12 ibid*.)

Pete ilikuwa ni ibada ya kumuabudu mwanadamu. Walokole wa zamani walijitenga na sherehe za Ndoa kwa kile kilichoitwa ishara ya upapa na matumizi ya Pete hayakuruhusiwa kabisa. *(19 Good Sell Uk 269)*

Thomas Cart Wright kiongozi wa chama cha Kilokole katika mswaada wake uliopelekwa Bungeni aliita uvaaji wa Pete ni makufuru ya upapa, wakati walipokuwa wakiinua Pete ya Ndoa kuimarisha na kuienzi. Wanapovaa wanakufuru jina la Utatu Mtakatifu kwa mujibu wa desturi za upapa humtengenezea mke sanamu akisema." *Kwa pete hii naunganishwa nawe na kwa mwili wangu nakuabudu"*Hatuhitaji kuvaa ishara maana tu waaminifu kwa viapo vya Ndoa zetu na uaminifu huu hauwezi kuthibitishwa na uvaaji wa Pete za Ndoa. Kamwe Isitumike hata senti moja kununua Pete ya aina yoyote ili kuthibitisha kuwa tumeoa au tumeolewa *( TM180,181)*

Pete iliyovishwa katika kidole chako yaweza kuwa ya kawaida isiyo na madoido lakini haifai na uvaaji wake huleta mvuto na mtazamo potofu kwa wengine. *(4T460)* Ukweli unaoukiri katika dini yako hautadhihirisha kwa kujipamba na mitindo na kuvaa Pete. *(MYP348)* Wengi wanaojidai kuwa ni wana wa Mungu hawaoni ubaya wowote kuungana na desturi za kidunia katika kuvaa Pete na vito mbalimbali vya thamani.Wale

wasiovaa vitu hivyo huonekana watu wasio na upeo kifikra na washika dini kupita kiasi lakini Mungu mwenyewe ameona atupatie maelekezo haya yenye hekima isiyo na kipimo.

Wale wanohusudu mapambo yaliyokatazwa na Mungu wanahusudu kiburi na majivuno katika mioyo yao. *(ITT599)* Mungu alionya Taifa la Israeli lisiige mila na desturi tabia za makafiri ili ili liendelee kuwa takatifu lililotengwa ulimwenguni. Onyo hilo litazidi kuwa hai kadri Mungu atakavyodumu. Maagizo yake matakatifu hayabadiliki. *(Malaki 3:6 Zaburi 12:6 Mithali 30:5-6)*

Maridhiano na dunia ni dhambi inayodhoofisha Roho na kuchafua huduma yetu. Ni upuuzi mtupu kutoa maonyo kwa watu huku wewe mwenyewe huyafuati maonyo hayo katika maisha ya kila siku. *(EV172)*

---

Fedha inayotumika kununulia vito vya thamani vya kujipamba vingalitumika kwa kununua mahitaji ya wajane au yatima ambao vilio vyao vinapanda mbinguni kwa kukosa mahitaji muhimu. Wale Wanaojidai ni Wakristo watasema nini siku ya hukumu? Walitumainia fedha kwa vitu vilivyokatazwa na Mungu. *(WM216)*

Mungu ametoa onyo hili zito ili kukuandaa. Maneno haya ni rahisi na mepesi kueleweka. Mungu hamlazimishi mtu yeyote amtumikie. Ikiwa Mungu ni Baba yako basi anakutaka ufanye mabadiliko ya Mavazi na mapambo maana umepimwa nawe unaonekana umepungua. Na ikiwa umemchagua shetani awe baba yako mpendwa endelea kujipamba kadri uwezavyo, ujipambe bila mipaka huku ukingojea kuja kuchomwa Moto katika siku ile kuu hasira za Mungu zitakapomwagwa kwako bila huruma. Mungu hana haja na yeyote mwenye Roho ya kusitasita.

---

SURA YA NANE

# MADHARA YA NYAMA

Uchu wa chakula unaomtawala mtu utapelekea maangamizi ya maelfu wakati ambapo kama wangalishinda katika jambo hili wangalipata nguvu za kiroho kwa jaribu lingine la shetani. Wale ambao ni watumwa wa uchu wa chakula watashindwa kujenga tabia kamilifu ya Kristo. Kwa kadri tunavyokaribia mwisho wa wakati ndivyo majaribu ya shetani ya uchu wa chakula yatakavyokuwa na nguvu zaidi na magumu zaidi kuyashinda. *(CD59).*

Kanuni inayowatawala watu wa MUNGU ingekuwa hii "Basi mlapo au mnywapo au mtendapo neno lolote fanyeni yote kwa utukufu wa MUNGU"(*1Wakorintho10:31)* Kwa kujizoesha kuwa na kiasi katika kula,kunywa,kuvaa, kufanya kazi na katika mambo yote tunaweza kujifanyia mambo ambayo tabibu hawezi kutufanyia.*(ML142).* Kutokuwa na kiasi ndiyo msingi wa maovu yote katika Ulimwengu *(Te.165)*

Hamjui yakuwa ninyi mmekuwa hekalu la MUNGU na ya kuwa Roho mtakatifu anakaa ndani yenu?, kama mtu akiliharibu hekalu la MUNGU, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la MUNGU ni takatifu ambalo ndilo ninyi *(1Wakorintho3:16,17).*

Ni jambo rahisi kupoteza afya, lakini ni jambo gumu kuipata tena. Hatuwezi kuidumaza na kuilemaza akili au mwili wetu kwa kuutumikisha vibaya sehemu yake. *(ML 142).* Au hamjui ya kuwa miili yenu ni hekalu la Roho mtakatifu aliye ndani yenu mliyepewa na MUNGU?. Wala ninyi si mali yenu wenyewe maana mlinunuliwa kwa thamani. Basi sasa mtukuzeni Mungu katika miili yenu *(1Wakorintho. 6:19-20).*

Maneno haya "mlinunuliwa kwa thamani" yangewekwa katika kumbi za kumbukumbu zetu ili daima tupate kutambua haki aliyonayo Mungu juu ya talanta zetu, mali, mvuto, na nafsi zetu wenyewe. Yatupasa kujifunza namna ya kuitunza zawadi hii ya Mungu kwa akili zetu roho zetu na miili yetu na kwamba sisi kama mali yake Kristo iliyonunuliwa tumpe huduma yetu iliyojaa afya na harufu nzuri *(RC 138).* Wale wanaotaka kuwa watendakazi pamoja na Mungu wajitahidi kupata ukamilifu wa kila kiungo cha mwili na akili *(3Yohana 1:2, COL 330.)*

## HAUKUWA MPANGO WA MUNGU

Mungu aliwapatia wazazi wetu wa kwanza chakula alichokusudia wakile *(Mwanzo11:29).* Ilikuwa ni kinyume na mpango wake kuua kiumbe chochote, naye Mungu hakupanga pawepo na mauti katika Edeni. Mungu hakumruhusu mwanadamu kula nyama mpaka baada ya gharika kwa sababu kila kitu ambacho mwanadamu angeweza kuponea kilikuwa kimeharibiwa. Hata hivyo wanyama walitolewa kwa masharti *(Mambo ya*

*Walawi11:1-47).*

Mungu akampa Nuhu ruhusa kula wanyama kwa ajili ya riziki, lakini nyama haikuwa chakula chenye kutia afya *(CD373).* Katika kuteua chakula cha wanadamu Edeni Mungu alionyesha kile kilichokuwa bora kuliko vingine vyote, katika kuwateua waisraeli alifundisha somo lile lile. Kwa njia yao alitaka kuwabariki na kuwafundisha walimwengu mkate wa mbinguni.

Katika kukaa kwao Kaanani waisraeli waliruhusiwa kutumia chakula cha nyama, lakini kwa masharti maalumu ambayo yalielekea kupunguza matokeo mabaya ya baadaye. Kuhusu nyama iliyoruhusiwa, damu na shahamu ilikataliwa kuliwa. Wanyama hao pia waliruhusiwa kuliwa wakiwa katika hali njema. Kiumbe kilichoraruliwa au kufa chenyewe, au kisichotolewa damu kwa uangalifu hakikuruhusiwa kuliwa. Kwa kuasi mpango wa Mungu waisraeli walipatwa na tamaa ya uchu wa nyama wakavuna matokeo yake. Alipowaletea mkate kutoka mbinguni wao walitamani anasa za Misri *(Hesabu 11:4).*

Wakalia wakisema ni nani atakayetupa nyama tule. Kwa sababu ya kumkataa Bwana na kukumbuka nyama za Misri hasira ya Bwana iliwaka juu yao kisha upepo ukavuma kutoka kwa Bwana nao ukaleta kware, watu wakaondoka mchana wote kuwakusanya na usiku wote na siku ya pili yote.

Nao wakawaanika wote kandokando ya kambi kuizunguka pande zote. Kisha hapo hiyo nyama ilipokuwa ikali kati ya meno yao hawajaitafuna bado hasira ya Bwana iliwaka juu ya watu. Bwana akawapiga watu kwa pigo kuu mno, jina la mahali pale likaitwa Kibrothhataava maana ni hapo walipowazika hao watu waliotamani *(Hesabu11:16-34).* Aliwapa walichomtaka akawakondesha roho zao *(Zaburi 106:15).* Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano yakaandikwa ili kutuonyesha sisi tuliofikiwa na miisho ya zamani *(1Wakorintho10:1-11)*

## KUPUNGUA KWA MAISHA YA WATU

Mtu yeyote mwenye akili timamu anaelewa kuwa afya ya mwanadamu inayohusisha umri wa kuishi imebadilika na kuwa katika hali mbaya. Kama Adamu au mjukuu wake Methusela aliyeishi miaka 969 (*Mwanzo 5:27)* angefufuka leo aone kizazi cha watu wanaozeeka wakiwa na umri wa miaka 80 angeshangaa na kuomba arudi kabla na yeye kuugua ugonjwa wa moyo. Maisha yetu yamepungua kwa kiasi kikubwa. Wengi wanakula vyakula kwa ajili ya kutokufa haraka ingawa wanakufa polepole.Umri wa kuishi kabla Mungu hajaruhusu watu kula Nyama ulikuwa hivi:

| KIUMBE | UMRI ALIOISHI | USHAHIDI |
|---|---|---|
| Adamu | Miaka 930 | Mwanzo 5:3 |
| Sethi | Miaka 912 | Mwanzo 5:8 |
| Enoshi | Miaka 905 | Mwanzo 5:11 |
| Kenani | Miaka 910 | Mwanzo 5:14 |
| Mahalaeli | Miaka 895 | Mwanzo 5:17 |
| Yaredi | Miaka 962 | Mwanzo 5:20 |
| Methusela | Miaka 969 | Mwanzo 5:27 |
| Lameki | Miaka 777 | Mwanzo 5:31 |

Ulaji wa Nyama hata ile ambayo Mungu alikuwa ameitoa yaani ya wanyama walio safi ulikuwa na athari kubwa sana. Baada ya gharika watu walikula zaidi chakula cha Nyama. Mungu aliona kuwa njia za wanadamu zilikuwa mbovu na ya kuwa huelekea kujiinua kwa kiburi na kutenda kinyume na Muumbaji wake, kwa kufuata tamaa zao wenyewe. Naye akaruhusu watu wake waliokuwa wenye maisha marefu kula chakula cha nyama ili apate kuyafupisha maisha yao ya dhambi.

Bwana akasema Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele kwa kuwa yeye ni nyama basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini (*Mwanzo6:3)* Unabii unaorejea nyakati zao unaonyesha kuwa watu hao walianza kula nyama hata kabla Mungu hajawaruhusu *(CD 373).*

Kumbukumbu za Biblia zinaonyesha tofauti kubwa ya miaka ya watu wale walioishi kabla ya gharika na wale walioishi baadaye. Yeye (Mungu) aliruhusu taifa lile kula chakula cha nyama, taifa lile lililokuwa linaishi miaka mingi liliruhusiwa kula chakula cha nyama ili kupunguza maisha yao ya dhambi. Mara tu baada ya gharika taifa lile likaanza kupungua kwa haraka katika ukubwa wa mwili na wingi wa miaka yao. *(CD 373).*

Ulafi uliwafanya watu wakala kila kitu, ingawa nyama zile zilizoruhusiwa na Mungu sasa hivi si salama kwani wataalamu wamegundua magonjwa mengi yanatokana na ulaji wa Nyama. Je, iwapo nyama halali iliyoruhusiwa na Mungu sasa hivi siyo salama itakuwaje kwa ile ambayo hata Mungu alikataa isiliwe?

Kwa ajili ya kutafuta pesa wengi wamefanya wanyama najisi kama nguruwe kuwa miradi yao. Bahari na maziwa leo kunatupwa uchafu wa kila namna ambapo mabomba ya uchafu wote wa mijini unatupwa huko jambo linalofanya samaki nao wasiwe na usalama. Je, iwapo wale samaki halali alioruhusu Mungu waliwe usalama wao ni mdogo, itakuwaje kwa wale samaki ambao ni najisi? Yapo mambo mengi yanayochangia kudhoofika kwa maisha ya mwanadamu, moja ya mambo hayo ni ulaji wa Nyama.

## MADHARA YA NYAMA

Wale wanaokula nyama hula nafaka na mboga za majani zilizokwishatumika, maana mnyama hupata kutoka kwa vitu hivyo chakula ambacho husaidia kukua. Uzima uliokuwa ndani ya nafaka hizi hupita na kuingia ndani ya mwenye kuzila. Twaupokea uzima huo kwa kula nyama ya mnyama hatimaye. Basi ingekuwa bora kama nini kuupata mara moja uzima huo kwa kula chakula ambacho Mungu ametupatia sisi tukitumie! *(MH 311-313)*.

Kamwe Nyama haikuwa chakula bora kwani magonjwa ya wanyama yanaongezeka upesi sana. Mara nyingi wale wanaokula Nyama ikiwa wangewaona wanyama hao wakiwa hai na kujua hali ya Nyama wanayoila wangeiacha na kuichukia kabisa. "Mtu mmoja alipotaka kununua Nyama muuzaji alimwambia siku hiyo asingeweza kumuuzia Nyama ya siku ile kwa vile anamfahamu" Wanyama wengi wana magonjwa na kwa kushiriki nyama zao tunapanda mbegu za ugonjwa katika minofu ya miili na damu zetu *(MH 313)*.

Madhara ya chakula cha Nyama mara nyingine hayawezi kubainika upesi lakini hilo si jambo lenye kuthibitisha kuwa hakuna madhara. Ni wachache wawezao kuamini kuwa Nyama waliyokula ndiyo ambayo imetia sumu damu yao na kuwaletea maumivu, wengi hufa na magonjwa ambayo hutokana na ulaji wa Nyama *(MH 314)*. Haiwezekani Nyama ya mnyama kuwa ya kufaa kwa afya ikiwa sehemu yake kwa asili ni uchafu na ikiwa analishwa kila kitu cha kuchukiza.

Mara kwa mara wanyama huchukuliwa na kupelekwa kuuzwa mnadani ili wakaliwe kama chakula wakati wakiwa na magonjwa tele kiasi kwamba wafugaji wenyewe wameogopa kuendelea kuwafuga. Baadhi ya njia za kuwanonesha kwa ajili ya kuuzwa zinaleta magonjwa. Wanyama wengi hufugwa wakiwa wamefungiwa mahali pasipo na nuru wala hewa safi huku wakivuta hewa ya maboma machafu na pengine wakinoneshwa kwa chakula kilichooza hata miili yao itiwe na uchafu.

Mara kwa mara wanyama husafirishwa mbali na kuwekwa chini ya mateso makubwa wanapofika mauzoni. Wakiwa wametolewa mahali penye malisho ya majani mabichi na kusafirishwa maili nyingi za uchovu juu ya barabara zenye joto na mavumbi mengi.

Wakiwa wamelundikwa kwenye mabehewa machafu, huku wamenyimwa maji na chakula kwa saa nyingi, wanyama hawa wa kuhurumiwa wanaendeshwa mpaka wakifikie kifo chao ili kwamba wanadamu wajifanyie karamu ya kula mizoga. *(MH 314)*.

Wanyama wanaona na kusikia, wanapenda, wanasumbuka na kuogopa. Wanyama wengi huonyesha upendo unaoonyeshwa na baadhi ya binadamu. Ni mtu yupi mwenye moyo wa mwanadamu ambaye amewahi kutunza wanyama wa kufuga angeweza

kutazama macho yao ambayo yamejawa na imani na upendo na akawatoa kwa hiari wakachinjwe na kisu cha mchinja nyama? Je, Atawezaje kula nyama yao kama chakula kitamu? *(MH 316)*.

Chakula cha Nyama huibadili tabia, kutia nguvu hali ya kuvutwa tamaa za mwili tu. Miili yetu hufanywa kwa chakula tulacho na kula Nyama kwa wingi kutapunguza uhodari wa akili. Wanafunzi wangeweza kufaulu mambo mengi zaidi katika masomo yao kama wasingeonja Nyama. Kadri minofu ya mwili wa mtu inavyotiwa nguvu kwa kula Nyama ndivyo uwezo wa akili unavyopungua *(CD 392)*.

Kama kuna wakati ambapo yafaa chakula kiwe cha kawaida tu wakati huo ndiyo sasa. Haifai kuweka Nyama mbele ya watoto wetu. Madhara yake ni yenye kusisimua na kutia nguvu tamaa mbaya na kuelekea kuua uwezo wa tabia ya adili *(2T 352)*.

Hatuchori msitari halisi wa kufuatwa katika chakula, lakini twasema katika nchi zenye matunda, nafaka na mbegu jamii ya njugu kwa wingi nyama si chakula bora kwa watu wa Mungu. Imeamriwa kuwa Nyama huelekea kufanya mwili uwe na tamaa mbaya za kinyama, huwanyang'anya wanaume na wanawake ule upendo na huruma ambazo yawapasa kuwa nazo kila mmoja wao na kuacha tamaa mbaya za mwili kuutawala uwezo bora wa mtu.

Ikiwa kula Nyama kulipata kuwa jambo la manufaa kwa afya, wakati huo si sasa! Nyama si salama kwa afya!. Magonjwa ya cancer, uvimbe na kifua hutokana zaidi na kula Nyama. Wachungaji wengi wa makanisa leo wanajichimbia makaburi kwa meno yao. Kama tumbo lisipotunzwa vizuri na kufanyizwa kwa tabia nyoofu na ya adili ubongo na neva haviwezi kulihurumia. *(9T 153-166)*.

Wajibu mzito unawakalia wale waijuao kweli. Watu walio masalio wa Mungu hawana budi kuongoka. Wale ambao wamepokea mafundisho juu ya ubaya wa kutumia nyama, majani ya chai, kahawa na vyakula vilivyokolezwa sana kwa viungo na matayarisho ya chakula yasiyofaa kwa afya, wenye kukusudia kufanya agano na Mungu wanapaswa wafanye matengenezo ya afya.

Mungu anadai kuwa tamaa ya chakula iwe safi. Hiyo ndiyo kazi ambayo haina budi kutendwa. Miongoni mwa wale wanaongojea marejeo ya Bwana hatimaye wataachana kabisa na matumizi ya nyama. Nyama itakoma kuwa sehemu ya chakula chao *(CH 450*. Wako wale ambao wanapaswa kuwa wanafahamu hatari ya ulaji wa Nyama ambao wangali wakila minofu ya wanyama,na kwa kufanya hivi huhatarisha afya zao kimwili, kiakili na kiroho. Wengi ambao sasa wameongoka nusu nusu kuhusu kuhusu ulaji wa Nyama watawaacha watu wa Mungu wasifuatane tena. *(CH 575)*.

## WAKATI MUNGU ANAPOKUWA KIMYA

*Ni kazi bure kuwafundisha watu kumtazama Mungu mponyaji wa magonjwa yao pasipo kuwafundisha kuyakataa mazoea yao mabaya yanayoharibu afya (MH227). Mungu hatafanya muujiza wowote kuwaepusha na magonjwa wale wote wasiojali kutunza miili yao bali wanaendelea kuvunja sheria za afya, na wala hawafanyi juhudi yeyote kuyazuia magonjwa (MM 13).*

Wale wanaoutosheleza uchu wao wa chakula kisha wakaumwa halafu wakanywa dawa zenye sumu ili kujaribu kutuliza maumivu yao wawe na hakika kuwa Mungu hataingilia kati kuwaokoa na kutojali kwao. Mungu huwa haoni vyema kujibu maombi ya watu kama hao. *(MM 14)*

Nyakati za hatari zi mbele yetu, magonjwa ya kila aina yanawashika wanadamu, shetani anafanya kila awezalo kuutumia ujinga wa wanadamu ili kuwaletea magonjwa wale wanaodai kuwa wao ni wana na binti za Mungu. Ni wakati wako sasa kutumia nafasi zilizotolewa ili kujipatia maarifa ya mwili wa mwanadamu jinsi unavyoweza kutunzwa katika hali ya afya. *(CH 504)*.

SURA YA TISA

# KANISA LA DICTIONARY

Kamusi ya lugha ya Kiswahili na ile ya lugha ya kiingereza Pamoja na kamusi za Lugha zote ni vitabu vya kidunia vinavyoandikwa na wanadamu ili kurahisisha mawasiliano hususani kupata maana ya neno fulani. Kamusi au Dictionary sio kitabu cha Mungu wala si kitabu kitakatifu kwa kuwa hakina uvuvio. Maneno yaliyomo kwenye kamusi yana maana nyingi na yana tabia ya kubadilika maana zake kulingana na matukio au kupita kwa wakati au umri wa wahusika wanaotumia maneno hayo.

Neno "mtoto" linaweza kuwa na maana ya kiumbe mdogo anayenyonyeshwa au kubebwa mgongoni. Lakini neno hilohilo linapotumika kwa baadhi ya vijana wa kiume linaweza kumaanisha binti mzuri mwenye tabia nzuri ambaye hajaolewa bado. Mfano huo ueleweke tunapojifunza maana ya neno "kanisa" Utalielewa tu kanisa la kweli la Mungu kama ukijua maana ya neno "kanisa" kulingana na Biblia Takatifu na Roho ya unabii na sio kulingana na kamusi wala Dictionary zilizotungwa na wanadamu wanaokufa na kutoweka.

Neno kanisa lina maana tofauti katika kamusi au Dictionary ukilinganisha na maana ya neno hilohilo katika Biblia Takatifu na Roho ya Unabii. Hivyo tunapojifunza kuhusu kanisa la kweli la Mungu kama wakristo tunalazimika kutumia maana ya neno hilo iliyopo kwenye maandiko matakatifu na siyo vitabu vya kidunia. Hatupaswi kuruhusu chochote nje na neno la Mungu kituthibitishie juu ya lipi ni kanisa la kweli.

Tusitafute kutoka kwenye vyanzo vya dunia kwa maana tutajitenga na Mungu *(Yakobo 4:4)* Tusitegemee maarifa ya watu maana kufanya hivyo ni laana *(Yeremia 17:5)* tusitegemee hekima zetu maana ni upumbavu (*1wakoritho 1:19-20,3:19)* Maarifa ya neno la Mungu ndiyo msingi pekee wa kutuonyesha kanisa la kweli na Mungu.Ni kwa sheria na ushuhuda *(Isaya 8:20)* wa maandiko matakatifu ndipo tu tutaelewa na kuamini kuhusu kile kinachomaanishwa wakati neno kanisa linapotajwa.

Kamusi nyingi za lugha zinakubaliana kuwa neno "kanisa" maana yake ni :-
*Jengo la ibada ya kikristo,auJumuiya ya kikristo mfano kanisa katoliki,au*
*Waumini wanaoabudu chini ya kanisa moja,au Taasisi au chombo cha kikristo,au Taasisi iliyosajiliwa kuendesha mambo ya dini ya kikristo.*

Kama neno kanisa likitumia maana hizo hapo juu kutatokea athali zifuatazo:

(1) *Vikundi vingi vya kikristo visivyosajiliwa vitakuwa vimepoteza sifa ya kuitwa kanisa.*
(2) *Kusajiliwa kutakuwa ni kigezo cha kikundi kinachotaka kiwe kanisa.*
(3) *Ili mtu awe muumini itamlazimu kuhudhulia sehemu ya kutaniko na wenzake.*
(4) *Hata madhehebu yasiyoamini misingi ya Biblia kama tu yamesajiliwa kwa jina la dini na yanaendesha ibada zake vizuri yataitwa makanisa.*
(5) *Utangazaji wa Injili ya Yesu lazima uambatane na kuwaelekeza waumini kwenye Dhehebu.*
(6) *Kila mtu ana uwezo wa kuanzisha kanisa lake ikiwa tu anao mtaji na ametimiza vigezo.(inawezekana wingi wa makanisa ya leo ni kwa sababu ya uhuru huu)*
(7) *Ni lazima atakuwepo kiongozi mwanadamu ambaye ndiye atakuwa kichwa cha kanisa.Yeye ndiye atakuwa msemaji mwenye kauli ya mwisho wa kanisa.*

(8) *Kama haujajiunga na kundi lolote wewe siyo sehemu ya kanisa kwani hautambuliki kwa wenzako.*

Je, hatuoni madhehebu mengi ya kikristo yakiwa yamechukua maana yote ya neno kanisa kulingana na kamusi ya Kiswahili au Dictionary za lugha? Je hatuoni karibu kila kanisa lina msemaji (mwanadamu) ambaye ndiye kichwa cha kanisa? Kumbuka kuwa kila unapogusa dini ya kweli unagusa maandiko matakatifu, Kila unapogusa maandiko matakatifu unamgusa Mungu aliyeyatoa. Huyu ndiye mmiliki wa wanadamu wote ambaye wote tunatarajia kufika kwake tukiwa hai au wafu.Je, maana ya kanisa kulingana na kamusi ndiyo maana ya kanisa aliyoitoa Mungu? Je tunaweza kulifahamu kanisa la kweli kwa kusoma na kuifuata dini ya Kamusi? Je, dini ya Dictionary ndiyo dini ya kanisa la Mungu?

## KANISA LA MUNGU

Mtu akinipenda atalishika neno langu na Baba yangu atampenda nasi *tutakuja kwake* na kufanya makao kwake *(Yohana 14:23)* Nawapenda wale wanipendao na wale wanitafutao kwa bidii *wataniona(Mithali 3:17)* Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu, ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake, tu watu wake na kondoo wa malisho yake *(Zaburi 100:3)* Heri wenye moyo safi kwa maana hao watamuona Mungu *(Mathayo 5:8)* Ee mwanadamu yeye amekuonyesha yaliyo mema na Bwana anataka nini kwako ila kutenda haki na kupenda rehema na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako! *(Mika 6:8)* Mche Mungu naweuzishike amri zake maana kwa ujumla ndiyo impasayo mtu. *Mhubiri 12:13*

Tangu mwanzo watu *waaminifu* wamefanya kanisa duniani.*(AA11)* Kwa kuwa walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina langu nami nipo hapo katikati yao *(Mathayo*

*18:20)Heri walio na hekalu liwe ni jengo zuri au hafifu, Mjini au miongoni mwa Mapango ya milima ya mawe, katika Banda la hali duni au Jangwani, ikiwa ndipo mahali bora wanapoweza kupapata kwa ajili ya Bwana yeye atapatakasa mahali hapo kwa kuwapo kwake na patakuwa patakatifu kwa Bwana wa majeshi (Ellen G White-Testimonies For the Church vol 5 uk 491-492)*

Mimi ndimi mlango wa kondoo, mtu akiingia kwa mimi ataokoka *(Yohana 10:7-9)* Mimi ndimi Mchungaji mwema nao walio wangu nawajua*(Yohana 10:14)* nao walio wangu wanijua mimi, kaeni ndani yangu nami ndani yenu *(Yohana 15:4)* Lango hili ni la Bwana wenye haki ndiyo watakaoingia *(Zaburi 118:20)* Hakuna kanisa lingine mbali na mkusanyiko wa wale walio na neno la Mungu na wanatakaswa nalo.*(4SP 237)* Na ninyi kondoo zangu, kondoo za malisho yangu ni wanadamu na mimi ni Mungu wenu asema Bwana Mungu *(Ezekieli 34:31)*

KILE KINACHOFANYA KANISA LA MUNGU

Kamusi ya lugha yoyote haiwezi kueleza kile kinachounda kanisa la Mungu. Jengo la Matofali, Mbao, Vigae na Bati haviwezi kuunda kanisa la Mungu. Kamwe Mungu haundiwi kanisa na mwanadamu yeyote mwenye roho ya kufa duniani. Dhehebu tu lililosajiliwa serikalini ili liitwe kanisa haliwezi kuwa kanisa la Mungu.

Mkusanyiko mkubwa wenye hadhi wa kimadhehebu unaopendwa na wengi ambao umezoeleka duniani hauna uwezo wa kuunda kanisa la Mungu.Vyombo vya dhehebu vilivyopatikana kwa ajili ya mikusanyiko halali duniani, misaada halali kwa wasiojiweza pekee haviundi kanisa la Mungu. Kanisa la Mungu haliundwi kwa mazoeya ya kidini.Waumini wanaoabudu tu pamoja chini ya kanuni moja hawawezi kuunda kanisa la Mungu.

Hata kama dhehebu lako na mkusanyiko wote wakubwa kwa wadogo matajiri na masikini mkusanyike, kisha wote kwa pamoja mkapaza sauti juu sana kujiita kanisa la Mungu, baadaye mkaweka bango kuwa sasa mmekuwa kanisa la Mungu na mkaanza kuabudu kwa kicho sana bado hamtakuwa mmekuwa kanisa la Mungu.

Mungu ana uwezo kuunda serikali za wanadamu lakini serikali haina uwezo wa kumuundia Mungu kanisa. Usajili wa dhehebu kamwe haufanyi dhehebu liwe kanisa la Mungu wala serikali haina uwezo wa kusajili agizo la Mungu. Kuwa mchungaji, Askofu, Shemasi au mwalimu wa dini tu hakukufanyi uwe sehemu ya kanisa la Mungu.

Cheo chochote cha kidini ulichonacho hakikupatii upendeleo ukawa sehemu ya kanisa la Mungu. Kelele za madhehebu ya kidini yanayoshindana kujitukuza kamwe haziwezi kubadili sharti la kile kinachounda kanisa la Mungu. Mungu hatakuwa na hasara yeyote akichoma madhehebu yote duniani na waumini wake ikiwa watathibitika kuwa kumbe

hawakuwa kwenye kanisa la Mungu pamoja na wingi wa ibada zote walizozifanya. *Kuwa Mzungu, Mweusi, Mhindi, Mchina au mrembo sana, Msomi, Mjinga, Tajiri au Masikini hakukupatii upendeleo wa kuwa sehemu ya kanisa la Mungu kama hauna sifa. Kutokuamini kwako maneno haya hivyo hakukufanyi uwe sehemu ya kanisa la Mungu.Hakuna cheo duniani kitakachokupatia upendeleo mbele za Mungu.*

Maneno haya ya Yesu yakuingie sana akilini, kamwe usiyasahau tunapojifunza kuhusu zizi la Kristo. Kuna kondoo wengi wanaotakiwa watoke katika madhehebu na kuingia zizini mwa Kristo.*"Kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo, na kondoo wengine ninao ambao si wa zizi hili, na hao nao imenipasa kuwaleta, na sauti yangu wataisikia.(Yohana 10:15-16)*

Kitu pekee kinachounda kanisa ni uwepo wa Kristo. Mahali ambapo Kristo yupo ndipo pekee panapokuwa kanisa. Uwepo wake ndiyo unafanya watu waitwe kanisa. Sio uwepo wa Raisi au Waziri mkuu au Mbunge la hasha ni uwepo wa Mungu unaofanya sehemu kuwa Kanisa. Popote ambapo Kristo hayupo ni makao ya mashetani na pepo wachafu.

Ibada yeyote inayofanyika bila uwepo wa Mungu hata kama wataifanya kwa kicho namna gani watakuwa wanamuabudu Mungu bure. Ibada hiyo haina utofauti wowote na *kilabu cha pombe ambako wanywaji hula, hunywa, hufurahi, hulewa na kupigana huko*.Mungu aliwaambia wana wa Israeli,nao na wanifanyie patakatifu ili nipate kukaa kati yao.*(Kutoka25:8)*

*"Mungu analo kanisa, siyo Kanisa Kuu au Jimbo au Dayosisi*
*na wala siyo mikazo ya kitaifa wala mkusanyiko wa Madhehebu mbalimbali bali ni watu wanaompenda Mungu na kushika amri zake!*
*Mahali Kristo alipo miongoni mwa wanyenyekevu wachache hilo ndilo*
*kanisa la Kristo,maana kuwepo kwa Mtakatifu akaaye milele ndiko tu*
*kunakounda kanisa"*(*UL315)*

Hivyo uwepo wa Kristo ndio tu unafanya Kanisa la Mungu mahali popote. Hapa kuna kuna kitu muhimu sana cha kufikiri katika maisha ya kiroho. Ni kitu gani humfanya Yesu asikaribie wakati ibada inafanyika? Kristo hakaribii sehemu yeyote iliyonajisika kimwili na kiroho. Kamwe usisahau kuwa maandiko matakatifu yameandika hivi:

*Kristo kamwe hajilazimishi kuwa pamoja na mtu yeyote,ataingia kwa furaha katika nyumba yeyote ya wanyenyekevu wanaojishusha,lakini ikiwa watu hawajali kumsihi huyu*

*mgeni wa Mbinguni akae atapitiliza.Wengi watapata hasara kubwa kwa sababu hawamjui Kristo kama ilivyokuwa wakati alipotembea kwenda Emau.*
*(DA800,Tumaini la Vizazi Vyote sura ya 83 ukurasa 451)*

Mahali ambapo pana watu wengi waovu ila kuna mtu mmoja mwaminifu kwa Mungu, mtu huyo anakuwa sehemu ya kanisa la Mungu. Nuhu, Lutu na Eliya ni mifano hai, wao hawakukusanyika wala kusajiliwa popote ili watambulike na wanadamu lakini walikuwa sehemu ya Kanisa kwa nyakati zao na Mungu alikubali kuwatumia. Kama kuna mtu mmoja sehemu fulani ambaye amezungukwa na waovu naye hana mtu wa kufanya naye ibada, kumfariji au kuungana naye kwa chochote kinachohusu mambo ya kiroho kwa vile yuko peke yake, Mungu humhesabu mtu huyo kuwa ni sehemu ya kanisa naye itampasa afanye ibada peke yake. Mungu atakuwa pamoja na Mtu yule ampendae, ataingia kwake na kufanya makao.Na ninyi kondoo zangu, kondoo za malisho yangu ni Wanadamu na mimi ni Mungu wenu .*(Ezekieli 34:31)*

Kuna hatua ya kwanza ya kukufanya kuwa sehemu ya kanisa la Mungu. Kujiunga na dhehebu tu au dini yeyote siyo hatua ya kwanza. Wengi sasa hawana dini yeyote lakini ni sehemu ya kanisa la Mungu. Utashangaa kuwakuta mbinguni wakiwa na Yesu kama Kornelio kwa sababu walikuwa waaminifu kwa Mungu.

Kuna wakati ambapo dini zote na Madhehebu yote yalimwabudu shetani akabaki mtu mmoja tu na familia yake ambaye hakuwa katika dini yeyote ila alibaki kuwa mwaminifu. Mungu aliwaangamiza wote akabaki yeye na familia yake. Hii ndiyo hatari ya kuwa na dini kuliko kuwa na Yesu. Siku zote dini hazina uhusiano wowote na Yesu ila zina uhusiano mkubwa na Pesa kwa kutumia jina la Yesu.

Ndiyo maana kundi kubwa lililomchukia Yesu lilikuwa ni kundi la viongozi wa Dini. Kundi hili ndilo lililokuwa mstari wa mbele kuchekelea kifo cha Yesu wakati akilia kwa uchungu pale msalabani. Wakuu wa makuhani waliwapa askari fedha nyingi ili watangaze kuwa Yesu hakufufuka*(Mathayo28:11-13)*

Hao wamejaa leo kwenye makanisa ya Dictionary. Orodha ni ndefu ya waliouawa na viongozi wa dini kuanzia agano la kale mpaka leo hii. Kwa kumuua Kristo Makuhani waligeuka na kuwa vyombo vya shetani, wakajiingiza katika mtego wasioweza kujinasua. Niseme nini kuwaamsha watu wetu? Nawaambieni tena kwa huzuni, Ni Wachungaji wengi wanaosimama mbele za watu kufafanua maandiko walio wachafu. Mioyo yao imejaa ufisadi, mikono yao ni michafu*(1T608, 5T78.)*

Hata katika siku zetu ni muhimu kuelewa kuwa kanisa moja la kweli la Mungu leo siyo dhehebu fulani, siyo dini fulani yenye jina lililotukuka na kujinadi kwa sauti, la hasha kanisa la kweli la Mungu linajengwa na watu binafsi ambao ni waaminifu kwa Mungu.

Hakuna ubaya ikiwa watu binafsi waaminifu kwa Mungu wasio na waa wala kunyanzi wakikusanyika pamoja lakini mkusanyiko wao hauongezi wala kupunguza utukufu wowote hata kuwazidi wale ambao hawajakusanyika kwa sababu kile kinachothibitisha na kudhihirisha kanisa la Mungu ni uwepo wa Kristo *(Mathayo 5:48)* Wakati Yesu akiwa duniani vita ya kidini ilikuwa inatisha, Watu wa madhehebu mbalimbali ya wakati huo walikuwa wakipigana vita wenyewe kwa wenyewe kwa ajili ya kupata waumini na kujitangaza kila dhehebu likijidai kuwa ndio la kweli la Mungu na kwamba wengine wote wamepotoka. Je, kristo alihalalisha Imani hiyo? Je Yesu alichagua dhehebu moja kuwa bora kuliko watu binafsi waaminifu kwa Mungu? Mwanamke mmoja alimuuliza Yesu swali hili moja kwa moja, Tafadhali soma kwa makini na kwa uangalifu uone jibu la Yesu kwa huyu mwanamke.

> "Yule mwanamke akamwambia Bwana naona ya kuwa u Nabii, Baba zetu waliabudu katika mlima huu *(Hekalu katika mlima Gerizimu)* nanyi husema ya kwamba huko Yerusalemu ni mahali patupasapo kuabudu. Yesu akamwambia, Mama unisadiki saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu wala kule Yerusalemu. Ninyi mnaabudu msichokijua sisi tunaabudu tukijuacho kwa kuwa wokovu watoka (ulikabidhiwa) kwa Wayahudi. Lakini saa inakuja nayo saa ipo ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho na kweli*(Yohana 4:19-24*)

Neno zuri la kunenepesha mifupa ni hili, unaweza kumwabudu Mungu ukiwa hapo hapo nyumbani kwako kama walivyofanya Mitume na Wafuasi wengine wa Kristo na Ibada yako itakubaliwa mbele za Mungu, soma *Warumi 16:4-11, IWakorintho16:19, Filemoni 1:1-2.* Maarifa haya mazuri kwamba kanisa la Mungu limejengwa na watu binafsi waaminifu popote walipo na kamwe halijajengwa na dini au Dhehebu fulani ndiyo yatakuweka huru katika Yesu. Imani hii itakutoa katika utumwa wa watu na kukuweka huru katika Kristo.

| KANISA LA MUNGU | KANISA LA DICTIONARY |
|---|---|
| Linajengwa na watu waaminifu. | Limejengwa na Dhehebu lililosajiliwa. |
| Ushirika na Yesu | Ushirika wa Dhehebu |
| Imani kwa Mungu wako | Imani kwa Dhehebu lako |
| Kristo tumaini letu | Dhehebu tumaini letu. |
| Linajulikana kwa kufanana na Yesu | Linajulikana kwa kusajiliwa |
| Kauli ya mwisho ni Biblia | Kauli ya mwisho ni kiongozi wa Dhehebu |
| Wanapita njia nyembamba ya Mbinguni | Wanapita njia pana ya Upotevuni |

KANUNI ZA KUJIUNGA NA KANISA LA DICTIONARY

Nijiunge kwenye Dini ya Dhehebu fulani kwanza, Nikashikamane moja kwa moja na Dhehebu hilo. Macho yangu, Imani na usikivu wote vielekezwe kwenye Dhehebu kama njia ya wokovu, Nilipende Dhehebu langu kuliko madhehebu mengine maana hili ndilo la kweli pekee. Nitii amri za kiongozi, sera na mafundisho yote ya dini yangu ili niwe muumini halisi. Niamini kuwa kwa kuwa katika Dhehebu hilo nimekuwa sehemu ya mwili wa Kristo na nikijitenga na Dhehebu au nikifukuzwa kwa kutowatii viongozi basi nimejitenga na mwili wa Kristo.Niamini kuwa lolote litakalofunguliwa na Dhehebu langu duniani basi na Mbinguni limefunguliwa na lolote litakalofungwa na Dhehebu langu Duniani basi na Mbinguni litakuwa limefungwa.

Niende kuwashawishi watu wajiunge na Dhehebu langu ili Mungu awapokee na kuwapa wokovu. Ubatizo ni hatua kubwa ya kujiunga na dhehebu na kama nikiasi Dhehebu nitakuwa nimemuasi Mungu. Sitapata pumziko kwa Kristo mpaka nimejiunga na Dhehebu.Yesu aliposema mwisho kutakuwa na zizi moja chini ya Mchungaji mmoja nielewe kuwa mwisho watu wote watatoka katika Madhehebu mengine na kuja katika Dini yangu na ndipo Yesu akija atatuchukua sisi huku wale waliogoma kujiunga na Dhehebu letu wakitupwa kwenye moto wa milele.

Ndugu zangu akina Dada na Kaka zangu, matokeo ya hatari kwa wale wanaoamini namna hii ni kwamba, viongozi wa Dini yako wanaweza kuwa wamepotoka na kuwa waovu kama shetani mwenyewe na dini yako inaweza kutoka katika ukweli wa Biblia na kuanza kufuata mafundisho ya kuzimu lakini wewe hutaliona hilo. Kwa nini? Kwa nini?, Kwa sababu wewe umejenga imani kwenye dini badala ya kujenga kwa Yesu nawe unaamini kuwa kanisa linajengwa na Dhehebu lako. Hata kama ungeonyeshwa na kuthibitishwa kuwa dhehebu lako linatawaliwa na shetani imani kwa Dini yako haitatikisika kwa sababu wewe umedanganyika ukaaminishwa kuwa ukijitenga tu na Dhehebu basi umejitenga na Kristo!. Huu ni udanganyifu wa kutisha unaohubiriwa sana duniani. Kwa kuamini hivi utakuwa umefuata barabara ile mbaya ya Dini ya Wayahudi. Je wayahudi walikuwa na dini gani ya namna gani?

Wayahudi waliabudu Hekalu nao walijazwa na hasira kwa kitu chochote ambacho kingesemwa kinyume na Jengo hilo kuliko hata kingesemwa kinyume na Mungu *(EW 198)* Kuhani wao Mkuu alikuwa ni Rais *(DA133)* na wakapangilia kanisa katika Msonge wa madaraka kikanisa ambapo mwanadamu alitawaliwa na mwanadamu *(DA232 & 395)*. walikuwa wamemchagua kiongozi (shetani) aliyewafunga kwa mnyororo kwenye gari lake kama mateka wakiwa wamechanganyikiwa na kudanganyika walikuwa wanakwenda katika msafara wa giza kwenye uharibifu wa milele katika mauti ambako hakuna tumaini la maisha huku wakielekea usiku ambao hapana asubuhi *(DA36)* Lakini

bado hawa viongozi waliwafundisha watu kwamba kule Yerusalemu ndipo wangemwabudu Mungu *(DA154)*.

Baraza la Sanhedrin lilikuwa limekataa ujumbe wa Kristo na lilinuia kumuua. Kwa hiyo Yesu alitoka Yerusalemu, Kutoka katikati ya Makuhani, hekalu, viongozi wa Dini na watu waliokuwa wameelekezwa katika sheria, na kugeukia tabaka jingine ili kutangaza ujumbe wake, na kuwakusanya wale wote ambao wangeweza kubeba Injili kwa Mataifa yote (DA232)

Ninakusihi sana uzielewe fikira hizi mbili tofauti na uchague upande mmoja wa kuamini. Upande mmoja unakuongoza katika kutokuguswa na kitu chochote zaidi ya kukuunganisha na Yesu Kristo na upande mwingine unamficha Kristo nyuma na kuwatanguliza wanadamu. Mungu hamlazimishi Mtu yeyote amuabudu wala kumfuata. Ninainua mikono yangu mbinguni kwa ajili yako nikikuombea sana kwa Mungu ulielewe hili. Ninakusihi sana tena kwa dhati ya moyo wangu wote kwako kwamba *usikubali kuwa chini ya mwanadamu anayekufa unapomtafuta Yesu asiyekufa*. Kiongozi wa Dhehebu anaweza kukuzuia usimtafute mwanakondoo alipo kisha kiongozi huyo huyo akakuelekeza kanisa lake lilipo. Kurasa za maneno haya zinapita mbele ya macho yako mimi nikiwa nimenawa mikono.

Hatupo tena chini ya mfumo wa agano la kale ambapo Uwepo wa Mungu ulikuwa katika Jumba linalooneka katika patakatifu pale ambapo Mungu alimwambia Musa, nao wanifanyie patakatifu ili nipate kukaa kati yao, kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai, *(2Wakoritho 6:16)* Kumbuka Yesu alisema yeye ndiye njia ya kweli na uzima mtu hafiki Mbinguni bila ya kuunganika naye wala hakusema Dhehebu ndiyo njia ya ukweli na uzima.

Je tufanye nini ili tuwe sehemu ya kanisa la kweli leo? Ni kwa kuungana na Kristo. Je, tunaunganaje na Kristo? Kwa kutambua kuwa tumevunja sheria zake na tunamuhitaji Mwokozi *(Yohana 3:4 Warumi 3:20*, *Warumi 6:23)* Kwa kumkiri, kumtukuza, kumwamini na kumpenda huku tukieneza neno lake, si kwa maneno ya wanadamu, ndipo tutavalishwa vazi la Kristo.Swali kuwa nifanye nini ili niwe sehemu ya kanisa la kweli, lina jibu sawa na lile ambalo mtu mmoja alimuuliza Yesu kuwa nifanyeje nini ili niurithi uzima wa milele. Majibu ya maswali hayo yote mawili yanafanana.

## HITAJI LA KUWA NA IBADA YA NYUMBANI

Kama wazee wa zamani, wale wanaompenda Mungu wanapaswa kujenga Madhabahu mahali popote wanapojenga hema yao. Kama kuna wakati ambapo kila nyumba inapaswa kuwa nyumba ya maombi wakati huo ni sasa. Akina Baba na akina Mama wanapaswa kuinua mikono yao kwa Mungu mara kwa mara wakiomba kwa unyenyekevu kwa ajili ya watoto wao. Hebu akina Baba wakiwa kama Makuhani wa nyumba zao watoe juu ya Madhabahu kafara za asubuhi na jioni wakati mke na Watoto wakiungana katika maombi na kusifu. Nyumba kama hiyo Yesu ataipenda na kukaa humo. Katika kila nyumba ya Mkristo Nuru takatifu inapaswa kuangaza. Upendo unapaswa kumiminika kwenda kwenye nyumba zote zinazozunguka maeneo hayo. Kwenye nyumba kama hizi maombi ya asubuhi na jioni hupanda juu kwa Mungu kama uvumba wenye harufu nzuri. Rehema zake na mibaraka hushuka kwa waombaji kama umande wa asubuhi. *(PP144)*

Wewe unayejikuta upo peke yako na wenzio wote wapo katika madhehebu usiyokubaliana nao usiwe na shaka maana Kristo Yesu ni kuhani mkuu na mpatanishi aliyekuwa na Nuhu yule mwenye haki. Yesu yupo nawe hatakuacha, Mungu aliyekuwa na Eliya pale Karmeli atakuongoza na kukulinda. Yule aliyekuwa katikati ya moto akawaokoa vijana wale watatu yupo karibu nawe kuliko unavyoweza kufikiri. Ameahidi kuwa hatakuacha wala kukupungukia, naye atakuwa nawe popote uendapo.

Wewe ambaye upo peke yako usisahau kuwa hata yesu alipita njia hiyo. yalikuwepo Madhehebu mengi wakati wa Yesu lakini mara nyingi alikutwa peke yake akiomba kwenye mlima wa mizeituni na penginepo,Yesu alikuwa akijiepua, akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba (Luka 5:16) Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko (Marko 1:35.) Mara nyingi Yesu na wanafunzi walienda zao faragha mashuani, mahali pasipokuwa na watu (Marko 6:32) Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu (Luka 6:12) Hata Danieli alikuwa peke yake alipojua ya kuwa yale maandiko yamekwisha kutiwa sahihi, hakutaka kwenda kwenye madhehebu ambayo yalikubaliana na Mfalme kumwasi Mungu bali aliingia nyumbani mwake, (na madirisha katika chumba chake yalikuwa yamefunguliwa kukabili Yerusalemu;) akapiga magoti mara tatu kila siku, akasali, akashukuru mbele za Mungu wake, kama alivyokuwa akifanya tokea hapo (Danieli 6:10)

Maneno ya kinywa cha nabii Isaya yanathibitisha kuwa hata wakati wa kubeba dhambi za ulimwengu Yesu alikuwa peke yake (kama wewe leo) hakuwa na mwenzie, Nalikanyaga shinikizoni peke yangu; Wala katika watu hakuwapo mtu pamoja nami; Naam, naliwakanyaga kwa hasira yangu, Naliwaponda kwa ghadhabu yangu; Na mavazi yangu yametiwa madoa kwa damu yao, Nami nimezichafua nguo zangu zote

(Isaya 63:3) Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao (Mathayo 18:20)

Ushindi mkubwa wa kanisa la Kristo au kwa mkristo mmojammoja haupatikani kutokana na talanta, elimu, utajiri au fadhila za wanadamu, bali unapatikana katika chumba pamoja na Mungu, wakati kusihi na imani yenye nguvu inapojiweka katika mkono wenye nguvu. *(PP203)* Na Mungu je! Hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku naye ni mvumilivu kwao? Nawaambia atawapatia haki upesi. *(Luka 18:7-8)*

SURA YA KUMI

# PICHA YA SHETANI

Jihadhari usije ukamsahau BWANA Mungu wako kwa kutozishika amri zake na hukumu zake na sheria zake ninazokuamuru leo. Angalia utakapokuwa umekula na kushiba na kujenga nyumba nzuri na kukaa ndani yake. Na makundi yako ya ng'ombe yatakapoongezeka na kila kitu ulicho nacho kitakapoongezeka, basi hapo moyo wako usiinuke ukamsahau BWANA Mungu wako maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri. *(Kumbukumbu la Torati 8: 11-14,18.)*

Lakini jihadhari nafsi yako ukailinde roho yako kwa bidii usije ukayasahau mambo yale uliyoyaona kwa macho yako yakaondoka moyoni mwako siku zote za maisha yako bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako. Jihadharini nafsi zenu basi maana hamkuona umbo la namna yeyote siku ile BWANA aliyosema nanyi kutoka kati ya moto. Msije mkajiharibu nafsi zenu mkajifanyia sanamu ya kuchonga mfano wa sura yeyote mfano wa mwanamume au mwanamke mfano wa mnyama yeyote aliye duniani au mfano wa ndege arukaye mbinguni…Tena usije ukainua macho yako hata mbinguni, na ulionapo jua na mwezi na nyota jeshi la Mbinguni lote pia ukashawishiwa na kuviabudu na kuvitumikia ambavyo BWANA Mungu wako amewagawanyia watu wote chini ya Mbingu zote. *(Kumbukumbu la Torati 4:9,15-19)*

*Msijifanyie sanamu yoyote wala msijisimamishie sanamu ya kuchonga wala mnara wala msiweke jiwe lolote lililochorwa katika nchi yenu ili kulisujudia kwa kuwa mimi ndimi BWANA Mungu wenu. (Mambo ya Walawi 26:1)*

Basi mtamlinganisha Mungu na nani? Au mtamfananisha na mfano wa namna gani? *(Isaya 40:18)* Mtanifananisha na nani basi nipate kuwa sawa naye? Asema yeye aliye mtakatifu (25). Mimi BWANA ndilo jina langu na utukufu wangu sitampa mwingine wala sitawapa wanadamu sifa zangu. *(Isaya 42:8)*

Kuna picha iliyo zoeleka machoni pa wengi inayojulikana kama picha ya Yesu Kristo. Je Yesu aliwahi kupigwa picha? wakati alioishi kulikuwa na vifaa vya kunasa picha? Lakini je mbona mara nyingi Yesu anachorwa Mzungu na Shetani Mwafrika? Je kuna mtu aliyewahi kumchora wakati akiwa duniani? Je hakuna hata mnara wowote wenye picha yake halisi? Biblia imezungumza nini juu ya picha tunayoiona leo ikidaiwa ni yake?.

Kwa hakika hakuna mwanadamu yeyote aliye na picha kamili ya Yesu Kristo. Wale waliokula na kunywa pamoja naye ambao ni wanafunzi wake hawakuacha chochote juu ya picha yake. Kristo akiishi ulimwenguni kwa miaka thelathini na mitatu alikabiliwa na fedheha, matusi na dhihaka alikuwa amekataliwa na kusulubishwa *(Isaya 53: 3 -9)*. Hata wakati wa kupaa kwake Mbinguni lilikuwa tukio lililowaduwaza tu wanafunzi wake wasiamini walichokiona. Hakuna mtu aliyekuwa na kamera kumpiga picha akipaa.

> "Akiinyosha mikono juu yao katika kuwabariki na kana kwamba anawahakikishia ulinzi wake kwao, aliinuliwa taratibu kutoka kwao akivutwa kwenda Mbinguni kwa nguvu kuu kuliko uvutano wowote wa duniani. Alipokuwa akipanda wanafunzi wake walimkodolea macho mara ya mwisho Bwana wao". *(DA831)*

Wazo la kuwa na kielelezo cha picha ya Yesu lilikuja baadaye Mitume wote walipokwisha kufa. Hata hivyo picha yenyewe imekuwa ikibadilika badilika kulingana na mataifa na rangi za watu. Waafrika wanataka picha ya Yesu awe Mwaafrika huku wazungu wakimuigiza kama mzungu. Wahindi na Wachina wanataka Yesu pia afanane nao, lakini yeye asema Mtanilinganisha na nani nipate kuwa sawa naye?

Bwana Mungu analinganisha wanaokaa duniani kama panzi wakiwemo wanadamu. Mungu hawezi kufananishwa na wanadamu waliofananishwa na panzi. Kwa muda mrefu shetani amekuwa na mkakati wa kushusha hadhi ya Kristo kwa kumdhalilisha machoni pa wanadamu.

Kwa ujuzi wa kutengeneza sanamu za kila aina ili waziheshimu badala ya Mungu. Mawazo ya wanadamu yamevutwa kwa vitu hivi hafifu. Mungu aliyeongea na Musa ndiye aliyetokea duniani tena, kama kuna mtu aliyepaswa kuwa na picha hiyo ni Musa maana yeye alimwona uso kwa uso. *(Kumbukumbu la Torati 34:10)* lakini Musa hakufanya hivyo.

Watu walioishi zamani hawakuhitaji picha ndipo waamini. Kuvunja amri za Mungu ni pamoja na kutengeneza picha ya Yesu ya kuchora au kuchonga ili kuiweka mahali patakatifu. Kuweka chochote kinachowakilisha Yesu, au Roho Mtakatifu ni dhambi picha hizo zimeondoa mawazo ya watu yasimwelekee Mungu.

*"Sanamu ya kuchora yafaa nini hata aliyeichora ameifanya? Sanamu ya kuyeyusha nayo ni mwalimu wa uongo. Je, kitu hicho kitakufundisha? ( Habakuki 2: 18-19)*

Mungu hapatani na sanamu yeyote, historia yaonyesha kuwa sanamu nyingi na picha zinazochorwa zilianza wakati miungu ya kale ya Kipagani ilipoanza kuabudiwa. Huu ni wakati watu walipo zifanya shingo zao ngumu wakaziasi amri za Bwana *(2Wafalme17:14)* Watu wasingeweza kuibadilisha sabato kwanza mpaka walipoikataa Torati kama ilivyo

leo. Kuigeuza sabato kwenda Jumapili kulitanguliwa na kukataa torati ndipo mlango wa upagani ulipoingilia wakati huo sanamu zikahalalishwa.

"Tena wana wa Israel wakafanya kwa siri mambo yasiyokuwa mema juu ya BWANA wakatenda mambo mabaya ili wamkasirishe BWANA. Wakatumikia sanamu ambazo Bwana aliwakataza,wakaziacha amri zote za BWANA, Wakajifanyizia sanamu wakaliabudu jeshi lote la Mbinguni wakamtumikia Baali , wakawapitisha watoto wao waume na wake motoni wakapiga ramli wakafanya uchawi wakajiuza nafsi zao wapate kufanya maovu machoni pa BWANA hata kumkasirisha". *(2Wafalme 17:8-17)*

Maandiko matakatifu yameonya juu ya uasi huu kwamba ungejitokeza tena siku za mwisho. Shetani anafanya kazi bega kwa bega katika makanisa ili kukamilisha Ukristo wake. Ukristo wa shetani umeambatana na picha ya shetani iliyobuniwa kwa ajili ya kuwatoa wanadamu katika imani kwa Mungu. Kupitia picha inayodaiwa ni ya Yesu wanadamu wamekoseshwa imani. Kamwe imani chanzo chake si kuona. Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo. *(Warumi10:17.)* Maana twaenenda kwa imani si kwa kuona. *(2 Wakorintho 5: 7)*

Yesu alipomwambia Tomaso heri wanaoamini bila kuona alitufundisha kuwa hatuhitaji kuona picha yake ndipo tuamini *(Yohana 20:24-29)* watu wa Mungu leo watampenda Kristo ijapokuwa hawamwoni; hawatahitaji kielelezo ndipo waamini. "Naye mwampenda ijapokuwa hamkumwona ambaye ijapokuwa hammwoni sasa mnamwamini na kufurahi sana kwa furaha isiyoneneka yenye utukufu. *(1Petro1:8)*

Kuchora au kuchukua picha ya mtu ili kutoa kielelezo jinsi Mungu alivyo ni makosa kwani Mungu hafananishwi na kitu chochote hata na malaika sembuse na binadamu aliyefananishwa na panzi?"Maana ni nani katika Mbingu awezaye kulinganishwa na BWANA? Ni nani afananaye na BWANA miongoni mwa malaika? *(Zaburi 89: 6, 40: 5.)*

Kulinganisha vitu vitakatifu kuwa sawa na vitu vya kawaida ni makosa makubwa mbele za Mungu. Wale wanaoshughulika na kazi ya Mungu wanapaswa kutembea katika hekima ya Mungu badala ya hekima yao. La sivyo watakuwa katika hatari ya kuweka vitu vitakatifu katika viwango sawa na vitu vya kawaida na mwishowe hali hii itawatenganisha na Mungu *(EV639)*

Tangu shetani alipotuletea picha inayodaiwa ya YESU Kristo watu walikoseshwa imani. Wakati wa maombi ya siri hisia takatifu zimeelekezwa katika picha ya uongo badala ya kuelekezwa kwa yule asiyeonekana. Wengi wameongozwa kuangalia vinavyoonekana badala ya kuangalia vile visivyoonekana. Watoto wadogo jilindeni nafsi zenu na sanamu. *(IYohana 5:21)*

Wanahistoria wa kidunia wanatusaidia kueleza picha hii ya shetani jinsi ilivyo kuja. Katika kitabu cha *The Human Experience A world History ukurasa. 248, 249,250* wanahistoria hao yaani *Farah, Karls* na *Korteper* wanaeleza kuwa "Wachoraji wa Kiitalia waliacha kuchora michoro yao ya kale na kuanza kuchora vitu, wanyama na watu katika hali ile ile wakionyesha uhalisia wa watu jinsi wanavyonekana maishani.

Baadaye *Giotto* alianza kuchora picha zenye Uhalisia zilizoleta hisia kali. Uchoraji ulifikia kiwango cha juu mwanzoni mwa mwaka 1500 ambapo wachoraji wengi walijitokeza mpaka alipojitokeza *Michelangelo Buonarrot* aliyemchora Yesu akiwa amekufa katika mikono ya Mariamu. Mchoro huu ulisifiwa na kuleta hisia kali.

Mwaka 1505 *Michelangelo* alikodishwa na Papa Julius wa Pili akafanye kazi ya uchoraji huo Vatican ambapo alichora picha nyingi za hadithi za biblia. "Wakati kazi zake zilipoonyeshwa hadharani ulimwengu wote ulikimbia kuja kuona kile *Michelangelo* alichofanya. Kwa hakika ilikuwa kama kila mtu alipatwa na butwaa na kukosa la kusema". Papa alimtukuza kwa zawadi nyingi za thamani zilizomtajirisha. Mchoraji mwingine aitwaye *Raphaeli Santi* anafahamika kwa kumchora Mariamu mama wa Yesu. Ndipo uchoraji huo ulipotawanyika na kuenea.

Wachoraji wa Italia na wanazuoni walisafiri kwenda nchi za kigeni na kuingia katika vyuo vikuu … katika mahusiano haya uchoraji wa Italia ulienea sehemu nyingi huku ukiboreshwa kwa kutumia rangi za mafuta. Wachoraji hao walichora picha hizi kwa kufuata utamaduni wao wa Kirumi.

Picha inayodaiwa ya Yesu Kristo inafanana na watawala wa Kirumi walioishi miaka mingi hata kabla ya kuzaliwa kwa Kristo duniani. Mpango wa shetani uliofaulu ni kututoa katika imani kwa Mungu na kutuelekeza katika picha iliyobuniwa kwa hila zake (Mchezo huu hatari umefikia kiwango cha juu ambapo leo watu hai wamesimama na kuigiza maisha ya Yesu. Hakuna mwanadamu atakayefanana na Kristo kwa kuigiza. Mungu ameonya mwanadamu asiongeze kile ambacho biblia haijaruhusu. Mwanadamu amepewa kikomo chake ambapo anapovuka mpaka huo hukumu za Mungu haziwezi kucheleweshwa zaidi. *(PK417)*

Shetani atakuja akimuigiza Kristo akitumia picha hiyo ambapo wengi watampokea. Kwa sababu Yesu atakuja tofauti na picha tuliyotazamishwa watu wengi hasa wakristo watamkana. Itakuwa rahisi zaidi wapagani wasioijua picha ya Kristo kumpokea ajapo, kuliko Wakristo waliodanganywa picha ya Kristo kisha Kristo akaja tofauti na picha waliyoizoea halafu wamwamini.

Wakristo wengi wamempokea shetani katika nyumba zao, makanisa yao na wengine wanatembea naye, wengi wamebandika picha ya shetani katika kuta za nyumba zao. Matendo haya potofu yanapofanyika Kristo huyatazama kwa huzuni akiurudia usemi

aliomwambia Tomaso kuwa heri wanaomwamini Kristo bila kuona picha yake. Ni wakati wa kutoa picha zote za shetani na kumkaribisha Kristo kwa imani ambaye chanzo chake ni kusikia.

Mkristo haupaswi kuiga kile wengi wafanyacho *(Mathayo7:13 – 14)* bali kufuata kile biblia ilichoagiza wala msiwe waabudu sanamu kama wengine walivyofanya. Maana wao walifanya shingo zao ngumu kama shingo za baba zao wakaziacha sheria za Mungu na agano lake na shuhuda zake wakafuata ubatili na kuandamana na mataifa waliowazunguka ambao Bwana alionya wasiende pamoja nao lakini wao waliziacha amri za Bwana wakajifanyia Baali, wakawapitisha watoto wao waume kwa wake motoni, wakapiga ramli, wakafanya uchawi, wakajiuza nafsi zao wapate kufanya yaliyo maovu machoni pa Bwana hata kumkasirisha. *(2Wafalme17:14-17)*

Damu za watoto wengi watakapopotea zitadaiwa mikononi mwa walimu wa uongo waliowapotosha wakawafundishia picha hizo. Wengi wamewadanganya watoto kwa kuwafundisha kuwa shetani ni kiumbe mbaya wa ovyo mchafu mwenye mkia asiyeeleweka. Ni mpango wa shetani kuuhadaa ulimwengu kwa mawazo hayo potofu. Biblia imeeleza shetani alipoumbwa aliumbwa akiwa mkamilifu, na mzuri. *(Ezekieli 28:12-18)*

Ukristo wa shetani ulianza kuenea tangu karne nyingi shetani alipoingiza maovu kwa siri. Wakristo wa kwanza waaminifu baada ya Kristo kufa walipotetea imani; Shetani aliazimia kusimamisha bendera yake katika kanisa la kristo ili kupata wakristo wadanganyifu *(GC42)* badala ya mateso yaliyotumika hapo kwanza sasa shetani akatumia vishawishi na hekima. Ibada ya sanamu ilikubaliwa na kuwa sehemu ya Ukristo na Ukristo wa kweli ukakataliwa. Katika vazi hili la Ukristo wa kujifanya shetani alijipenyeza kanisani na kuchafua imani yao.

Mtume Paulo akitazama tukio hili kwa darubini ya Kinabii alionya kuwa baada ya kufa kwake jambo hili lingejitokeza tena. *(Matendo 20:28-30)* Wakristo wengi baadaye walipotoka kabisa, mwisho wakafanya muungano wa Ukristo na Umizimu. Muungano huu ndio ulionywa na Mtume Paulo *( 2 Wakorintho 6:14 – 16)* ingawa waabudu sanamu walijidai kuungana na kanisa lakini walishikilia sanamu zao tu ila walibadili sanamu zao ziwe mfano wa Yesu na mfano wa Maria na watakatifu wengine *(GC43)* Uovu huu unaoendelea tena ulikatazwa tangu wana wa Israel wanatoka Misri *(Kumbukumbu 4:15 – 17)* Picha zinazodaiwa za Yesu na Maria zilipoingizwa kanisani shetani alishangilia *(GC45)* kama vitu hivyo ni maadui wa shetani iweje vilipoingia kanisani shetani ashangilie? Tangu wakati huo kanisa lilichafuka huku shetani akipandikiza Mbwa Mwitu katikati ya Kondooo. Kwa wengi leo ni ndoto za mchana kuamini kuwa katika kila dhehebu idadi kubwa ya viongozi wanaongoza kwa kutetea maovu wengine ni wapagani wa kutisha.

Ukweli unayeyuka kama barafu huku uongo ukizidi kukumbatiwa. Hata lini Yesu atalia kwako kuwa damu yake ilipotea bure?

Adui anajiandaa kuudanganya ulimwengu mzima kwa njia ya kutenda miujiza. Atajigeuza awe mfano wa malaika wa nuru, atajigeuza awe mfano wa Yesu Kristo. *(2SM96)* Kwa maana watatokea makristo wa uongo na manabii wa uongo watakaofanya ishara na maajabu wapate kuwapoteza yamkini hata walio wateule. *(Mathayo 24:24)*

Shetani anatanda uwanjani na kuigiza umbo la Kristo atayawakilisha mambo kinyume na kutumia vibaya kupotosha kila kitu wala si ajabu maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru *(2 Wakorintho 11: 14 – 15)*

Matukio ya ajabu ambayo shetani atajifungamanisha nayo karibu kutokea shetani atawafanya watu kuwa wagonjwa na ghafla atawaondolea nguvu zake za kishetani. Matendo haya yanayoonekana kama ya uponyaji yatakuwa ni mtihani kwa Waadventista wa Sabato.*(2SM53)*

Kwa kadri kutokea mara ya pili kwa Bwana wetu Yesu Kristo kunavyokaribia mawakala wa kishetani wanaendeshwa kutoka kuzimu. Shetani hataonekana kama mwanadamu tu bali ataigiza umbo la Kristo na ulimwengu ambao umeukataa ukweli utampokea shetani kama Bwana wa Mabwana na Mfalme wa Wafalme. *(5Bible Commentary ukurasa1105 –1106)*

Kama watu wa Mungu tunapaswa kusimama katika jukwaa la ukweli wa milele ambalo limesimama imara dhidi ya majaribu na taabu. Tunapaswa kushikilia nguzo zetu za imani, kanuni kuu za kweli za Mungu zimefunuliwa kwetu ndizo misingi ya imani yetu pekee. Wingi wa miaka hauwezi kugeuza thamani yake. Ni mkakati wa adui kuondoa kweli hizi mahali zilipowekwa na mahali pake kuwekwa mafundisho ya uongo. Adui ataingiza kila kitu cha uongo wake lakini Mungu atainua watu wenye hisia kali za utambuzi watakaorudisha kweli zote kulingana na mpango wa Mungu. *(1SM201)*

## MUIGIZAJI WA FILAMU YA YESU NI NANI?

Brian Deacon ni raia wa Uingereza mwenye asili ya Kiisraeli. Huyu ni binadamu wa kawaida mwenye mke na watoto. Huyu ndiye muigizaji aliyeigiza kama Yesu na kuvaa Uhusika wa Yesu. Alizaliwa tarehe 13/2/1949 huko Oxford Nchini Uingereza. Brian Deacon ni mtoto wa pili katika familia yao. Baba yake alikuwa Fundi makenika na mama yake alikuwa muuguzi. Wakati akiigiza alikuwa muumini jina wa kanisa Katoliki.

Brian Deacon alishawahi kuwa katika ndoa yake ya kwanza na Bi.Rula Lenska (1977-1987) na baadaye kuvunjika ambapo alifanikiwa kuzaa naye mtoto wa kike aitwaye Lara

Deacon. Pamoja na hayo aliamua kufunga ndoa yake ya Pili na Bi. Natalie Bloch mnamo mwaka 1998 na mpaka sasa wapo kwenye ndoa hiyo.

Hata hivyo Bwana Brian Deacon alishawahi kushiriki filamu kama A Zed &Two Nougats ya mwaka 1985,The Feathered Serpent ya mwaka 1976-1978 na Tamthilia iitwayo kwa jina la Lillie iliyoigizwa mwaka 1978 akitumia jina la Frank Miles katika Tamthilia hiyo. *(Gazeti-Tazama Tanzania ISSN 0856-9193 Toleo Namba 586 Jumanne January 21-27, 2014)*

Kama umeibandika nyumbani kwako picha ya mtu huyo ukidhani ni ya Yesu tafadhali iondoe haraka sanamu hiyo. Usiweke picha ya mwanadamu anayeonekana unapotaka kuuona uso wa Mungu asiyeonekana. Tupilia mbali imani hizo zenye mioyo migumu kama ya farao, Jishushe na unyenyekee mbele za Yule ambae ni Roho, kweli haki na uzima. Maelfu watakutwa wamelala usingizi kama wanawali wale wapumbavu kwa ajili ya udanganyifu huu.

Ikumbukwe kuwa daima kutakuwako na watu wanaojitenga na Mungu siku zote mpaka mwisho wa vita kuu kati ya haki na uovu. Hatuwezi kuwa salama hata kwa dakika moja tusipomtegemea Mungu hasa hasa na maisha yetu yafichike ndani ya Kristo kukesha katika sala ndiyo salama yetu ya kukaa katika hali ya usafi. Kwa mambo hayo tunaonywa wazi kuwa usalama wetu vijana kwa wazee ni kukesha katika sala tu na kujiepusha na ibada yoyote ile ya kisanamu ili tubaki upande wa Mungu na kusimama tukiwa salama siku ya kupimwa ambapo wengi watakapopimwa wataonekana wamepungua.

"Basi wanangu, nisikilizeni sasa, maana heri hao wazishikao amri zangu sikieni mafundisho mpate hekima wala msiikatae, ana heri mtu yule anisikilizae. Akisubiri siku zote malangoni pangu akingoja penye vizingiti vya milango yangu. Maana yeye anionaye mimi aona uzima naye atapata kibali kwa BWANA. Bali anikosaye hujidhuru nafsi yake, nao wanichukiao hupenda mauti; *(Mithali 8:32-36.)*

SURA YA KUMI NA MOJA

# CHOMBO CHA SHETANI

Katika wakati huu ambapo giza la kiroho limewafumba watu macho ukristo wa shetani umeinuka juu na bendera yake kupeperushwa sana. Popote lilipo taifa pana bendera pia, Ukristo wa shetani una bendera yake popote shetani anapoabudiwa. Chanzo cha bendera hii ni katika kinywa cha yule mnyama, bendera hii ikaingia hata kwa nabii wa uongo *(Ufunuo 16:13)* bendera hii ndicho chombo cha shetani kinachotambulisha ukristo wake.

Mungu ametoa onyo kali thabiti lisilopingwa na kinywa cha mwanadamu kuwa popote Mungu anapoabudiwa kamwe pasiwepo bendera ya shetani. Milele zote chombo cha shetani hakitakuwa alama ya Ukristo wa kweli. Shetani amekitumia chombo hiki tangu zamani hata kabla ya Kristo kuzaliwa. Wale wanaojidai wakristo wamekipigia debe chombo hiki huku Yesu akionya kuwa hakuna mwenye mwili atakayeokolewa kama ana uhusiano na chombo hiki. Mtego huu utawanasa wazembe wote na wasiojali maandiko ya Mungu matakatifu. Katika siku inayokuja ndipo watakapolia lakini Yesu atawaambia hakika siwajui! *Mathayo 7:21*

Shetani bila aibu alibuni tangu zamani bendera yake kuwa alama ya ukristo kinyume na agizo la Mungu. Ni alama gani hiyo? Ni alama ya msalaba"Hakuna andiko katika biblia linaloonyesha kuwa msalaba ni alama ya ukristo. Mitume hawakuwa na alama au ishara ya msalaba kuonyesha kuwa wao ni wakristo.

Baada ya Kristo kupaa Mbinguni kanisa la kwanza hawakuwa na msalaba wala Kristo hakuagiza mti wa msalaba au nembo wala bendera ya msalaba itumike kama ishara ya ukristo. Kanisa la Mungu limeonywa lisiweke, lisichore, wala kusimika mti wa msalaba. Msalaba kamwe hauna uhusiano na ukristo. Shetani aliutumia msalaba kutesa watu wa Mungu hata kabla ya kuzaliwa kwa Kristo.

Umbo la Msalaba lilikuwa na mwanzo wake katika Kardea ya zamani (Babeli) na lilitumika kuwa mfano na Mungu Tamuzi. Katika nchi hiyo na katika nchi ya jirani ya Misri *(An expository of New Testament Words (London) 1962 E. W. E. Vine Uk. 256*)

Kuabudu Msalaba ilikuwa ni sehemu ya ibada ya Mungu Tamuzi ukiwa katika umbo la T au ya kifimbo ikiwakilisha herufi ya kwanza ya jina lake *(ibid)*. Mungu alimfunulia nabii Ezekieli juu ya ibada ya kumwabudu shetani kupitia Mungu Tamuzi. "Ndipo akanileta mlango wa kuingilia katika nyumba ya BWANA ulioelekea upande wa Kaskazini, Na tazama wanawake wameketi wakimlilia Tamuzi. Akaniambia mwanadamu umeyaona haya? Utaona tena machukizo makubwa kuliko haya akanileta mpaka ua wa ndani wa

nyumba ya BWANA na Tazama Mlangoni Pa hekalu la BWANA kati ya ukumbi na madhabahu walikuwako watu kama ishirini na watano wamelipa kisogo hekalu la BWANA na nyuso zao zimeelekea upande wa Mashariki; nao wanaliabudu jua kuelekea upande wa Mashariki. *Ezekieli 8: 14 – 16*

Historia ya Msalaba inarudi nyuma hata kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Msalaba ulitumika kwa mauaji wakati wa zamani *(Esta 5: 1 – 14)*. Shetani ni muuaji naye alitumia Msalaba kumwaga damu ya mwana wa Mungu. Shetani alikuwa amejidhihirisha mwenyewe kuwa ni Muuaji *Mathayo 27: 27-50, DA761*. Wahalifu waliohusika na kifo cha msalaba iliwapasa kujichukulia msalaba mpaka mahali pa kusulubiwa, kila mara walipobebeshwa misalaba walifurukuta sana na kutaka kujiokoa. *(DA 417.)*

Msalaba ulikuwa ukitumika katika utawala wa Kirumi. *(ibid)* ya shetani hutumia msalaba kama ishara ya matendo yake ya ukatili msalaba ndiyo bendera halisi ya shetani. Shetani alitumia msalaba kumuua mwana wa Mungu. Msalaba ni chombo cha mauaji. Malaika Mbinguni wanashangaa kuona chombo cha shetani kinatumika kama alama ya Ukristo katika madhehebu. Siku chombo hiki kilipotumika na Warumi kumdhalilisha Yesu Mbinguni kulikuwa na mshangao mkuu kuhusu ubaya wa chombo hiki.

"Mbingu iliangalia kwa mshangao Kristo akiwa ametundikwa msalabani, damu ikitirika kutoka katika jeraha za vichwani, mikononi na miguuni. Majeraha yake yaliachama kutokana na uzito wa mwili wake kuning'inia kwa mikono peke yake.*(DA760.)* Warumi walipokuwa wanakuja kuwapiga Wayahudi walikuja wakiwa na misalaba. Hayo yalionekana pia wakati wa kuangamia kwa Yerusalemu.

"Viongozi wa majeshi ya Kirumi walikusudia kutoa kipigo kizito kwa wayahudi ambacho kingewafanya wasalimu amri mara moja. Mateka walipigwa, wakateswa sana na kutundikwa mitini, mbele ya kuta za miji kufuata bonde la Yehoshafati na kuendelea mpaka mlima wa Golgota misalaba mingi sana ambako watu walikuwa wametundikwa ilijazana. Hapakuwa na nafasi ya kupita kati yake". *(GC32)*.

Wayahudi wakati wa Kristo kama ilivyo leo walikuwa wamezikanyaga amri za Mungu lakini kwa juu juu walionekana wacha Mungu wa kweli wakikaza sana amri za Mungu na kuzifanya kuwa mzigo kwa watu. Jinsi Wayahudi walivyokuwa wakidai kwamba wanashika sheria za Mungu, hali kadhalika Warumi hujidai kuwa wanautukuza msalaba. Huweka misalaba kila mahali makanisani, madhabahuni, kwenye mavazi n.k kila mahali huutukuza msalaba kijuu juu tu lakini mafundisho ya Kristo wakiyazika chini na kuyainua mapokeo ya bure ya kibinadamu. *(GC568)*

Manabii wakiwa katika njozi walihuzunika kwa uchungu walipoona chombo hiki cha shetani kikiingia katika nyumba ya Mungu *(IT578)* kupitia kanisa Katoliki adui ameingiza bendera yake katika nyumba ya Mungu. Tumeonywa na Mungu tusiweke kamwe vitu

visivyofaa ambavyo ni kazi ya waliopotoka *(Zaburi 101: 3)* Daudi alimwomba Mungu amgeuze macho yake ili asivitazame vitu visivyofaa *(Zaburi 119: 37)* Tumeonywa na Mungu tusiweke wala kuchora kitu chochote cha Warumi kilichotumika kumuua Yesu. Yatosha tu kuamini kuwa Yesu alikufa. *(CW172)*

Wengine mpaka leo hawaelewi kuwa hata msalaba ule uliotwishwa katika mabega ya Yesu ulikuwa umeandaliwa kwa ajili ya Baraba yule jambazi sugu *(DA741)* Yesu alipoubeba ule msalaba alikuwa katika hatua ya kubeba dhambi zote za ulimwengu akimkomboa na Baraba pia. Katika Biblia Mti wa Msalaba, picha, na alama za msalaba hujulikana kama Sanamu za kuchora na za kuchonga. *Habakuki 2: 18,* Yesu aliposisitiza kuubeba msalaba na kumfuata hakuwa na maana ya kuubeba mti. *"Sasa Yesu aliwaeleza wanafunzi wake kuwa maisha yake ya kujinyima, na ya kimasikini ni kielelezo cha maisha ambayo lazima waishi. Alisema, Mtu yeyote akitaka kunifuata lazima ajikane nafsi ajitwike msalaba wake kila siku anifuate"(DA 416)*

Shetani amepotosha walimwengu kuwa kuubeba msalaba ni kuubeba mti. Ikiwa kuubeba msalaba ni kuubeba mti, basi uwepo na mkuki uliomchoma Yesu, basi na iwepo pia taji ya miiba iliyopigiliwa kichwani. Maana Yesu hakufa kwa maumivu ya kuubeba mti peke yake, na iwepo misumari ile iliyopigiliwa ili kukamilisha huduma aliyoitoa Kristo pale msalabani. Ilikuwepo siki aliyonyweshwa ambapo aliitema alipoionja. Kama ni hivyo na liwepo na vazi lililopigiwa kura. Je hiyo ndiyo maana halisi ya kuubeba msalaba? La hasha; Yesu hakufundisha tufanye hivyo.

Lipo dhehebu mama lenye historia mbaya ya mauaji. Historia yaonyesha jinsi dhehebu hili lilivyoua wengi nyakati zilizopita. Mwaka 538 AD zaidi ya watu Milioni hamsini waliuawa na kanisa hili; Hili ndilo kipenzi cha shetani, nalo limepewa msalaba kama bendera kuashiria jinsi lilivyo, siku si nyingi zilizopita limezungusha bendera hii dunia nzima.

Waumini wa dhehebu hilo wanapokufa huwekewa bendera hii juu ya makaburi bila kujua wakidhani ni alama ya kuonyesha wanavyomjali Kristo. Wengi wataelewa udanganyifu huo wa shetani wakiwa wamechelewa. Mipango imeandaliwa na dhehebu hilo kwa ajili ya kuua wote watakaokaidi wakati mpinga Kristo atakapotawala dunia yote muda mfupi ujao. Hili ndilo dhehebu pekee lililopewa mamlaka ya joka kupeperusha alama hiyo ya mauaji bila aibu.

Mungu ametuonya juu ya haya ili tuyaache, Wala tusijifanyizie miungu ya kuyeyusha *(Kutoka 34:17)* Tusichore wala kuchonga sanamu *(Habakuki 2: 18)* wala tusijisimamishie mnara ili kuuabudu *(Mambo ya Walawi 26: 1)* Mungu ameonya tujitenge na uovu *(2 Wakorintho 6: 14 – 16)* kwa hiyo nendeni zenu nendeni zenu tokeni huko msiguse kitu kichafu tokeni kati yake iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya BWANA *(Isaya 52:11)* Maana Mungu wako amekuchagua kuwa watu wake hasa *(Kumbukumbu la Torati. 14:2, Zaburi 132: 13)*

Mtu mwenye busara na Roho ya huruma kamwe hataangalia mtu akiteswa na kudhalilishwa kama Yesu bila kuhuzunika. Tendo la ukatili lililofanyika pale msalabani ni uthibitisho wa ukatili wa shetani. Kamwe matendo ya kikatili hayatakuwa alama ya Ukristo milele. Kuna raha gani kuangalia tukio la kutisha ambalo Mbingu zilipoliona zilishangaa? Kadri unavyoweka chombo cha ukatili katika nyumba yako ile huruma ya Mungu inapotea. Hii ni sheria ya akili za mwanadamu kwamba kwa kutazama, tunabadilishwa. *(PP91)*

Lipo kabila moja Mkoa wa Rukwa ambalo baadhi ya watu wake huabudu mizimu na kujihusisha na uchawi. Wakati wanapofanya matambiko kwa ajili ya kutimiza malengo yao, huwa wanabeba msalaba pia. Kwao msalaba ni moja ya nyenzo muhimu ili kukamilisha huduma zao za Kipagani ambazo Mungu hazikubali. Ndugu zangu wakristo huu ni uthibitisho tosha kuwa hiki ni chombo cha shetani.

Ni kosa kwa kanisa kuwakilishwa na alama ya shetani, Ni fedheha kwa malaika wanapokuta chombo cha uchungu kilichotumika kumuua Yesu kikiwa nyumbani kwako. Iweje uache bendera takatifu na badala yake ukatundika picha na alama zilizotumika kumuua Yesu?. Kuna uhusiano gani kati ya Mtu wa Mungu na Matendo ya Shetani?. Je mtu wa Mungu uambatane na sanamu? Iweje maisha yako matakatifu yachafuliwe na kazi potofu za shetani? Je ni halali kuweka au kuona kazi potofu za waliopotoka?

*"Sitaweka mbele ya macho yangu neno la uovu kazi yao waliopotoka naichukia, haitaambatana nami, moyo wa ukaidi utaondoka kwangu. Lililo ovu sitalijua (Zaburi 101: 3 – 4.) Unigeuze macho yangu nisivitazame visivyofaa, unihuishe katika njia yako" (Zaburi 119: 37)*

Wale waliohusika kumuua Kristo, ambao waliwaua watakatifu pia karne zilizopita, ambao wanajiandaaa kuja kuua tena watakatifu kipindi kifupi kijacho, ndiyo hao hao wanaotembea wakiwa na mavazi yenye misalaba huku wakiibusu sana kwa huruma kana kwamba wana utii wa kweli kwa Mungu. Ndio hao hao wauaji wakiwa na bendera yao ile ile ya mauaji. Sasa wameficha makucha yao lakini punde watayatoa hadharani maana ni walewale na bendera yao ileile.

Wakristo wa leo wamekubaliana na dini za makafiri kinyume na biblia *(Yoshua 23: 7)* wameweka alama za misalaba ambayo ni chombo cha shetani, wengine wamechora alama hizi katika vitabu vitakatifu kinyume na Mungu alivyoagiza. Wengi wametumia alama hii ya Kipagani na kumfukuza Kristo kwa kuiweka katika nyumba za ibada. Laiti kama ungelijua mambo yapasayo amani yako, kamwe bendera za Warumi zisingepepea juu ya kuta zako!. Kutoka kwako njiwa wa amani Mngeruka kuyaendea mataifa yote, ungekuwa Taji ya Utukufu wa Ulimwengu *(DA577)* Lakini hayo yamefichwa machoni pako kupitia mbwa mwitu wakali wanaotawala dini wakifukuza kondoo wa Mungu na kuwaacha wakitangatanga milimani.

Wewe uliyependwa na Mungu kama Israeli ya kale, utakumbuka uasi wako wakati utakapokuwa umechelewa mno kuokolewa! Kwa maana umejifunua nafsi yako kwa ajili ya mwingine, si kwa ajili yangu, ukakwea juu, umekipanua kitanda chako nawe umefanya maagano na hao, ulikipenda kitanda chao hapo ulipokiona. *(Isaya57:8.)* Jinsi jua litakavyopita juu yako usiyetaka kutubu na kugeuka, likielekea upande wa Magharibi, ndivyo utakavyopotea kwa umilele.Wakati wino wa nuru hii ukipita katika macho yako, nafasi ya mwisho ya kutubu bado ipo.Usikubali kulala na watu wa Babeli katika kitanda cha mapenzi.

Na watu wa Babeli wakamwendea katika kitanda cha mapenzi, wakamtia unajisi kwa uzinzi wao, akatiwa unajisi nao kisha roho ikafarakana nao. Basi alifunua uzinzi wake na kufunua uchi wake ndipo roho yangu ikafarakana naye (*Ezekieli23:17–18)* Maana huyo Mtesi amenyosha mkono wake juu ya matamaniko yake yote, maana ameona ya kuwa makafiri wameingia ndani ya patakatifu pake, ambao kwa habari zao wewe uliamuru wasiingie katika kusanyiko lako. *(Maombolezo 1: 10)*

"Nilimuona muelekezaji wetu akielekeza kwenye mavazi ya wale walioitwa wenye haki akiwaweka utupu, akiuweka wazi uchafu uliokuwa ndani. Ndipo akaniambia, huwezi kuona walivyofanya kuficha uchafu na uozo wao wa tabia? Ni jinsi gani mji uliokuwa mtiifu umekuwa Kahaba? Nyumba ya baba yangu imefanywa nyumba ya biashara, mahali ambapo uwepo wa Mungu umetoweka. Kwa sababu hii kuna udhaifu, upungufu na nguvu. *(8T250)*

Muda usingetosha kueleza juu ya upagani wa kuweka msalaba kwenye kaburi pindi mtu afapo. Daima kutakuwepo na watu wanaojitenga na Mungu siku zote mpaka mwisho wa dunia. Hao wataifanya kazi ya shetani kwa uaminifu wataweka bendera ya shetani katika madhehebu, makaburi na katika nyumba zao kama alama ya ukristo wa shetani.

Waanzilishi wa uovu huu wanayajua yote haya na ubaya wake, nao watahukumiwa kwa kuwaficha ukweli kondoo wao. Hao ni vipofu wapendao usingizi na kuota ndoto. Ni mbwa bubu wenye choyo sana, wala hawashibi kamwe. Na hao ni wachungaji wasioweza kufahamu neno, wote pia wamegeuka upande wazifuate njia zao wenyewe kila mmoja kwa faida yake toka pande zote. *(Isaya 56: 10 – 11)*

SURA YA KUMI NA MBILI

# SHETANI NA MAITI

Na wakati watakapokuambia, tafuta habari kwa watu wenye pepo na kwa wachawi, waliao kama ndege na kunong'ona, je haiwapasi watu kutafuta habari za Mungu wao? Je waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai? *(Isaya 8:19)*

Kwa maana linalowatukia wanadamu, linawatukia wanyama, jambo moja lawatukia, anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu naam wote wanayo pumzi moja wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama kwa maana yote ni ubatili., wote huenda mahali pamoja wote hutoka katika mavumbi na hata mavumbini hurudi tena. *(Mhubiri 3:19-20)*

Kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa lakini wafu hawajui neno lolote wala hawana ijara tena maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Mapenzi yao na machukio yao na husuda yao imepotea yote pamoja wala hawana jambo lolote linalofanyika chini ya jua. *(Mhubiri 9:5-6)* Pumzi yake hutoka huurudia udongo siku hiyo mawazo yake yapotea. *(Zaburi 146:4)*

Upo msingi uliojengwa na shetani kuhusu hali ya mtu aliyekufa. Uongo wa shetani pia unahusika na maiti, watu wengi huogopa maiti na kuiheshimu sana kuliko hata mtu aliye ha.  Kupitia uongo huo shetani amedumisha uongo juu ya kutokufa kwa roho. Ingawa Biblia inaeleza wazi kuhusu hali ya mtu aliyekufa lakini ni wachache kiasi gani leo wanaojali ukweli huo? Wengi hushughulika na uongo wa shetani wakitumia akili zao, muda na mali zao.

Tunaishi katika wakati wa Biblia kutokusadikiwa. Watu huvutwa kuamini uongo bila kupeleleza ukweli wa kila walichoamini. Wengi wanamwabudu shetani wakati wa msiba bila kujua Biblia imeeleza wazi kuhusu hali ya wafu lakini wengi hawaelewi ukweli huu.

Je! mwanandamu anapokufa huenda wapi? "kwa jasho la uso wako utakula chakula hata utakaporudia ardhi ambayo katika hiyo ulitwaliwa, kwa maana u mavumbi wewe nawe mavumbini utarudi. *(Mwanzo 3:19)*

Je! Wafu hulala wapi?

"Tena wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele. *(Danieli 12:2)*

“Vivyo hivyo mwanadamu hulala chini asiinuke hata wakati wa Mbingu kutokuwako tena hawataamka wala kuamshwa usingizini. *(Ayubu 14: 1)* Mbingu zitatoweka wakati wa kuja kwa Yesu *(Ufunuo6:14)* Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko wa sauti ya malaika Mkuu na parapanda ya Mungu nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. *(IWathesalonike 4:16)*

Tumaini liko wazi kwa wale waliolala katika Kristo kwani kwao kuna ufufuo kwa ajili ya uzima wa milele. Msistaajabie maneno haya maana saa yaja ambayo watu wote walio makaburini wataisikia sauti yake, nao watatoka wale waliofanya mema kwa uzima nao waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu Amini Amini nawambia saa inakuja na saa ipo wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu na wale waisikiao watakuwa hai. *(Yohana 5: 25,28)*

Shetani alisema watu hawatakufa bali wataongezeka hekima *(Mwanzo 3: 4-5)* kwa miaka mingi upagani uliojengwa katika imani juu ya waliokufa kuwa hawafi umejengwa kwa wale wasio mwamini Mungu na hata wanaojidai kumwamini Mungu. Wengi wamepotoshwa kuwa waliokufa wanakwenda mbinguni, wengine wanapitia mahali pa utakaso kwanza ndio waingie mbinguni. Kwa sababu hiyo maiti ya aliyekufa imeheshimiwa sana na kuhudumiwa kuliko wakati alipokuwa hai. Upendo wa wengi unapoa lakini haujapoa kwa maiti. Ni katika msiba ambapo mtu anatoa mchango wake kwa hiari.

Gharama kubwa inatumika kumrudisha aliyekufa udongoni. Pesa ambazo zingetumika kusaidia yatima wanaobaki hupotea kwa matumizi yasiyo lazima wakati wa msiba. Wengi wameanza kushona sare maalum za msiba. Ni rahisi kukopeshwa pesa kwa ajili ya kusafirisha maiti kuliko kukopeshwa pesa kwa ajili ya kumtibia mgonjwa. Wajane na yatima hukabiliwa na deni kubwa lililokopwa ili kusafirishia mzoga ambao maandiko matakatifu yalionya kuwa maiti ni najisi. Mtu akifa mwili wake ni najisi tangu agano la kale.

Desturi nyingi za kuzika haziko katika biblia. Kitendo cha wengi kuiogopa maiti na kuiheshimu kuliko hata mgonjwa kimefanya wengi kuiga hata mila za kipagani. Ni vigumu kuanzisha chama cha tiba na uhai lakini ni rahisi kiasi gani kuanzisha chama cha kufa na kuzikana? Shetani ameuhamisha upendo kutoka kwa walio hai na kuuelekeza kwenye maiti. Wakati wa msiba ni vigumu kumsujudia Mungu lakini ni rahisi kuinamia maiti kwa ajili ya heshima zinazodaiwa kuwa ni za mwisho. Hakuna heshima za mwisho ambazo maiti hupokea. Katika biblia kuheshimu kitu kisicho na uhai na kukiinamia ni Ibada ya sanamu.

| MGONJWA | MAITI |
|---|---|
| Ni vigumu kumchangia atibiwe | Ni rahisi kumchangia akazikwe |
| Hapewi heshima maalum | Anapewa heshima za mwisho |
| Hana chama cha Tiba na Uhai | Kuna chama cha kufa na kuzikana |
| Wengi hawamuogopi mgonjwa | Wengi huogopa maiti |
| Ni vigumu kumtia moyo apone | Ni rahisi kumsifu akifa |
| Ndugu huchelewa kumtibu | Ndugu hufika haraka kumzika |

Jambazi ambaye hudharauliwa hata na watoto wadogo wakati anapozikwa naye hupewa heshima yake ya mwisho. Ni rahisi maiti kujengewa kaburi zuri, hata kama ndani imebaki mifupa lakini ni vigumu yatima waliobaki kujengewa hata nyumba ya makuti.

Matendo haya yanafanywa na watu wanajidai kumpenda Mungu na kuzishika amri zake. Hawa wanajitayarisha kuja kukataliwa na Yesu atakaporudi. Mambo haya ya kipagani yamekatazwa katika biblia. Mwanzo wa upagani huu ulianzia zamani katika nchi za mbali kule ambako ustaarabu ulianzia. Historia ya Wamisri katika huduma za mazishi imeeleza hivi:-

“Wamisri wa kale waliamini kuwa wangekuwa na maisha ya raha baada ya kufa. Imani hii wakati mwingine ilipelekea matayarisho yaliyovuka mpaka kwa ajili ya mauti na maziko. Kwa mfano ilipelekea wafalme na malikia kujengewa piramidi na makaburi makubwa. Wamisri wengine wa kawaida walikuwa na makaburi madogo tu ya kawaida.

Wamisri waliamini kuwa miili ya waliokufa ni lazima itunzwe kwa ajili ya maisha ya baadaye, waliipaka maiti mumiani ili isioze wakiifunika maiti hiyo kwa kitani na kuiweka katika jeneza. Baadhi ya mumiani za kimisri zingalipo hata leo. Wamisri walijaza vitu vingi katika kaburi kwa ajili ya maisha ya baadaye ya maiti. Vitu hivi ni pamoja na nguo, wigs, vyakula, vipodozi na vitu vya thamani. Makaburi ya matajiri wa Kimisri yalizikwa pamoja na mtumishi ambaye angewahudumia katika ulimwengu huo.*(World Book Encyclopedia, Volume 6 Uk. 137-138)*

Wakati wana wa Israel wanatoka Misri kwenda katika nchi ya Kaanani Mungu aliwaonya wasiige desturi hizo mbaya. Nchi hii ya Misri ndiyo ambako kulikuwa na desturi hizi mbaya za huduma za mazishi na upagani mwingine ambao hauruhusiwi katika biblia. Lakini wao walikaidi wakaiga mila hizo za kipagani, pia waliiga desturi mbaya za sherehe, harusi na anasa haramu. Mungu aliwaonya wajiepushe na mila hizo ili wadumu kuwa safi *(Kumbukumbu la Torati. 7:2)* Shetani anajitahidi kuufumba ulimwengu kwa hila ili kuupotosha.

“Wanadamu wamegundua mila kuelezea huzuni, faraja kwa wafiwa na pia kuheshimu maiti. Kwa wengi kifo huonyesha hatua ambayo mtu anapiga kutoka maisha haya kuingia maisha mengine. Karibu dini zote huamini hivyo. Ushahidi huonekana katika maneno yanayozungumzwa wakati wa mazishi na namna mazishi haya yanavyofanywa. Watu wanapokesha katika msiba wana imani kuwa wanafariji roho ya marehemu na pepo wabaya. Desturi ya kukausha maiti kwa kuweka dawa ya manukato ili isioze ilifanywa na Wamisri wakiamini kuwa siku moja roho ya marehemu itarudi katika mwili, hivyo ilikuwa muhimu kutunza mwili huu ili kuzuia roho yake isipotee” *(World Book Volume 7 UK 557-558)*

Mpango wa shetani wa mwisho ni kuhakikisha kuwa mazishi yanageuka kuwa ibada ya sanamu popote yatakapofanyika. Tayari makaburi ambayo ndani kuna mifupa yameanza kuwa na misalaba juu yake ambayo ni alama ya mamlaka ya shetani.. Hatutaelezea upagani wa kuweka shada kwenye kaburi la maiti. Hakuna aliyeweka shada la maua kwenye kaburi la Yesu. Kuna hila za shetani katika tukio hili kila linapofanyika. Watu hawajiulizi kwa nini mishumaa inawashwa kwenye keki ya arusi mchana wakati mwanga upo. Wale wanaotaka kuonyesha upendo onyesheni wakati mtu akiwa hai, kinyume chake ni upagani.

“Mariamu aliamua kuonyesha upendo wake kwa Yesu kwa tendo la kumiminia mafuta ya thamani kubwa. Kristo alikubali na kusema amemwandaa kwa mazishi. Yusufu wa Arimathaya na Nikodemo walipata hasara walipokwenda na manukato kwenda kuipaka maiti ya Yesu. Hata hivyo hawakumkuta.

Mariamu alifanya hivyo wakati Yesu akiwa hai. Ni hasara kiasi gani wanayopata wengi wanapotumia gharama kubwa ili kuonyesha upendo wao kwa ndugu zao wakiwa wamekufa? Zawadi zinazotolewa, maneno yanayosemwa yangekuwa na faida kiasi gani kama yangetolewa kwa mhusika wakati akiwa hai?” *(DA560)*

Desturi nyingi za Kiyahudi hazikutoka katika neno la Mungu. Yesu alipokuja alizipinga ili watu waziache. Walikumbushwa kutoiga desturi za makafiri kwani kuiga njia za mataifa ni machukizo. *(Yeremia 10:2)* Kuosha maiti kulifanywa na watu mbalimbali katika dunia. Kwa Wayahudi wao waliamini ni kutakasa maiti *(S.D.A Bible Commentary Volume 6 Ukurasa 242)* hata hivyo hakuna utakaso wa kiroho kwa kuosha maiti.

Kupeleka maiti kanisani ni upagani wa wazi ambao shetani anauthamini. Kanisa ni takatifu. Miongoni mwa vitu vinavyotia unajisi nyumba ya Mungu ni maiti. Maiti ni najisi tangu zamani za kale. *Hesabu19: 11-13.* mahali patakatifu hapawezi kupelekwa mzoga wa mbwa au nguruwe. Tumeelezwa kuwa wakati wa kufa mwanadamu hana kitu chochote cha kumpita mnyama. *(Mhubiri 3: 19-20)*

Maiti ya Yohana alipokufa haikupelekwa kanisani. Maiti za Musa, Haruni na Petro hazikupelekwa kanisani walipokufa. Wengi wamedanganyika hapa na ukristo wa shetani katika makanisa yao. Wamesahau kwamba hata Yesu mwenyewe ambaye ndiye mwenyewe wa ukweli na uzima na haki na njia ya kutupeleka mbinguni, Siku alipokufa maiti haikupelekwa kanisani wala msikitini kwani Wayahudi waliijua Torati kuwa wangeitia unajisi maskani ya Bwana. Lakini maiti zingali zinapelekwa kanisani. Mungu hakai mahali paliponajisiwa *(Rejea sura ya nne ya kitabu hiki)* Kupeleka maiti mahali patakatifu ni tendo la kumchukiza Mungu.

Kuhusu mazishi ya (Haruni) yule kuhani Mkuu maandiko yameeleza kifupi tu "Haruni akafa akazikwa huko" *(Kumbukumbu la Torati 10:6)* Tofauti kubwa leo ambapo kuna uharibifu wa mali. Huduma ya mazishi na harusi vitapoteza wengi wasimuone Yesu ajapo. "Haruni alipokufa alizikwa na rafiki zake wawili walioshuhudia kifo chake. Kaburi lake limefichwa hadi leo. Mungu hapewi heshima katika mazishi yetu kwa gharama inayotumika kwa mazishi na maiti yenyewe inaporudishwa katika udongo"(PP427)

Leo mazishi ni sherehe kubwa ambapo wafiwa hushona sare huku maiti ikizikwa pamoja na vitu vya thamani, kuna wimbi la watu maskini wanaohitaji msaada. Yesu alipoona maovu haya aliyakemea. Nabii aliandika hivi:"Wakati wa Kristo gharama ilitumika kujengea makaburi na kuyapamba. Mbele ya Mungu hii ilikuwa ni Ibada ya sanamu. Katika kushughulika na wafu wanadamu huonyesha ni jinsi gani wasivyompenda Mungu na majirani zao wenyewe. Watu wana hatia ya kusahau wajane, wagonjwa ili kujenga makaburi ya gharama kwa ajili ya ndugu zao. Muda, fedha na nguvu hutumika ovyo kwa kazi hii huku wajibu tuliopewa na Yesu ukiachwa bila kufanyika. Hili ni lazima liwe fundisho kwetu. Macho yetu yafunguke ili tuone nguvu za shetani zilizotundanganya na kutugeuza katika nuru ya ukweli"*(DA618)*

Watu wanaopeleka maiti kanisani wanatumia maandiko vibaya wanapomsomea maiti *(Ayubu14:2)* kwa kumuaga wakati yeye hana habari. Inapofikia kwa matendo hufanywa kinyume. Maiti ya mtu mashuhuri kupewa hadhi tofauti na maiti ya mtu wa kawaida. Hii nayo ni Ibada ya sanamu. Yale yanayofanyika kwa viongozi wa serikali na wengine yameingizwa katika madhehebu pia.

Maiti ya mpagani haiingizwi kanisani lakini maiti ya mshiriki ambaye jina lake lipo katika ushirika (Hata kama alikwisha kuasi) inapelekwa kanisani. Mchungaji aliyewekewa mikono maiti yake inabebwa na wachungaji waliowekewa mikono. Mapokeo haya ya kipagani yamepewa baraka na madhehebu mengi. Yesu anapoyaangalia anatutazama kwa huruma. Ajabu inakuja tena watu wanapoingiza maiti kanisani halafu huanza tena kuipiga picha. Kweli nyumba ya Mungu imefanywa pango la biashara!

Wale wanaojificha kwenye kichaka cha (Dorka) thabitha hawaelewi kwa nini maiti yake ilioshwa. Imani ya kumwosha Thabitha haikuwa kumzika.

Mtu yeyote angeweza kufanya mazishi ya Thabitha, haikuwa lazima awe Petro. Huenda walifanya hivyo ili awe safi kabla ya kumuita Petro. Huenda pia walifanya hivyo kulingana na desturi zao za kutakasa maiti lakini katika N eno la Mungu hakuna agizo hilo la kuosha maiti. Desturi za kuzika katika jeneza zilifanywa na Wamisri*(Mwanzo50:26)* Waebrania hawakuwa na uzoefu wa kuzika wafu katika sanduku tangu kale. *(SDA Bible Dictionary Ukurasa 167, 230)*

"Yusufu alipowaambia ndugu zake kubeba mifupa yake watakapotolewa Misri na Mungu alitaka kuwakumbusha kwamba walikuwa wageni katika nchi ya Misri nao walipaswa kuweka tumaini lao katika nchi ya ahadi kwani wakati huo ingekuja kwa uhakika.*(PP240)*. Wengine wametumia kisa hiki ambacho kwetu leo ni mfano wa safari yetu ya kule tunakoenda (Kaanani ya mbinguni)

Kwa ajili ya upagani wa kuosha maiti ilibidi ifunguliwe ofisi ya Mashemasi wa kike. Kuwa na mashemasi wa kike mahali patakatifu ni chukizo kwa Mungu. Hakuna fungu katika maandiko matakatifu wanawake walipochaguliwa kuwa mashemasi. Pamoja na kazi zingine mashemasi hawa wa kike kazi zao ni kuosha maiti. Mbele za wanadamu hili ni tendo jema lakini machoni pa Mungu huu ni uasi. Katika 1 Timotheo 3 na Matendo 6 mashemasi wa kiume tu ndiyo waliochaguliwa. Hata Fibi hakuwa shemasi. Ellen G White alipoonyeshwa njozi akimwona Fibi aliandika hivi:-

*Fibi alikuwa na karama ya ukarimu akawahudumia wageni waliohitaji msaada (6T. 341, 2TT 570)*

Ukarimu ni kipawa sio ofisi. Paulo mtume anasisitiza kuwa mashemasi wawe ni wanaume wa mke mmoja *(1 Timotheo 3)* Ukristo kwa shetani wa kuwa na mashemasi wa kike umevuka mpaka ambapo sasa kuna wazee wa kanisa wa kike na wachungaji wa kike. Tulisubiri kuona siku moja Maaskofu wa kike na tayari haya nyanatokea. Haya yanafanyika kwa kuwa wachungaji wa mishahara wamewapotezea kondoo wa Mungu milimani.

Siku zote wajane ni wanawake mashemasi waliochaguliwa katika matendo 6 walikuwa na kazi ya kuhudumia wajane lakini hawakuchaguliwa mashemasi wa kike pamoja na kwamba wajane ni wanawake. Mtume Paulo anamweleza Tito kuwa wanawake wazee wawasaidie wanawake vijana kuwapenda waume zao. Na watoto wao kuwa safi na kufanya kazi nyumbani ili jina la Mungu lisitukanwe. *(Tito 2:3-5.*

Mila na desturi za kuzikana ambazo si halali zimeingizwa kanisani zikawa ni sehemu ya ukristo. Kanisa la Rumi halikuweza kugeuza sabato ya Mungu mpaka kwanza limeikataa torati ndipo ikawa ni rahisi kuigeuza sabato toka Jumamosi kwenda Jumapili. Ndivyo

ilivyo hata leo. Kuikataa torati kumefanya watu kupotea njia hata wasijue wako kwenye meli ambayo inakwenda kasi kugonga mwamba.

Moja kati ya wanafunzi wa Yesu alipofiwa na baba yake Yesu alimzuia asiende kumzika, alimwambia waache waliokufa kiroho wawazike waliokufa kimwili. wapagani wa leo mgekuwepo maneno haya yalipotamkwa mngesema, Yesu hajui kufiwa lakini Yesu aliongea kile alichomaanisha akiona kwa wazi jinsi shetani anavyotawala huduma za mazishi. Aliongea kauli akiwa na lengo na nia takatifu ya kumkomboa mwanadamu.

Maandiko haya matakatifu ndiyo yatakayoamua hatima yako kwa umilele. Tupo mbali kiroho na pale tulipopaswa kuwa. Dalili zinaonyesha wazi kile shetani anachokitaka katika makanisa. Karani wa shetani sasa yuko ofisini akifanya kazi kwa bidii. Ujumbe huu ni moja ya maadui wakubwa wa shetani na hakuna wakala wa shetani atakayeuona asiupige vita. Hata hivyo hakuna atakayepingana na Mungu akafanikiwa.

Tunazikaribia nyakati zile za dhoruba. Kila msimamo wa imani yetu lazima uchunguzwe. Tunapaswa kuwa wanafunzi wazuri wa biblia. Jifunzeni biblia zenu kwa namna ambayo hamjapata kamwe kujifunza siku za nyuma, maana madanganyifu ni makubwa duniani. Ulimwengu wote upo kinyume nasi makanisa yale yanayopendwa sana yapo kinyume nasi.

Sheria za nchi hivi punde zitakuwa kinyume nasi. Kama ulipata kuwako wakati ambapo watu wa Mungu wangeshikamana kwa karibu na kujifunza ukweli juu ya madanganyiko ya shetani ni sasa. Nawataadharisha kwa uchungu mwingi ya kuwa shule nyingi pamoja na vyuo vikubwa vya dini vimekuwa malango ya jehanamu kwa kufundisha mafundisho ya kuzimu ambayo ni mienge ya kijehanamu. Katika majira ya usiku maneno haya yalinenwa kwangu-

*"Waagize Walimu katika Shule zetu*
*kuwatayarisha Wanafunzi wetu kwa kile*
*kinachoujia Ulimwengu" (FE526,527)*

SURA YA KUMI NA TATU

# UCHAWI KANISANI

Mwanadamu umepewa onyo litakalokuepusha na madanganyifu ya shetani: mwanadamu unapaswa kulinda imani yako asije mwovu akakupotosha kupitia miujiza yake ya uongo. Roho ya miujiza imeenea kila mahali ili kuuhadaa ulimwengu. Ni juu yako kufuata neno la Mungu ili uokolewe. Mungu asema nimekuwekea uzima na mauti; baraka na laana, basi chagua uzima ili uwe hai wewe na uzao wako.(*Kumbukumbu la Torati30:19-20)*

## HISTORIA FUPI YA MIUJIZA YA SHETANI

Muujiza wa kwanza wa shetani aliufanya katika bustani ya Edeni ili amnase Hawa. Shetani alizungumza na Hawa akiwa amevaa umbo la nyoka. *(Mwanzo 3:1-5)* Shetani alidhihirisha udanganyifu wake kule Misri aliposhindana na Musa na Haruni waliokuwa wametumwa na Mungu akiwatumia wachawi na waganga. Pale Mungu alipofanya miujiza na shetani alijitahidi ili afanye miujiza hiyo ingawa mingine alishindwa. Miujiza ifuatayo ilifanywa kule Misri na waganga wakaigiza .

| MUSA NA HARUNI | MIUJIZA YA WACHAWI |
|---|---|
| Waligeuza fimbo kuwa nyoka. *Kutoka 7:10* | Waligeuza lakini fimbo ya Haruni ikazimeza fimbo zao. *Kutoka.7:12* |
| Waligeuza maji kuwa damu. *Kutoka 7:20* | Walifanya mfano wa hayo. *Kutoka 7:22* |
| Walileta vyura katika nchi ya Misri. *Kutoka 8:6* | Waganga pia walifanya mfano wa hayo. *Kutoka 8:7* |
| Waligeuza Mavumbi kuwa chawa. *Kutoka 8:17* | Waganga hawakuweza. *Kutoka 8:18* |
| Waliletwa mainzi. *Kutoka 8:24* | Farao alifanya moyo kuwa mgumu. *Kutoka 8:32* |
| Waligeuza majivu kuwa majipu. *Kutoka 9:10* | Waganga hawakuweza. *Kutoka 9:11* |

Shetani aliendeleza miujiza yake kwa kutumia uganga na uchawi wake. Wakati Sauli alipomwasi Mungu na kutamani amwone Samweli ili aweze kupata habari, naye alimwendea mwanamke mwenye  pepo wa utambuzi ili ambashirie "Ndipo yule mwanamke aliposema, je ni nani nitakayekupandishia? Naye akasema nipandishie Samweli *(1Samweli 28:11)*Udanganyifu huu ulipelekea pepo kuvaa sura ya Samweli ili kumhadaa Sauli. Shetani alisujudiwa katika umbo la Samweli. *(1Samweli12:14)*

Siyo vigumu kwa malaika waovu kuigiza mfano wa watakatifu na wadhambi waliokufa, na kufanya maigizo hayo yaonekane machoni pa wanadamu, mambo haya yatakuwa yakiendelea mara nyingi sana, na maigizo ya kushtusha zaidi yataonekana kwa kadri tunavyokaribia kufungwa kwa wakati. *(EV604)*

Shetani hakuchoka bali aliendeleza mapambano mpaka kwenye mlima Karmeli ili kutetea miungu ya Baali, mpaka aliposhindwa. Waliomba miungu yao ya kipagani lakini haikutoa jibu. Wakapiga kelele, wakajikatakata kwa visu na nyembe kama ilivyo desturi yao hata damu ikawachuruzika. Ikawa, wakati wa adhuhuri ulipopita, walitabiri hata wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, lakini hapakuwa na sauti wala aliyejibu wala aliyeangalia. *(1Wafalme.18:28-29*) Mwisho walikamatwa wakachukuliwa ili wauawe huko.*(1Wafalme.18:40)* Ndivyo itakavyokuwa kwa wachungaji wa uongo watakaowatazamisha waumini kwenye miujiza badala ya ukweli.

Na waende kwa sheria na ushuhuda na ikiwa hawasemi sawasawa na neno hili bila shaka kwa hao hapana asubuhi. *(Isaya 8:20)*

"Katika neno imeelezwa kwamba yule adui atafanya kazi yake kupitia mawakala wake waliojitenga na imani nao wataonekana kana kwamba wamefanya miujiza hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje mbele ya wanadamu". *(2SM54*)

Wakati Mfalme Nebukadreza alipoota ndoto akaisahau alitaka kupata tafsiri, ndipo akawaita waganga na wanajimu, wachawi, wasihiri na wakalidayo ili wamtafsirie lakini walishindwa. *(Danieli2:2-4)* Mungu alimfunulia mtumishi wake Danieli ili aitafsiri ndoto. Siku zote Mungu ni mshindi. Kuna kikomo ambacho shetani hawezi kukifikia.

Tunaonywa kwamba katika siku za mwisho shetani atafanya kazi yake kwa kutumia ishara na maajabu. Naye ataendelea na maajabu hayo mpaka mlango wa rehema utakapofungwa ili apate kuwaonyesha ushahidi kuwa yeye ni malaika wa nuru wala siyo wa giza. *(2SM51)*

## RAFIKI WA WACHAWI

Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. (*Mathayo7:15)* Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu, aliye mbinguni; wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe, ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu. *(Mathayo7:21-23)*

Shetani ni rafiki wa wachawi siku zote. Shetani hawezi kutenda miujiza mpaka ameshirikiana na wachawi ili kutimiza azma yake. Wachawi wengi wanafanya kazi za uchungaji katika madhehebu ya dini, wanao uwezo wa kumfanya mtu kuwa mgonjwa na kumwondolea ugonjwa huo kwa miujiza.

Watu wakiwa chini ya uwezo wa roho wachafu watatenda miujiza. Watafanya watu wawe wagonjwa kwa kuwadumaza kwa uchawi na hirizi nao watawaondolea uchawi huo wakiwaongoza watu wengi kusema wale waliokuwa wagonjwa wameponywa kimuujiza. Jambo hili litaongezeka tena na tena. *(2SM53)*

Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. Wala si ajabu maana shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao. *(2Wakorintho11:13-15)*

Wale wanaotenda matendo ya kuponya huelekea kuihalalisha dharau yao ya sheria ya Mungu kwa ajili ya haya maonyesho, na hata kuendelea katika uharibifu. Ingawa wana kila cheo kikubwa si sharti wawe na zile nguvu kuu za Mungu?. Kinyume chake hizo ndizo nguvu za ibilisi. Mtu aligeuzaye sikio lake asiisikie sheria hata sala yake ni chukizo. *(Mithali 28:9.)*

Mtu awaye yote atakayeshika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote. *(Yakobo2:10)* Yule atendaye miujiza huku akikataa amri za Mungu yu mvunja sheria. *(Yohana.14:15)* hutumia kila hila ajuayo, ili awapofushe wanadamu dhidi ya tabia adilifu ya sheria. *(1Yohana2:4)*

Tumeonywa na neno la Mungu kuwa shetani atatenda ishara na maajabu ya uongo katika siku za mwisho.*(Mathayo24:24)* Nao wataendelea kuyaonyesha kama ushuhuda ili waonekane kuwa si manabii wa uongo. Kwa maana wanakiri ya kuwa wanamjua Mungu bali kwa matendo wanamkana; ni wenye machukizo waasi; wala kwa kila tendo jema hawafai. *(Tito1:16)*

Roho Mtakatifu hajidhihirishi kamwe kwa kawaida za namna hiyo wala kwa kelele. Hizo

ndizo hila za shetani; ili afiche mashauri yake.*(1Petro 5:8)* Shetani ana mpango kufuta ukweli kwa wakati huu. Ukweli ulio safi, mnyoofu, mtumainifu, mwadilifu na wenye kutakasa ndiyo unaotakiwa kwa wakati huu. *(Yohana17:1)*

Machafuko na makelele hustusha akili na kupotosha mambo yaliyo mema na mabaya. Nguvu za shetani huchanganyika na kelele na ghasia kuwa sherehe kuu. Haya yote ndiyo wanaita matendo ya Roho Mtakatifu. Matokeo yake ni kwa wale wanaoshiriki uamusho huu wa kuigiza hutumia mawazo ya kuwapoteza. Hawawezi kukumbuka tena mafundisho yake ya Biblia ambayo waliyajua tangu zamani.

Kutakaswa si kitu cha kupapasa papasa, si kazi ya ghafla bali ni kazi ya maisha yote. Kama mtu akijisema ya kuwa Bwana amemtakasa na kumfanya mtakatifu, ushuhuda wa madai yake ya mibaraka hiyo huonekana katika matunda ya upole, uvumilivu, ukweli na upendo.

Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kwanza kinyume cha mafundisho mliyojifunza mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo bali Matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza, waidanganye mioyo ya watu wanyoofu. *(Warumi16:17-18)*

Tunaishi nyakati za hatari ambapo manabii wa shetani wanafanya fitina duniani. Fitina ya manabii wake imo ndani yake, kama simba aungurumaye, akirarua mawindo yake wamekula roho za watu, hutwaa kwa nguvu hazina na vitu vya thamani waongeza hesabu ya wajane ndani yake.

Makuhani wake wamehalifu sheria yangu wameitia unajisi vitu vya kutumiwa sikuzote; wala hawakuwafundisha watu kupambanua vitu vichafu na vilivyo safi nao wamefumba macho yao, wasiziangalie sabato zangu, nami nimetiwa unajisi kati yao. Wakuu wake kati yake wamekuwa kama mbwa-mwitu wakurarua mawindo; ili kumwaga damu, na kurarua roho za watu, wapate faida isiyo halali. Na manabii wake wamewapaka chokaa isiyokorogwa vema, wakiona ubatili maneno ya uongo, wakisema, Bwana Mungu asema hivi iwapo hakusema neno. *(Ezekieli 22:23-28)*

Namna ambayo kwayo Kristo alitenda kazi, ilikuwa ni kulihubiri neno, na kuwapa ahueni wenye kutaabika kwa kufanya miujiza ya uponyaji. Lakini nimeelezwa kuwa hatuwezi kutenda kazi kwa namna hii; kwa maana shetani atatumia uwezo wake kutenda miujiza. Watumishi wa Mungu leo hawawezi kufanya kazi ya Mungu kwa njia ya miujiza, kwa sababu matendo bandia ya uponyaji yanayodaiwa kuwa yametoka mbinguni yatafanywa. *(2SM 54)*

Wengi watayapa kisogo maneno matakatifu na kugeukia miujiza ya shetani, lakini

uongo hautageuka kuwa ukweli kwa sababu wengi wameuamini. Mtategemea miujiza ya uongo hata lini? Mtasitasita kati kati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu mfuateni, bali miujiza ikiwa ndiyo miungu yenu ifuateni hiyo. Leo kama mtasikia sauti yake msifanye migumu mioyo yenu kama wakati wa kukasirisha. *(Waebrania3:15)*

Tutie nanga kwa Kristo, tuweke imara misingi yetu, shetani ana mawakala wake. Huchagua wale wasiokunywa maji yaliyo hai wenye kiu ya vitu vya kigeni na vya ajabu, watu walio wepesi kunywa katika chemchemi yoyote ile njiani. Sauti husikika, Tazama Kristo yupo hapa, au yuko pale. Hebu Sisi tusiziamini sauti hizo.

======================================================================

SURA YA KUMI NA NNE

# MADARAJA YA IMANI

Katika imani kuna madaraja matatu ambapo daraja la tatu ni hatua ya mwisho ya juu ya Kiroho.

*Daraja La Kwanza.Giza La Upagani* Hili ni daraja ambalo Yesu alitukuta tumezama dhambini hatujitambui, tulikuwa wapumbavu *(Zaburi 14*:1) tuliitwa watu wa mataifa ambapo watu wa Mungu walifundishwa wasiige matendo yetu *(Kumbukumbu 7:18-26, 2Wakorintho 6:14-17)*

Watu walioishia daraja hili bila kuingia daraja la Pili ni Farao mfalme wa Misri *(Kutoka 14: 10-30)*Watu wa Sodoma *(Mwanzo 19:1-25)*Yezebeli na Ahabu (*1Wafalme 21:25-26)* Wote watakaokataa kumtii Mungu na kufa kabla ya kuja kwa Yesu mara ya pili. *(2Petro 3:7)* Kanisa la kiyahudi la Mafarisayo na Masadukayo wale walilomkataa Yesu wakataka kumpiga mawe *(Luka 4:28 -29, Yohana 10; 24-31*) Walikua vipofu kanisa lote na Wachungaji wao  (Isaya 56: 10-11) Walikuwa wauaji (*Yohana 12:10)* Kuhani wao mkuu aliidhinisha kifo cha Yesu *(Yohana11:49-51)* Hao wamejaa leo katika Makanisa wakifundisha ubatili.(*Ezekieli 22: 25-28)* Ni wafanyabiashara wa Roho za watu ambao Mungu alishaondoka katika Madhehebu hayo *(Ufunuo 18:9-13, Ezekieli13:4-7, Mathayo 19:23-38)* Kundi hili lote ni mateka wa shetani, Yesu aliagiza kundi hili lote lihubiriwe Injili*(Mathayo 28: 18-20, Marko 16:15-16)* Kwa hiyo kundi la kwanza ni hatua ya kwanza kabisa ya upagani, wengi kabla hawajampokea Yesu walitokea kundi hili lakini kuna wengine waliamini bila kupitia kundi hili la awali.

## DARAJA LA PILI- UANAFUNZI

Daraja la pili linaitwa uanafunzi, Baada ya kuhubiriwa Injili na kumfuata Yesu sasa mtu anakuwa mwanafunzi *(wa Biblia)* akila chakula na kunywa maji na maziwa kutoka katika Maandiko Matakatifu. Anakuwa ni mtoto mchanga wa Imani anayeukulia Wokovu. "kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa ila kwa hayo mpate kuukulia Wokovu"*1Petro2:2*

Hawa wanaitwa wanafunzi (*Marko16:15-16),* siyo wakamilifu wanaanguka na kusimama (*Muhubiri 7*:20) Hawajavumilia hadi mwisho hivyo hawajaokoka (*Mathayo24;13)Imani yao si* moto wala baridi ni uvuguvugu *(Ufunuo3:14-22)* Wanalopenda hawalitendi lakini wanatenda wanalolichukia (*Warumi7:17-20)* Shetani anawatafuta awarudishe kundi la kwanza na Yesu anawaita kwa upole awapeleke kundi la Tatu. Wapo vitani wanapaswa kuvaa *Silaha (Waefeso 6: 10-18)*Wasipojitahidi waingie kundi la Tatu Mungu atawatapika warudi kundi la kwanza (*Ufunuo 3:15)* Bado wamemfungia Yesu nje lakini anawagongea ili aingie *(Ufunuo 3:20*) Hii ni mifano ya watu waliopita katika kundi hili

i. *Petro alimkana Yesu na akatubu (Luka 22:54-62)*
ii. *Daudi alikuwa anaanguka na kusimama (Zaburi 51:10-11)*
iii. *Wakati Musa anamuua mtu na kumfukia kwenye Mchanga alikuwa katika kundi hili (Kutoka2:11-15)*

*Yuda, Anania na Safira* walikufa katika kundi hili na wamepotea milele.Watu wengine wapo katika kundi hili nao wanadhani wako kundi la Tatu kwa hiyo wameridhika, ni hatari kubaki katika kundi hili. Paulo alikuwa katika kundi hili lakini akahamia kundi la tatu. Kuna watu wenye bahati ambao huokolewa katika kundi hili mfano mwivi msalabani, na wale ambao watatubu muda mfupi kabla ya kukutana na mauti ingawa si wengi.

## DARAJA LA TATU- UKRISTO

Ukristo ni kutenda na kutii chochote ulichoagizwa na Kristo bila kujali chochote hata kama kupoteza maisha . Ukristo ni kufanana na Kristo kwa kila kitu (*Mathayo5: 48, Walawi 19: 2, Ufunuo14:2-5, Maombolezo 6: 8-10)* Tangu alipowachagua mitume na miaka yote ya mafundisho yake Wanafunzi wa Yesu hawakuitwa Wakristo mpaka Yesu alipopaa Mbinguni. Yawezeka walikuwa hawajafikia daraja hili mpaka Roho mtakatifu alipowashukia. Baada ya Pentekoste kwa mara ya kwanza waliiitwa Wakristo kule Antiokia *(Matendo 11: 19-26)* Kuanzia hapo walianza kuitwa Wakristo baada ya matendo Imani na shuhuda zao kufanana na Kristo (*Matendo 26:25-29, 1Petro 4:15-16)*

Hili ni daraja la mwisho la juu ambalo wengi hushindwa kufika,si baridi wala vuguvugu ni moto wakiwa na sifa zifuatazo.

- *Hawatendi dhambi kabisa(1Yohana 5:17)*
- *Mwovu hawagusi kabisa(1Yohana 5:19)*
- *Wamepiga vita vizuri vya imani*
- *Wamekuwa kiumbe kipya (2Wakorintho 5:17)*
- *Wanashinda kila kikwazo (2Wakorintho 12:9-10)*
- *Katika safari yao wanayaweza yote (Wafilipi 4:13)*
- *Yesu, Paulo, Petro,Yohana, Eliya, Daniel na Henoko walikuwa katika tabaka hili. Henoko alitembea na Mungu katika daraja hili miaka 300 bila kutenda dhambi mpaka Mbingu zikamchukua.*
- *Mtu anayefika daraja hili ndiye pekee anaitwa Mkristo. Huyu ametoka kwenye ubaridi na uvuguvugu yupo kwenye moto. Mpango wa Yesu kila mtu afikie hapa ili aingie mbinguni.*
  *Mwisho wewe ujiulize mwenyewe katika madaraja haya matatu wewe upo kundi lipi?*

*Swali*: Kama nikiwaambia watu nimeokoka kumbe sijafikia katika kundi hili, pia ni na kasoro, udhaifu na madoa katika tabia yangu je, ninatakiwa nifanye nini?

"*Nayajua matendo yako ya kuwa hu baridi wala hu moto, ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto, basi kwa sababu una uvuguvugu wala hu baridi wala moto nitakutapika utoke katika kinywa changu, kwa kuwa wasema mimi ni tajiri nimejitajirisha wala sina haja ya kitu nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge na mwenye mashaka na masikini na kipofu na uchi, nakupa shauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto upate kuwa tajiri na mavazi meupe upate kuvaa aibu ya uchi wako isionekane na dawa ya macho upate kuona. Wote niwapendao nawakemea na kuwarudi, basi uwe na bidii ukatubu. (Ufunuo3:15-19)*

SURA YA KUMI NA TANO

# MWISHO WA DUNIA

Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya mwanakondoo walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao. *(Mathayo7:15)* Kwa maana watatokea manabii wa uongo nao watatoa ishara kubwa na maajabu wapate kuwapoteza yumkini hata walio wateule. Tazama nimekwisha kuwaonya mbele, Basi wakiwaambia yuko jangwani msitoke, yumo nyumbani msisadiki. *(Mathayo 24:24-26)*

Tutakutana na madai ya uongo, manabii wa uongo watainuka patakuwa na ndoto na njozi za uongo. Mamilioni ya watu wameshadanganywa na mtego wa ibilisi ambao umetegwa katika madhehebu. kama kuna wakati ambao shetani anapendwa sana katika madhehebu wakati huo ni sasa,Hakuna imani tena duniani upendo umekwisha kuanzia ngazi za juu mpaka mtu kwa mtu, uongo umefanya kila dhehebu lionekane ni la kweli huku ukweli wa Biblia ukitupwa chini.

Kiongozi mkubwa wa dini anasimama na Biblia mbele ya waumini na kumkiri shetani kuwa baba yake. Tunaishi wakati wa kutimia kwa unabii uliotabiriwa na Yesu na mitume. Tunatazamia kutokea kwa Kristo mara ya pili. Hatimaye huo mwisho utafika. Ni mwisho wa kila mwenye uhai duniani. Ni wakati ambao Falme na mamlaka za dunia hii zilizojaa uonevu, dhuluma na unyonyaji zitakoma. Huo ndiyo mwisho wa dunia. Je mwisho huo wa dunia utakuwa lini?

HAKUNA AJUAYE

Tunakaribia siku ile kuu ya Mungu. Ishara zinatimia kwa haraka na mfululizo wa matukio unadhihirisha kuwa tupo mwishoni kabisa kuiaga dunia hii. Hata hivyo Bwana kwa hekima alituficha juu ya siku na saa ya kuja kwake. Bwana ametuficha jambo hili kusudi wakati wote tuweze kuwa katika hali ya maandalizi, kwa habari ya siku ile na saa ile hakuna ajuaye hata malaika walio mbinguni ila Baba peke yake. *(Mathayo 24:36)*

Wengine wameweka tarehe na tarehe ilipopita bila mafanikio roho zao hazikutubu bali walirudia kuweka wakati. Lakini mfululizo wa kutofaulu kwao kumewadhihirishia kuwa wao ni manabii wa uongo *(FE335)* maana watu kama hao ni mitume wa uongo watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa Kristo *(2Wakorintho11:13)* Kesheni basi kwa maana hajui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. *(Mathayo 24:42)* Nanyi jiwekeni tayari kwa kuwa katika saa msiyodhani ndipo ajapo Mwana wa Adamu. *(Luka 12:40)*

Angalieni msije mkadanganyika kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu wakisema mimi ndiye tena majira yamekaribia, basi msiwafuate hao. (Luka 21:8) Tarehe kamili ya kuja kwa mwana wa Adamu ni siri ya Mungu *(DA633)*.

Biblia haina tarehe ya kuja kwa Kristo wala mwisho wa dunia. Ni udanganyifu wa shetani kutisha watu kwa kuweka tarehe. Waanzilishi wa mpango huu wanajua lengo lao la makusudi ya kuweka tarehe. Daima patakuwa na miamko ya uongo ya watu washupavu wa dini kanisani wadaio kuongozwa na Mungu watakaopiga mbio kabla hajatumwa nao watatoa siku na tarehe ya matukio ya unabii ambao bado haujatimia, adui anapendezwa kuona wakifanya hivi kwa maana wanapoendelea kutoa tarehe za unabii usiotimizwa husababisha machafuko na kutokuamini *(2SM84)*.

<u>UNYAKUO WA SHETANI</u>

Shetani ni mwerevu sana asomaye maandiko ili kusoma alama za nyakati kwa ajili ya udanganyifu wa kati huu ambapo wengi hawasomi Biblia. Buibui anapomnasa nzi humnyonya damu na kumuacha inzi amekauka kana kwamba yu hai ili awe chambo kwa wengine. Nzi walio hai wanapomuona ametulia humsogelea wakidhani yu hai na huo ndio huwa mwisho wa maisha yao. Hivi ndivyo ilivyo katika madhehebu leo.

Hii ni kauli nzito kuisema lakini lazima ieleweke hivyo. Wengi wanaodhani wanajua kuwa wanajua hawajafikia hata nusu kujua kile shetani anachofanya katika makanisa. Kulikuwepo na watu mashuhuri wenye majina kabla ya gharika. Kulikuwepo na viongozi wa dini maarufu waliojua kuchunga madhehebu, walikuwepo waimbaji maarufu na vituo vya habari za mambo ya dini, yalikuwepo makanisa makubwa ya wakati huo. Lakini kati ya hao hakuna waliookolewa siku gharika iliposhuka. Shetani aliwanyakua wasomi, madaktari, wanasheria, wabunge na mawaziri wote wakawa chakula cha samaki mbele ya hasira za Mungu alipoinyesha mvua kwa siku arobaini. Hii ndiyo njia tunayoiendea.

Wengi watakuwa chakula cha ndege muda mfupi kabla ya mazishi ya shetani. Mazishi ya shetani yataambatana na watu maarufu katika Jehanamu soma *Ufunuo 6:14-17, Yeremia 4:29-31, Isaya 2:11-21, Ufunuo 18:15-24*. Shetani amekamilisha kazi kiasi kwamba madhehebu mengi shetani leo ni baba yao.

Makanisa mengi leo ni maduka ya kuuza makaburi ambapo muumini anapoingia humo anazikwa kiroho, kuna maiti nyingi za walio hai katika madhehebu ambao bado wanadai kumkanyaga shetani wasione wako katika utawala wake kikamilifu. Mafundisho ya uongo yatawaongoza wengi katika mauti ya milele. Kuna uongo wa shetani kuhusu kuja kwa Yesu kuwa Yesu atanyakua kanisa kwa siri, hili ni fundisho lenye roho ya wokovu

wa shetani uliojaa katika  madhehebu.

Yesu hatakuja kwa siri. Tazama yuaja na mawingu na kila jicho litamwona hata wale waliomchoma na kabila zote za dunia wataomboleza kwa ajili yake. *(Ufunuo 1:7)* kwa dakika moja kufumba na kufumbua wakati wa parapanda ya mwisho maana parapanda italia na wafu watafufuliwa wasiwe na uharibifu. *(1Wakorintho16:22)* Kuja kwa Yesu kutaonekana wazi kwa kila mmoja. Ni tukio la wazi ambalo kila mmoja atahusika nalo. *(1Wathesalonike 4 :13-17)*

Biblia inapoandika kuwa Yesu atakuja kama mwivi ina maana kuja kwa Kristo kutakuwa kwa ghafla bila watu kutegemea ambapo wengi watakutwa hawajajiandaa. Ndiyo maana akatufundisha kuwa kesheni ili siku hiyo isiwakute ghafla. Kesheni basi kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu. *(Mathayo 24:42*

Kurudi kwa Kristo kutawaghafilisha waalimu wa uongo, siku ya Mungu itawajia waovu pasipo kutarajia, wakati hali ya maisha inaendelea kuwanyookea wengi, wakati watu wanapozama katika anasa, na shughuli za biashara katika kutengeneza fedha, wakati viongozi wa dini wanatukuza maendeleo ya ulimwengu na maarifa yake wakipumbazwa na hali ya usalama bandia, ndivyo maangamizi yatakavyowajia ghafla wazembe na waovu nao hawataokoka. *(GC38,  DA 635)*

Hakika Bwana hatafanya neno lolote bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake *(Amosi 3:7)* Ni kweli Mungu atawafunulia siri yake lakini siri ya Bwana iko kwao wamchao. Ni siri ya kufunuliwa mambo ya unabii kuelewa unabii wa Danieli na Ufunuo kwa wazi ndiko kunakonenwa hapa *(soma Yoeli 2:28-32, Matendo 2:16-20, Daniel 12:4,10 na Ufunuo 22:10.)* Hata hivyo pamoja na Mungu kumfunulia mwanadamu lakini kuna mambo ambayo mwanadamu hajafunuliwa. Ni mambo gani ambayo mwanadamu hajapewa tarehe siku yatakapotokea?

- Tarehe ya kufungwa kwa mlango wa rehema.
- Tarehe ya kumwagwa kwa mapigo saba duniani.
- Tarehe ambayo shetani atakuja akimwigiza Kristo .
- Tarehe ya kufa kwako.
- Tarehe ya kurudi kwa Yesu.
- Tarehe itakapokwisha miaka 1000 ya Ufunuo 20:7.
- Tarehe ambayo mji mtakatifu utashuka kutoka mbinguni kwa Mungu.

Pamoja na kwamba sisi hatumo gizani mpaka siku ile itujie ghafla *(1Wathesalonike 5:4)* bado kuna mambo mengine ni siri ya Mungu. Ikumbukwe kuwa hata kama Mungu angetoa tarehe mwezi na mwaka bado mwanadamu wa leo asingeelewa tarehe halisi ya kuja kwa kristo. Kujua hili kunahitaji hekima yenye upeo kupita lugha kutamka.

Jifunzeni unabii wa biblia muone jinsi unabii wa pembe ndogo ulivyotimia, kwa nini pia tarehe ya kuja kwake isingejulikana? Kwa sababu ya dhambi ya Yule mnyama wa nne wa Danieli sura ya saba. Dunia imechelewa kujua historia ya tawala za shetani zilizopita,mnyama alishaazimu kubadili majira na sheria toka siku nyingi sana, soma unabii wa *Danieli 7:1-25.*

Majira ya siku saa mwezi na miaka ya leo ni tofauti kulingana na Biblia.wenye dunia walishafanya kitu chao na dunia, tupo mwishoni mwa wakati zaidi kuliko tarehe tulipo sasa. Ni miaka mingi sana imepita ukilinganisha na tarehe ya leo unayoifahamu wewe. Waliokaririshwa uongo wanahitaji kukombolewa kifikra kwa kujisomea wenyewe historia ya unabii katika siku zetu. Tupo nyuma ya wakati kuliko hatari zilizo mbele yetu wakati huu ambapo falme za dunia zinafanya vita na Mwanakondoo.

Tusingeeleza mengi sana lakini nirudi tu kusema kuwa mambo ya siri ni ya Mungu wetu na mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele ili tuyafanye maneno yote ya sheria hii *(Kumbukumbu la Torati.29:29, Mithali 30:5-6)*

## DHEHEBU LA SHETANI

Mbweha wana pango na ndege wa angani wana viota lakini Mwana wa Adamu hana hata mahali pa kulaza kichwa chake *(Mathayo 8:20).* Alikuwa masikini kwa ajili yetu ili katika umasikini tuwe matajiri wa Roho *(2Wakorintho 8:9).* Ni kinyume kama nini kwa maaskofu na wachungaji na mapadre wa leo. Wengi ni matajiri wa kutisha kuliko hata BWANA wao.

Basi nawaambia, wakati utakapoona kiongozi wa dhehebu lako anaishi kwa anasa huku akikusanya sadaka kwa masikini na kuwahubiri watoe ili wabarikiwe ili yeye aendelee kuneemeka kwa kuchukua jasho la masikini huku akidai kumfuata Yesu, usijisumbue kutoa sadaka yako maana haiendi kwa Mungu. Huo ni wakati maalumu wa shetani kukusanya jasho la masikini kwa kutumia Biblia *(Mathayo 7:13-14)*

Utakapoona nyimbo zinazodaiwa za dini zimeanza kupendwa mpaka zikawa na mashabiki wanaoingia kwa kiingilio ufumbuke macho. Utakapoona nyimbo hizo zinapigwa mpaka sehemu za ulevi ambapo shetani ni makao yake ujue muungano wa dini na umizimu umekamilika kupitia muziki wa shetani maana kamwe nuru na giza havipatani. *(Amosi 3:3, 2Wakorintho, 6:14-16)*

Utakapoona dhehebu limeruhusu anasa na arusi za gharama kubwa kuliko Biblia ilivyoagiza, utakapoona vilio vya masikini yatima wajane na wagonjwa wanakosa mahitaji yao huku tabaka lingine katika dini linapoteza muda, mali, pesa kwa anasa na sherehe huku wanandoa wakipeana talaka muda mfupi baada ya kuoana, mambo

hayo yaonekanapo katika madhehebu ujue ukristo wa shetani umefikia kiwango kama kile kabla ya gharika *(Ezekieli16:49, Mathayo24:37-39.* Wakati utakapoona mwanamke ameanza kudai zile haki ambazo Mungu hakumpatia, atakapoanza kuingia kanisani na suruali kinyume na neon la Mungu, ukiliona jambo hilo usiingie katika dhehebu hilo.

Utakapoona mwanamke ameanza kuwa kiongozi kanisani na kuanza kufundisha, utakapokuta waumini wameanza kumfokea Mungu wakati wanaomba badala ya kunyenyekea, utakapoona katika kanisa watu wameanza kuomba bila kupiga magoti, hayo yote yatakapofanyika huku viongozi wakiwa kimya bila kuyakemea, ukiona nuru inapingwa sana badala ya kufuatwa, ujue sasa tayari upo katika dhehebu ambalo mapepo yanaongoza watu. Kuongezeka kwa maovu katika dini ni dariri ya mwisho dunia kuongozwa na mapepo *(Kumbukumbu la Torati 24:5, 1Petro 3:3-4. 1Wakorintho 14:34, 1Timotheo 2:9-12, 3:1-12. Mathayo 6:6, Danieli 6:10, Isaya 29:15-16, Warumi.9:2021, CW 172,IT578, Habakuki 2:18.)*

Utakapoona waprotestanti wamepoteza nuru yao na kuanza kuungana na kinyume na msimamo wa wanamatengenezo wa zamani ujue muda mfupi waaminifu wa neno la Mungu wataanza kuteswa, utakapoona wimbo wa Bwana unaimbwa *nchi ya ugeni*, utakapoona Roho ya Martin Luther, Stefano, Ellen G. White na roho ya Danieli haipo katika makanisa, utakapoona wengi wameanza kuwa matajiri kwa kuombea wagonjwa na wenye shida wakati Yesu hakupokea hata senti kwa kuombea watu, ukiyaona hayo usiingie katika dhehebu hilo hata kama kweli mtu aliyeombewa amepona. *(Kumbukumbu la Torati. 13:1-2, Isaya 8:20, TM260, 2T440, ufunuo 16:13-14,)*

Utakapoona kitabu chochote cha dini au bango lolote limetaja tarehe ya mwisho wa dunia kinyume na ulivyojifunza ujue hiyo ni njia ya shetani kunyakua akili za watu zitoke katika neno la Mungu. Utakapoona kiongozi wa serikali amekaribishwa kufungua mkutano au tamasha lolote la dini basi ujue muungano wa dini na serikali unatimilika. Epuka dhehebu lolote lenye waumini wengi *(Mathayo7:13-14, Isaya 42:22, Isaya 52:11)*

Mpinga Kristo yuaja hata sasa wapinga Kristo wengi wamekwisha kuwapo *(Yohana 2:18)* kwa maana kuna waliojiingiza kwa siri, makafiri, wabadilio neema ya Mungu kuwa ufisadi na kumkana Bwana wetu *(Yuda 1:4)*

Wachungaji wao ni mbwa bubu wasiobweka *(Isaya 56:10-11)* hawakupanda kupajenga mahali palipobomoka *(Ezekieli13:5)* manabii wao walitoa maneno laini ya amani yanayodanganya *(Isaya 30:6)*. Na hivyo kundi kubwa la watu wamekuwa mateka wa shetani maana wamepotezwa. Ndivyo walivyotiwa uchafu kwa kazi zao wakafanya uasherati kwa matendo yao. *(Zaburi 106:39)*

SURA YA KUMI NA SITA

# TUKUTANE MJINI

Kuja kwa Yesu Kristo mara ya pili kutasimamisha shughuli zote duniani. Kila kitu duniani kitakuwa kimesimama. Uzuri wa Dunia tunayoiona utatoweka punde wakati wa Mapigo saba yale ya Ufunuo 16:1-21 yatakapoiangukia Dunia. Kunakuja mapigo saba ambayo ni hasira za Mungu zisizochanganywa na huruma juu ya wanadamu waliochagua kusimama upande wa shetani na kumkiri kwa matendo yao kuwa ni baba yao. Mapigo hayo yatafanya dunia isiweze kukalika kwa sababu ya maumivu. Mwanadamu ataharibiwa kwa Majipu mabaya sana, Pigo la pili litamuongezea mateso mwanadamu baada ya Maji yote duniani kugeuzwa kuwa damu, naye atalazimika kunywa maji hayo ambayo yatakuwa na harufu mbaya kwa sababu viumbe vyote vya majini vitakuwa vimekufa humo. *(Ufunuo 16:2-3)*

Jua litapewa uwezo wa kuwaunguza wanadamu kwa joto, Wanadamu wataunguzwa vibaya sana, nao watalia kwa sababu ya maumivu hayo ya moto na Majipu *(Ufunuo 16:8-9)* Na tena nuru ya mwezi itakuwa kama nuru ya jua na nuru ya jua litaongezeka mara saba kama nuru ya siku saba katika siku ile Bwana atakapofunga mapigo ya watu wake na kuliponya pigo la jeraha yao *(Isaya 30:26)* Watu watatafuna ndimi zao kwa sababu ya maumivu hayo ambayo hayatakuwa na msaada.Historia ya mapigo ya Misri wakati wa utawala wa Farao kabla Israel hawajakombolewa inatuonyesha vile dunia itakavyokuwa wakati mapigo saba yatakapomwagwa duniani.

Kwa hakika wanadamu Watakaokutwa hai wakati huo watalaani ni kwa nini hawakufa mapema. Hakuna mwanadamu atakayemhuzunikia mwenzake, ni wakati ambao Mbingu zitakunjwa kama ukurasa na milima itasukwasukwa na kusogeleana huko na huko, vilima na visiwa vitahamishwa mahali pake kwa nguvu za Mungu. *(Ufunuo 6:14)* Matukio hayo yatafanya nyota zianguke kutoka Mbinguni kwa wingi. *(Ufunuo 6:12-13)* Wakati pigo la saba litakapomwagwa kutakuwa na umeme na sauti na radi, Kutakuwa na tetemeko kubwa Duniani ambalo halijawahi kutokea tangu Dunia kuumbwa. Na mvua ya mawe kubwa sana ya Mawe kama Taranta ikashuka kutoka Mbinguni juu ya Wanadamu. Wanadamu wataangukiwa na mawe makubwa sana nao hawatakuwa na mahali pa kukimbilia. Urembo wako unaojivunia bila Yesu utafikia tamati wakati huo. Mapambo yako yatapondwapondwa na mvua ya Mawe. Siku hiyo wanawali wazuri na wavulana watazimia kwa kiu.*(Amosi 8:13)*

Kichwa chako kitapondwapondwa kwa nguvu ya mawe makubwa kutoka juu, mawe hayo yataponda mwili wako wote bila huruma kuanzia Uso, Kifua, Miguu, Mikono na

viungo vyako vitapondwapondwa kwa nguvu bila huruma Maana ni siku ya kisasi cha Bwana atakapokulipa malipo.

Wingi wa mawe hayo pamoja na mfululizo wa mapigo mengine ndiyo utasimamisha shughuli zote Duniani. Magari hayatasafiri wa sababu barabara zitakuwa zimeharibiwa na mvua ya mawe.Ndege hazitaruka angani, Mawe hayo yatavunjavunja Minara ya mawasiliano yote Duniani. Hospitali hazitafanya kazi, vyombo vyote vya usafiri wa majini vitakuwa vimekwamishwa na mapigo hayo, Biashara zote duniani zitasimama na hakuna chochote kitakachokuwa kinafanyika duniani zaidi ya uharibifu. Polisi na Bunduki zao watapigwa na Mvua hii ya mawe hata wasiweze kutoa msaada wowote.Wakati huo wanadamu watakutwa wapo hoi kwa mapigo hayo, sura zao zitakuwa mbaya na miili yao itakuwa inanuka kwa sababu ya Majipu mabaya. Watu watakuwa wachafu kwa maana wataoga maji yaliyogeuzwa kuwa damu inayonuka sana Licha ya majipu mabaya waliyonayo. Mambo haya yapo karibu sana mbele yetu. Tena watajifungia nguo za magunia na utisho utawafunika na aibu itakuwa juu ya nyuso zote na upaa juu ya vichwa vyao vyote. Watatupa fedha yao katika njia kuu za mji na dhahabu yao itakuwa kama kitu cha unajisi. Fedha yao na dhahabu yao hazitaweza kuwaokoa siku ya ghadhabu ya Bwana. Hawatajishibisha roho zao, wala hawatajijaza matumbo yao kwa sababu zilikuwa kwazo la uovu wao. *(Ezekieli 7:17-19)*

Hiyo siku ya Bwana iliyo kuu i karibu, i karibu nayo inafanya haraka sana.Naam sauti ya siku ya Bwana shujaa hulia kwa uchungu mwingi huko! Siku ile ni siku ya ghadhabu na fadhaa na dhiki, siku ya uharibifu na ukiwa, siku ya giza na utusitusi, siku ya mawingu na giza kuu, siku ya Tarumbeta na ya Kamsa, juu ya Miji yenye maboma, juu ya Buruji zilizo ndefu sana. *(Sefania 1:17-19)* Kwa maana hiyo siku ya Bwana i karibu juu ya mataifa yote; kama ulivyotenda, ndivyo utakavyotendwa; malipo yako yatakurudia juu ya kichwa chako mwenyewe *(Obadia 1:15)*

Kelele milimani kama kelele za watu wengi sana; kelele za falme za mataifa waliokutana pamoja; Bwana wa majeshi anapanga jeshi kwa vita; watu waliotoka katika nchi iliyo mbali, tokea upande wa mwisho wa mbingu; naam, Bwana na silaha za ghadhabu yake, ili aiangamize nchi yote. Pigeni kelele za hofu; maana siku ya Bwana i karibu; itanyesha kama maangamizi yatokayo kwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hiyo mikono yote italegea, na moyo wa kila mtu utayeyuka. Nao watafadhaika; watashikwa na utungu na maumivu; watakuwa na utungu kama mwanamke aliye karibu na kuzaa; watakodoleana macho; nyuso zao zitakuwa ni nyuso za moto.Tazama, siku ya Bwana inakuja, siku kali, ya hasira na ghadhabu kuu, ili iifanye nchi kuwa ukiwa, na kuwaharibu watu wake, wenye dhambi, wasikae ndani yake. Maana nyota za mbinguni na matangamano havitatoa nuru yake; jua litatiwa giza wakati wa kucha kwake, na mwezi utaacha nuru yake isiangaze. Nami nitaadhibu ulimwengu kwa sababu ya ubaya wake,

na wenye dhambi kwa sababu ya hatia yao; nami nitaikomesha fahari yao wenye kiburi; nami nitayaangusha chini majivuno yao walio wakali; nitafanya wanadamu kuadimika kuliko dhahabu safi, na watu kuliko dhahabu ya Ofiri. Kwa hiyo nitazitetemesha mbingu, na dunia itatikiswa itoke katika mahali pake, kwa sababu ya ghadhabu ya Bwana wa majeshi, na kwa sababu ya siku ya hasira yake kali. *(Isaya 13:4-13)*

*Nami nitawaletea wanadamu dhiki hata watakwenda kama Vipofu kwa sababu wamemtenda Bwana dhambi, na damu yao itamwagwa kama mavumbi na nyama zao kama Mavi. Fedha yao wala dhahabu yao havitaweza kuwaokoa katika siku ile ya ghadhabu ya Bwana. Bali Nchi yote itateketezwa kwa moto wa Wivu wake, maana atawakomesha watu wote wakaao katika Nchi, naam kwa ukomo wa kutisha (Sefania 1:17-18)*

Jikusanyeni,naam jikusanyeni ee Taifa lisilo na haya, kabla haijazaa hiyo Amri, kabla haijapita siku ile kama makapi, kabla haijawajilia hasira kali ya Bwana. Mtafuteni Bwana enyi nyote mlio wanyenyekevu, itafuteni haki, utafuteni unyenyekevu, huenda mtafichwa katika siku ya hasira ya Bwana *(Sefania2:1-3)*

Lakini mbingu za sasa na nchi za sasa zimewekwa akiba kwa moto kwa neno hilohilo zikilindwa hata siku ya hukumu na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu. Siku ya Bwana itakuja kama mwivi, katika siku hiyo Mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa na Nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea, *(2Petro 3:7,10)* Hivi ndivyo Dunia hii unayoipenda sana itakavyokoma . Utakuwa ndiyo mwisho wa Utajiri na Umasikini.Matabaka yaliyopo duniani yatakoma. Utandawazi na sera zake zilizokandamiza maelfu utakuwa umekoma.

Ndipo itakapoonekana ishara ya Mwana wa Adamu Mbinguni, Ndipo Mataifa yote ya ulimwengu watakapoomboleza, nao watamuona Mwana wa Adamu akija juu ya Mawingu ya Mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi, naye atawatuma Malaika zake pamoja na sauti ya Parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa Mbingu mpaka mwisho huu *(Mathayo 24:30-31)*

Kwa dakika moja kufumba na kufumbua wakati wa parapanda ya mwisho, maana parapanda italia na Wafu watafufuliwa wasiwe na uharibifu nasi tutabadilika. Maana sharti huu wa kuharibika uvae kutokuharibika nao huu wa kufa uvae kutokufa. Basi huu uharibikao utakapovaa kutokuharibika na huu wa kufa utakapovaa kutokufa, hapo ndipo litakapokuwa lile neno lililoandikwa, Mauti imemezwa kwa kushinda, Ku wapi ewe Mauti kushinda kwako? U wapi? ewe Mauti uchungu wako? Uchungu wa Mauti ni dhambi na nguvu za dhambi ni Torati. (*1Wakorintho 15:52-56)* Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka Mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya Malaika Mkuu na Parapanda ya Mungu nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza kisha sisi tulio hai

tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani na hivyo tutakuwa na pamoja na Bwana milele.(*1Wathesalonike 4;16-17)*

MAKUNDI MAWILI YA WANADAMU

Wakati huo wanadamu watakuwa katika makundi mawili tu duniani, kundi moja ni hili litakalokutwa halikujiandaa kiroho hivyo kupotea na kupata aibu na kudharauliwa milele, kundi la pili ni lile litakalonyakuliwa na Bwana wakati wa kuja kwake, kundi hili ni lile lililofuata mapenzi ya Mungu na kupita njia nyembamba, ni kundi ambalo lilimfuata mwanakondoo kila aendapo, watu waliopo katika kundi hili wanasifa za kufanana na Kristo kwa sababu wakati wakiwa duniani maisha yao yalithibitisha kuwa:-

1. Walimfuata Mungu na kumuweka mbele bila kujali kitu chochote.
2. Wanashika amri za Mungu kwa Matendo.
3. Maisha yao hayana mawaa wala kasoro.
4. Walinyenyekea kwa Yesu naye akawaongoza.
5. Hawakuchafuliwa na mivuto ya dunia hii.
6. Mavazi na tabia zao vilimtangaza Mungu.
7. Walivaa silaha zote za Nuru.
8. Walijitenga na Madhehebu yote yaliyoasi.
9. Walifanya matengenezo ya Afya na vyakula.

10. Walivumilia usaliti wa kiroho waliofanyiwa na Ndugu zao.

Ndipo Yesu atawakaribisha kwake na kuwaambia, njooni mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa kwa ulimwengu kwa maana nalikuwa na njaa mkanipa chakula, nalikuwa na kiu mkaninywesha, nalikuwa mgeni mkanikaribisha, nalikuwa uchi mkanivisha, nalikuwa mgonjwa mkaja kunitazama, nalikuwa kifungoni mkaja kunitazama. "Sote tukaingia winguni pamoja tukapaa siku saba kwenda kwenye bahari ya kioo, wakati Yesu alipozileta taji kwa mkono wake mwenyewe alituvika vichwani mwetu,Wengine walikuwa na nyota nyingi huku wengine wakiwa na nyota chache tu, wote waliridhika kabisa na taji hizo na walivikwa vazi jeupe la utukufu kutoka mabegani mwao hadi chini miguuni mwao, Malaika walituzunguka pande zote tukitembea juu ya bahari ya kioo kwenda langoni mwa Mji. Yesu akainua mkono akashika milango ya Lulu na kutuambia, mmeyafua mavazi yenu katika damu yangu mkasimama imara kuitetea kweli yangu ingieni, sote tukaingia kwa taratibu na kujiona tulikuwa na haki ya kuingia Mjini.

Hapo tukauona mti wa uzima na kiti cha enzi cha Mungu, katika kiti hiki cha enzi kukatoka mto wa maji safi, kila upande wa mto huu palikuwa na mti wa uzima sote tukaenda chini ya mti huu na kuketi kuangalia utukufu wa mahali hapa. Tulijaribu kukumbuka taabu zetu kubwa kabisa za duniani lakini zilionekana kuwa ni ndogo sana

zikilinganishwa na utukufu mwingi wa milele uzidio sana uliotuzunguka, nasi tukapaza sauti, haleluya! Mbinguni ni rahisi na ya kutosha, nasi tukavigusa vinubi vyetu vizuri mno na kuifanya Mbingu kurudisha mwangwi. Ni wito wa pekee kwa kila mwanadamu kuwa usikose kuwepo pale mbinguni!, ni Nchi nzuri ambayo tumendaliwa wapendwa. Unakaribishwa uingie huko, tumechoka kuishi katika dunia hii ya mateso, tumechoka kulia na kuomboleza. Dunia hii si chochote ukilinganisha na Mbingu mpya na Nchi mpya ambayo watakatifu watakaa, ni Nchi nzuri mno ing'aayo ambayo jua la haki litawazukia lenye kuponya katika mbawa zake, nanyi mtatoka nje na kuchezacheza kama Ndama wa Mazizini. (Malaki 4:2)

Tutawaona wapendwa wetu waliokufa katika Bwana tukijuana nao na kusalimiana, Tutamwona Yesu uso kwa uso aliyetukomboa, Kutakuwa kukutana ajabu tutakapoungana na Ndugu zetu wema tukionana na Mungu tena uso kwa uso.

Tutamwona Adamu Yule wa kwanza kuumbwa, tutakula naye na kuulizana maswali tukisimuliana jinsi Yesu alivyotukomboa.Edeni mpya itarudishwa, Edeni iliyopotea itarudishwa, tutavikwa asili ya utukufu ule uliopotea, Lugha za kibinadamu hazitoshi kueleza bustani ya Edeni ilivyokuwa. Uzuri wa binadamu Yule wa kwanza hauwezi kueleweka kwa kutumia lugha hizi hafifu za Mnara wa Babeli. Hata hivyo nitajaribu kidogo kuelezea uzuri ule wa Edeni iliyopita ili angalau upate picha ya uzuri wa Edeni mpya ya Mbinguni na jinsi paradiso tuliyoandaliwa itakavyokuwa na kukualika Mpendwa kuwa, kwa kweli hupaswi kuikosa!,Vuta usikivu kuanzia hapa.

Mwanadamu alipotoka mikononi mwa Muumba wake alikuwa mwenye umbo kubwa lililo na uwiano sawa, muonekano wake wa uso ulikuwa na afya ukiwa na nuru ya maisha na furaha. Akili yake ilikuwa na uwezo wa kuelewa mambo ya Mbinguni, alikuwa Mtakatifu na mwenye furaha.Urefu wa Adamu ulikuwa ni zaidi ya Wanaume wanaokaa duniani leo. Hawa alikuwa na Umbo dogo kiasi hata hivyo Umbo lake lilikuwa bora na lililojawa na uzuri. Wawili hawa wasio na dhambi hawakuvaa nguo za kutengenezwa ila walifunikwa kwa nuru ya utukufu kama ule wanaovaa Malaika. Kadri walivyoishi katika utii kwa Mungu Nguo hii ya nuru iliendelea kuwafunika. Hawa aliumbwa kutoka katika ubavu wa Adamu ikimaanisha kwambahakupaswa kumtawala Adamu kama kichwa wala kumkanyaga chini ya miguu yake kama aliye duni bali kuwa naye pembeni akipendwa na kulindwa naye . (*PP45-46)*

Kama vile Adamu alivyotoka katika mkono wa muumba wake, alikuwa mrefu mwadilifu na mwenye uzuri linganifu. Yeye alikuwa mrefu zaidi ya mara mbili ya watu wanaoishi sasa duniani na mwenye uwiano sawa. Sehemu za uso wake zilikuwa kamili na nzuri. Sura yake siyo nyeupe wala njano nyeupe lakini yenye afya iking'aa kwa utajiri wa rangi ya afya. Hawa hakuwa mrefu kama Adamu, kichwa chake kilifika kidogo tu juu ya

mabega ya Adamu naye pia alikuwa na umbo nadhifu kamilifu linalolingana na alikuwa mzuri mno! *(3SG34)*

Dunia ilikuwa tambarare yenye vilima vidogovidogo kamaVichuguu. Uso wake ulipambwa na majani mazuri ya kijani kibichi, wakati wote hakuna hata jani lolote lililonyauka, hata hivyo majani haya hayakufanya Misitu kukua bila utaratibu, lakini yalikuwa kana kwamba yanafyekwa ingawa hakuna aliyefanya kazi hiyo.Mabonde makubwa kama bustani yalikuwa yamejaa mimea ya kijani, Harufu nzuri ya Maua hayo ilikuwa ni marashi ya pekee yaliyonukia bila kuikaribia. Vilima vilikuwa na miti mikubwa ikiwa na matawi yaliyojaa Zabibu, matunda ya nchi yalikuwa mengi yakipatikana wakati wote, miti iliyokuwepo ilijazwa na sauti za Ndege waliokuwa hawajui kiangazi wala masika na walishiba miaka yote kwa matunda yaliyokuwa yametapakaa kila mahali. Misitu naVichaka vilijazwa na wanyama wazuri wa kila aina ambao hawakuwa na mlaji. Dhahabu, Lulu, Almasi na madini mengine vilikuwa vimetapakaa juu ya uso wa Nchi.(*PP90)*

Watu walioishi nyakati hizo waliweza kuishi zaidi ya miaka mia nane kwani hewa waliyokuwa wanavuta ilikuwa nzuri na safi mno, hakukuwa na viwanda wala Magari yaliyotoa moshi, nao walilala mahali pa wazi bila kujifungia usiku kwani hakukuwepo na wezi, kwa ujumla Maisha yao yalikuwa mazuri na rahisi, watu walifanya kazi kidogo na kuvuna Mazao tele.

Ulimwengu wa wakati ule kabla dhambi haijaingia ni mfano wa ulimwengu ujao wakati dhambi itakapokoma. Kutakuwa na Mbingu mpya na Nchi mpya ambazo Yesu alikwenda kuandaa, Yesu alisema nakwenda kuwaandalia mahali, mimi nikienda kuwaandalia mahali nitakuja tena niwakaribishe kwangu ili nilipo mimi nanyi muwepo *(Yohana 14:1-3)*

Kisha nikaona Mbingu mpya na Nchi mpya maana Mbingu za kwanza na Nchi za kwanza zimekwisha kupita *(Ufunuo 21:1)* Nami nikauona Mji ule mtakatifu Yerusalemu mpya ukishuka kutoka Mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari kama bibi arusi aliyekwisha kupambwa tayari kukutana na Mume wake, naye atafuta kila chozi katika Macho yao wala mauti haitakuwapo tena wala maombolezo wala kilio wala maumivu hayatakuwepo tena kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita. (*Ufunuo21:1-4)* Yesu atasisimika ufalme wa milele ambao hautakomeshwa.

Na wewe Mnara wa kundi kilima cha binti Sayuni utajiliwa, naam mamlaka ya kwanza yatakuja. *(Mika 4:8)* Ufalme ule wa kwanza uliokuwa umepotezwa utarudi, wenye haki watairithi nchi nao watakaa humo milele *(Zaburi 37:29)* Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu yafanyeni imara magoti yaliyolegea waambieni walio na moyo wa hofu, jipeni moyo

msiogope tazama Mungu wenu atakuja na kisasi na malipo ya Mungu atakuja na kuwaokoa ninyi. Ndipo macho ya Vipofu yatafumbuliwa na masikio ya Viziwi yatazibuliwa, ndipo mtu aliye kilema atarukaruka kama Kulungu na ulimi wake aliye bubu utaimba maana katika nyika maji yatabubujika na vijito jangwani.Wala hapana mwenyeji atakayesema mimi mgonjwa.*(Isaya 35:3-6,33:24)*

Bwana asema, furahini mkashangilie daima, kwa ajili ya hivi niviumbavyo, maana tazama naumba Yerusalemu uwe Shangwe na watu wake wawe furaha, nami nitaufurahia Yerusalemu nitawaonea shangwe watu wangu, sauti ya kulia haitasikiwa ndani yake tena wala sauti ya kuomboleza, nao watajenga nyumba na kukaaa ndani yake. Hawatajenga akakaa mtu mwingine ndani yake, hawatapanda akala mtu mwingine. Maana kama siku za mti ndivyo zitakavyokuwa siku za watu wangu,na wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi.*(Isaya 65:18-25)*

Oo, utakuwa Utukufu jinsi gani kumuona yeye na kukaribishwa kama waliokombolewa!, tumengoja kwa muda mrefu lakini tumaini letu halipaswi kufifia, kama tungeweza tu kumuona Mfalme katika uzuri wake tutabarikiwa milele. (*8T253)* Katika siku hiyo waliokombolewa watang'aa katika utukufu wa Baba na Mwana. Malaika wakivigusa vinubi vyao vya Dhahabu watamkaribisha Mfalme na Nyara zake za ushindi na wale ambao wameoshwa na kufanywa weupe katika Damu ya Mwanakondoo. Wimbo wa ushindi utatoa sauti na kuijaza Mbingu yote. Atayaingia makao ya Mbinguni akifuatana na waliokombolewawalio mashahidi kwamba utume wake, mateso, na kafara yake havikuwa bure. *(9T285-286)*

Tuliokombolewa tutakapopaa na Yesu tutakuwa naye milele. Furaha iliyoandaliwa katika makao ya huko hupaswi kuikosa, kaza mwendo safisha uchafu wa Roho, tengeneza njia ili roho Mtakatifu afanye makao kwako. Makao mapya yameandikwa kwa ajili yako. Mwaliko huu unamhusu kila mwanadamu. Katika mwaliko wa kuurithi uzuri wa Edeni mpya ya Mbinguni si salama kukawia maana unaweza usiusikie tena. Wale wanaofunga makomeo ya milango ya Mioyo yao na kupuuza mwaliko huu, wanatupilia mbali bahati yao ya pekee iliyoandaliwa kwa ajili yao. Ninakusihi kwa jina la Mwenyezi Mungu toka gizani njoo nuruni uone wema wa Yesu katika mji mpya ulioandaliwa. Wengi watashupaza shingo zao na kusitasita kama mke wa Lutu hata wachelewe. Wale wanao ng'ang'ania dini za mababu zao na madhehebu yaliyopotoka watajikuta wamechelewa kupaa na Yesu winguni. Wakiwa katika moto wa jehanamu wataikumbuka bahari ya kioo waliyoikosa kwa sababu waliipenda dunia na anasa zake,

Enyi watu nawaita ninyi na sauti yangu ni kwa Wanadamu, kwa kuwa bado kitambo kidogo yeye ajaye atakuja wala hatakawia, lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani naye akisitasita Roho yangu haina furaha naye. *(Waebrania 10:37-38)* Tumechoshwa na

kelele za maombolezo na huzuni zilizojaa duniani, tunatamani furaha na vigelegele ambavyo punde washindi watavisikia, tumechoshwa na sauti za mabomu na milio ya bunduki inayoogopesha uhai wa sayari hii, tunaitamani milio na sauti za vinubi ambavyo washindi watapiga kwa shangwe. Tunaitamani nchi ile ambayo watu wake watavikwa miili ile ya kutokufa isiyozeeka. Tafadhali Toka gizani njoo ujiunge na hoihoi za washindi zilizokaribu.

Hii ni taarifa ndogo tu ya vichala vichache toka Kaanani ya Mbinguni ambayo kwavyo wengi wangetamani kuingia, nami nakuambia, ni Nchi nzuri sana na tunaweza kabisa kupanda na kuimiliki, waliokombolewa watang'aa katika utukufu wa Baba na Mwana. Wimbo wa ushindi utaimbwa, Malaika watapiga Vinubi vyao na kuimba nyimbo za ukombozi wakimsifu Mfalme Immanueli atakapowakaribisha wale ambao wameoshwa na kufanywa weupe kwa damu ya Mwanakondoo.

Kabla ya kuingia Mjini Mwokozi atawatunuku wafuasi wake namba za ushindi na kuwavisha tepe ya kifalme. Hakutakuwa na mtu jeuri wala mkorofi, kila kitu kitakuwa bora ajabu, Mfalme wa Mbinguni atatawala dola hii yenye nguvu ambayo hushindana tu katika mema wakitafuta furaha na raha wao kwa wao. Katika mji huo furaha na Pendo vitatawala daima, huko pazia ambalo huyatiagiza macho yetu litaondolewa na macho yetu yatakapotazama ulimwengu ule mzuri ambao sasa tunaona kidogo tu kwa darubini ya kinabii, wakati tutakapotazana juu ya utukufu wa Mbingu zote ambazo sasa tunaziangalia kwa mbali, wakati uharibifu na dhambi vitakapondolewa, dunia yote itaonekana katika uzuri wa ajabu!!. Hazina zote za ulimwengu zitafunguliwa kwa ajili ya kujifunza watoto wa Mungu, tutaingia katika ndelemo na hekima ya viumbe ambao hawakuanguka dhambini, tutashiriki hazina zilizopatikana kwa vizazi na vizazi ambazo zilitumiwa kufikiri juu ya kazi za mikono ya Mungu. (*ED301,303)*

Hakuna atakayepumzika wala kuchoka, Katika mji huo kila mmoja atatukuza jina la Kristo na kutenda mapenzi yake. Tukutane katika mji huo ndio wito wangu kwenu.*Tukutane mjini* ambako hakuna kufa wala kuzeeka, Tusipoonana hapa *duniani basi na tukutane mjini Mbinguni* ambako tutashangilia utukufu wa mahali pale. Na miaka ikizidi kupita tutaendelea kuyavumbua mambo makuu zaidi juu ya Mungu. Kadri ujuzi utakavyoongezeka ndivyo tutakavyozidi kumpenda Mungu mwenye Enzi.

Na kila kiumbe kilichoko Mbinguni juu ya Nchi na chini ya Nchi na juu ya bahari na vitu vyote vilivyomo ndani yake nalivisikia vikisema Baraka na heshima na Utukufu na Uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha Enzi na yeye Mwanakondoo hata milele na milele *(Ufunuo5:13)* Kiini cha ukombozi kitatumika kwa mioyo na mawazo na ndimi za waliokombolewa kupitia vizazi vya milele. Wanadamu watafahamu ukweli ambao Kristo alitamani kuufunua kwa Wanafunzi wake lakini wao wakawa hawana imani

kuyapokeayatakayoonekana. Kwa zama za milele waaminifu watatoa katika hazina *ya Mungu*vitu vipya na vya kale. *(COL134)*

Kutakuwa na Muziki huko na Nyimbo, Muziki na nyimbo kama hizo isipokuwa kwa njozi ya Mungu hakuna sikio linalokufa lililopata kusikia nyimbo ambazo waliokombolewa wataimba! Lugha za kibinadamu hazitoshi hata kujaribu kusimulia jinsi Mbingu ilivyo. Uzuri wa Nchi ile utaeleweka tu kwa wale watakaoiona, kama nikiwaza mambo haya nashangaa na kuvutwa moyoni kwa Utukufu. Naiweka kalamu chini nikifikiri ninachelewa kuiona maana vitu vyote vya duniani hapa huonekana vibaya na vya kutia huzuni sana. Nikikumbuka matunda ya mji ule pamoja na malaika wale wanaozunguka kiti cha enzi najiona hali ya upweke sana maana kuna Nchi nzuri sana imeandaliwa kwa ajili yako. Laiti kama ningekuwa na mabawa kama Njiwa ndipo ningeruka mbali juu, juu zaidi na kukaa huko katika raha. Roho na bibi arusi wasema njoo! Naye asikiaye na aseme njoo, naye mwenye kiu na aje, Naye atakaye na ayatwae Maji ya uzima bure *(Ufunuo 22:17*) Tokea vizazi vyote vyenye mawazo yanayokufa vimekuwa vikitafuta kufahamu siri ya upendo usioweza kufahamika, Hatimaye vitashangaa na kuabudu.

UFUNUO 14:6-12

# AMRI ZA MUNGU NA IMANI YA YESU

AMRI ZA MUNGU NA IMANI YA YESU

AMRI ZA MUNGU NA IMANI YA YESU

## VITABU VYA REJEA

Biblia na Roho ya Unabii ni kitu kimoja. Biblia inamrudisha mwanadamu kwa Mungu na Roho ya Unabii inamrudisha mwanadamu kwenye Biblia. Roho ya Unabii ni ushuhuda wa Yesu uliotumwa kwa Manabii waliovuviwa ambao walikuwa na sifa zote za kuitwa Manabii. Nabii hachaguliwi na watu wala yeye hapangi kuwa nabii bali Mungu humteua.

Nabii Ellen G. White (1827-1915) ndiye Nabii wa mwisho ambaye Mungu alimtumia mara tu baada ya zama za giza . Wale waliokosa vitabu vyake wanakosa nuru ya mwisho ya rehema ambayo ingewaangazia wakati huu ambao giza la kiroho limeyafunika madhehebu. Kamwe Biblia na Roho ya Unabii havipingani.

Wale wanaojishughulisha kusoma vitabu wanachimbua udongo wa maarifa yenye thamani isiyokadilika. Hatimaye wataikuta hazina iliyositirika ambayo wavivu wa kusoma hawawezi kuifikia. Wanaosoma vitabu nuru ya maarifa itawazukia na kuwafanya weupe katika akili zao. Usomaji vitabu hupunguza uwezo wa kutenda mabaya.

Nguvu ya kutenda mema inapatikana kwa kusoma vitabu. Kadri unapovikosa vitabu hivi uwezo wa kupambanua nuru na giza utapungua. Kadiri unavyoacha kusoma vitabu ndivyo uwezo wa kutenda mabaya unavyoongezeka.

Kuna maelfu ya mitego imetuzunguka mpaka sasa ambayo tutashinda tu ikiwa tutasoma vitabu. Ushindi upo kwa wale tu wanaotaka kulipia gharama yake. Mungu, Malaika na Jeshi lote la Mbinguni wangependa kuona kuwa hazina takatifu iliyofichwa vitabuni inachimbuliwa kikamilifu. Kadri macho yako yanavyoona nuru ya jua nafasi ya pekee ya kusoma bado ingalipo. Tafuta ushindi maadam macho, miguu na mikono yako ina nguvu.

AA Acts of Apostles

AH Adventist Home

CD Counsels on Diet and Foods

CG Child Guidance

CH Counsels on Health

COL Christ Object Lessons

CM Colporteur Ministry

CSSW Counsels on Sabbath School Work

CT Counsels to Parents Teachers and Students

DA Desire of Ages

ED Education

EV Evangelism

EW Early writings

FE Fundamentals of Christian Education

GC Great Controversy

GW Gospel Workers

LS Life Sketches

MH Ministry of Healings

MM Medical Ministry

IMR Manuscript Release. *(Volume 1-19)*

MYP Message to Young People.

PK Prophets and Kings.

PP Patriarchs and Prophets.

RC Reflecting Christ

SM Selected Message. *(Volume.1,2 and 3)*

T Testimonies for the Church. *(Volume 1,2,3,4,5,6,7,8,and 9 )*

TM Testimonies to Ministers.

UP The Upward Look.

WM Welfare Ministry.

Te Temperance.




"Hii ni taarifa ndogo tu ya vichala vichache toka Kaanani ya Mbinguni ambayo kwavyo wengi wangetamani kuingia.

Nami nakuambia, ni Nchi
nzuri sana nasi tunaweza
kabisa kupanda na kuimiliki.
Waliokombolewa watang'aa
katika utukufu wa Baba na
Mwana. "